# TASWIRA YA MALEZI YA WATOTO KATIKA RIWAYA ZA *TUMAINI* (2006) *NA DUNIA MASHAKA MAKUU* (2004)

**NA**

**AGNES KANANU MWENDA**

**C50/CE/26040/2011**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA ILI KUTOSHELESHA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI.**

**MACHI, 2020**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu kingine.

--------------------------------- 3/3/2020

AGNES KANANU MWENDA TAREHE

C50/CE/26040/2011

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

--------------------------------- 3/3/2020

DKT. PAMELA, M.Y. NGUGI TAREHE

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

--------------------------------- 3/3/2020

DKT. JOSEPH NYEHITA MAITARIA TAREHE

IDARA YA LUGHA NA FASIHI

CHUO KIKUU CHA KARATINA



ii

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu Silas Mwenda na Lucy Kangai, mume wangu Naftaly Kathurima na mwanangu Rawlings Muturi. Uvumilivu wenu na ushauri mlionipa ulinipa ari ya kukamilisha kazi hii.

# SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, afya njema na kuniwezesha kufika kiwango hiki cha elimu. Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Pamela Ngugi na Dkt. Joseph Maitaria kwa uvumilivu wenu, uelekezi mwema na ushauri bora. Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili kwa mwongozo na ushauri walionipa nilipohitaji msaada wao.

Aidha, nawashukuru wanafunzi wote tulioanza safari hii: Rachel Kathure, Joanta Ireri, Asenath Kebaso, Charles Sereti, Lucy Kamba na Chokera Kithinji. Tulisaidiana na kuhimizana wakati wa kufanya kazi hii. Mungu awabariki.

Vilevile, ningependa kushukuru familia yangu kwa kunitia moyo kila nilipofanya kazi hii. Pia, ningependa kuwashukuru ndugu zangu Fridah Kawira, Hellen Kaimuri, Joy Gatwiri na Stella Mukethi. Mlinifaa kwa hali na mali nipokuwa nikishughulikia kazi hii. Asanteni sana.

## IKISIRI

Utafiti huu unalenga kuchunguza taswira ya malezi ya watoto katika riwaya mbili za Kiswahili ambazo ni: *Tumaini* ya Clara Momanyi (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* ya Lamin Omar (2004*)* Malezi ya watoto ni mambo halisi yanayoikumba jamii ya kisasa ambayo inapitia mabadiliko mengi. Mabadiliko haya huwa ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidini na kiteknolojia. Waandishi wa riwaya huteua masuala yenye mguso kwa jamii na kuyasimulia kwa kiwango cha juu cha ubunifu. Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo: Ni mbinu zipi za malezi zinazobainika katika riwaya teule? Ni asasi na hali gani zinazochangia katika malezi ya watoto? Mbinu za malezi zina athari gani kwa watoto katika riwaya teule? Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo: Kueleza aina ya malezi yanayobainika katika riwaya teule, kubainisha asasi na hali za jamii zinazochangia katika malezi ya watoto katika riwaya teule na kueleza athari za mbinu za malezi zinazobainika katika riwaya teule. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia ya Gustave Flaubert (1850). Baadhi ya waitifaki wa nadharia hii ni Rene wellek (1960), Hegel (1971) na Lukacs (1979). Nadharia ya uhalisia inaeleza kuwa kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira. Baadhi ya mihimili ya nadharia hii ni: Matukio yanayosimuliwa sharti yawe yanatokea katika ulimwengu halisi, kazi ya msanii inapaswa kuonyesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao na jinsi wanavyohisi na kutenda wanapokumbana na hali Fulani na wahusika huwa halisi na lugha wanayotumia huwa rahisi. Huku mtafiti akiongozwa na mihimili ya nadharia alihakiki riwaya zilizoteuliwa ili kupata data iliyotoshelesha mahitaji ya utafiti huu. Uteuzi wa sampuli ulitumika na riwaya mbili ziliteuliwa: *Tumaini* ya Clara Momanyi (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* ya Lamin Omar (2004). Riwaya hizi zilitupa data faafu katika utafiti huu. Utafiti huu ulifanywa maktabani. Mtafiti alisoma kwa kina vitabu vya fasihi, majarida na tasnifu zilizoandikwa awali ili kufanikisha kazi yake. Data iliyopatikana ilichanganuliwa kulingana na malengo na maswali ya utafiti pamoja na mihimili ya nadharia. Data iliwasilishwa kwa maelezo katika sura tano. Utafiti huu umekusudiwa kuwafaa wanafunzi, walimu, wahakiki na waandishi wengine katika kubainisha umuhimu wa kuwapa watoto malezi mema. Pia, utawafaidi walezi na jamii kwa jumla.

## ABSTRACT


### PORTRAYAL OF PARENTING IN TWO SELECTED KISWAHILI NOVELS NAMELY: *DUNIA MASHAKA MAKUU* (2004) AND *TUMAINI* (2006)

This research investigates how parenting is portrayed in two selected Kiswahili novels namely: *Tumaini* (2006) by Clara Momanyi and *Dunia Mashaka Makuu* (2004) by Lamin Omar. The present society is going through many changes in the social, economic, political, technological and religious domain. All these changes affect children and the society at large. The contemporary novel writers address issues affecting the society in a creative way. This research was guided by the following questions: What are the styles of parenting reflected in selected novels? Which institutions and situations influence parenting in selected novels? What are the effect of different ways of parenting in selected novels? The objectives of this research were to analyze different styles of parenting as reflected in selected novels, to analyze various institutions and situations in the society that influence parenting and to examine the effects of parenting styles on children in selected novels. This research was guided by the tenets of realism theory of Gustave Flaubert (1850). Rene Wellek (1960), Hegel (1971) and Lukacs (1979) are among the researchers who have contributed to this theory. This theory stresses on the depiction of contemporary life and society as it exists. The major tenets of this theory include: Literary writers represent familiar things as they are, authors depict everyday activities and experiences instead of stylized presentation, literary work shows the feeling of characters and their solutions when faced by certain problems and the characters used by writers are real and they use simple language. Purposive sampling was used; two modern Kiswahili novels were selected: *Tumaini* (2006) by Clara Momanyi and *Dunia Mashaka Makuu* (2004) by Lamin Omar. Data was collected in the library. The researcher embarked on reading books, novels, journals, magazines and thesis. Data that was obtained was analysed based on the research objectives, questions and theories. Data was presented by discussion method. This research will benefit students, teachers, critics and other authors in demonstrating the role of parents in child development. It will also be beneficial to citizens and the society in comprehending their role in parenting.

## MAELEZO YA ISTLAHI MUHIMU

**Mtoto:** Mtu mwenye umri mdogo, aliye chini ya miaka kumi na minane. Anayetegemea wazazi na walezi kwa mahitaji ya kila siku. Katika muktadha huu tulilenga watoto wa miaka kumi hadi kumi na minane.

**Malezi:** Njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki.

**Uhalisia:** Kueleza hali au jambo jinsi lilivyo kwa uyakinifu

**Utamaduni**: Ni namna maalum ya maisha ya jamii mahsusi.

**Itikadi**: Ni mfumo wa mawazo na maadili yaliyopendekezwa na jamii ili kuwaongoza wanajamii.

**Asasi**: Kitengo maalum cha kijamii chenye kuelekeza jamii. Kwa mfano, familia, dini, utamduni n.k

## YALIYOMO

**IKIRARI** ........................................................................... Error! Bookmark not defined.
**TABARUKU** ........................................................................... **iii**
**SHUKRANI** ........................................................................... **iv**
**IKISIRI** ........................................................................... **v**
**ABSTRACT** ........................................................................... **vi**
**MAELEZO YA ISTLAHI MUHIMU** ........................................................................... **vii**
**SURA YA KWANZA** ........................................................................... **1**
**UTANGULIZI** ........................................................................... **1**
1.0 Usuli wa Mada ........................................................................... 1
1.1 Suala la Utafiti ........................................................................... 3
1.2 Maswali ya Utafiti ........................................................................... 4
1.3 Malengo ya Utafiti ........................................................................... 5
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ........................................................................... 5
1.5 Upeo na Mipaka ........................................................................... 6
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........................................................................... 7
1.6.1 Tafiti za Kishosholojia ........................................................................... 7
1.6.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Malezi ya Watoto Katika Fasihi ........................................................................... 9
1.7 Misingi ya Nadharia ........................................................................... 14
1.8 Mbinu za Utafiti ........................................................................... 18
1.8.0 Utangulizi ........................................................................... 18
1.8.1 Muundo wa Utafiti ........................................................................... 18
1.8.2 Mahali pa Utafiti ........................................................................... 18
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli ........................................................................... 19
1.8.4 Ukusanyaji wa Data ........................................................................... 19
1.8.5 Uchanganuzi wa Data ........................................................................... 19
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti ........................................................................... 20
**SURA YA PILI** ........................................................................... **22**
**MBINU MBALIMBALI ZA MALEZI YA WATOTO KATIKA RIWAYA TEULE** ........ **22**
2.0 Utangulizi ........................................................................... 22
2.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ........................................................................... 23

2.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Tumaini* (2006) ..... 26
2.3 Mbinu za Malezi ya Watoto Katika Riwaya Teule ..... 30
2.3.1 Malezi ya Kimabavu ..... 31
2.3.2 Malezi ya Kimamlaka ..... 35
2.3.3 Malezi ya Kudekeza. ..... 38
2.3.4 Malezi ya Kutojihusisha ..... 40
2.3.5 Malezi ya Ushirikiano ..... 42
2.3.6 Hitimisho ..... 46
**SURA YA TATU ..... 48**
**ASASI NA HALI ZINAZOCHANGIA KATIKA MALEZI YA WATOTO ..... 48**
3.0 Utangulizi ..... 48
3.1 Asasi ya Kitamaduni ..... 49
3.2 Asasi ya Familia na Ndoa ..... 53
3.3 Asasi ya Elimu ..... 57
3.4 Hali ya Jinsia na Uana ..... 61
3.5 Hali ya Hadhi/ Cheo ..... 65
3.6 Hali ya Ubinafsi na Tamaa ya Wahusika. ..... 69
3.7 Hali ya Taasubi ya Kiume ..... 71
3.8 Hali ya Kiuchumi ..... 72
3.9 Hali ya Ulevi ..... 74
3.10 Hitimisho ..... 76
**SURA YA NNE ..... 77**
**ATHARI ZA MBINU ZA MALEZI KATIKA RIWAYA TEULE ..... 77**
4.0 Utangulizi ..... 77
4.1 Utengano katika Familia ..... 78
4.2 Mimba na Ndoa za Mapema kwa Wasichana ..... 81
4.3 Wizi na Watoto Kufungwa Jela ..... 84
4.4 Utovu wa Nidhamu ..... 87
4.5 Watoto kukumbwa na Maradhi ..... 90
4.6 Matumizi ya Dawa za Kulevya ..... 91
4.7 Kuzorota kwa Elimu ..... 93

4.8 Majuto kwa Wazazi ........ 97
4.9 Watoto kutamauka ........ 98
4.10 Hitimisho ........ 101
**SURA YA TANO ........ 102**
**HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ........ 102**
5.0 Utangulizi ........ 102
5.1 Muhtasari wa Utafiti ........ 102
5.2 Matokeo ya Utafiti ........ 105
5.4 Mchango wa utafiti ........ 106
5.5 Changamoto za Utafiti ........ 107
5.6 Mapendekezo ........ 108
5.7 Hitimisho ........ 108
**MAREJELEO ........ 109**

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.0 Usuli wa Mada

Malezi ya watoto ni suala muhimu katika jamii yoyote. Hii inatokana na kuwa watoto ndio msingi wa jamii na wanahitaji kulindwa na kuongozwa vyema. Kulingana na Zombwe (2008), mafanikio ya mtu mzima huchangiwa na malezi ya utotoni pamoja na mwingiliano wa mazingira na jamii yake. Wazazi au walezi wakifanya jitihada kumjenga mtoto na kumwandaa mtoto kuwa raia makini anayejitambua, mchango wa mtoto huyu kwa maendeleo ya jamii utakuwa mkubwa na familia yake itanufaika zaidi. Makuzi na maendeleo ya mtoto yanachangiwa na wazazi, familia na jamii kwa jumla. Hivyo basi, ni muhimu wazazi na walezi kuwatunza na kuwalea watoto kwa kufuata misingi inayofaa.

Santrock (2006), anaeleza kuwa katika jamii nyingi za Afrika, malezi ya watoto yalichukua maumbo tofauti yaliyowasaidia watoto kuwa watu wazima waliowajibika na wenye maadili. Malezi pia yaliathiriwa na utamaduni na itikadi za jamii husika. Ilikuwa ni jukumu la wazazi na jamii nzima kuhakikisha kuwa kila mtoto alipata malezi mema tofauti na ilivyo sasa ambapo jukumu la kumlea mtoto ni la mzazi binafsi.

Cummings na Davies (1994), wanaeleza kuwa uhusiano wa wazazi katika familia huathiri tabia za watoto wao. Hii inatokana na sababu kuwa watoto hutazama mambo wanayotekeleza na kuyaiga. Migogoro inaweza kutokea katika familia ambazo wazazi hutumia mbinu tofauti kuwalea watoto wao. Migogoro hii inatokana na kuwa hakuna mbinu mahsusi ya kuwalea watoto hivyo, wazazi hutofautiana katika malezi ya watoto

wao. Itakuwa vigumu sana kwa mzazi anayetumia mbinu ya kimabavu na mzazi anayewapa watoto uhuru kushirikiana katika malezi. Mivutano kama hii katika familia huweza kuathiri watoto kiakili na hata kitabia.

Baumrind (1968) anaeleza kuwa kuna aina tatu za malezi ya kijadi; ya kwanza ni malezi ya kimabavu ambapo wazazi huweka sheria kali kwa watoto wao ambazo ni lazima wazifuate. Kukosa kufuata sheria hizo hupelekea kupewa adhabu kali. Watoto wanaolelewa kwa njia hii huwa na nidhamu sana ila ni ya woga. Aina ya pili ni malezi ya kimamlaka ambapo mzazi huwa na mamlaka kwa watoto lakini si kwa mabavu. Mzazi hutunga sheria na mwongozo mzima kwa watoto na huweka sababu ya sheria zile. Huwa tayari kuongea na watoto na kusikiliza hoja zao. Aina ya tatu ni malezi ya uhuru au malezi ya kudekeza. Wazazi wa aina hii mara nyingi huwaacha huru wafanye kile watakacho. Hawaweki sheria zozote za kuwaongoza watoto bali huwafanya kama marafiki zao. Watoto wanapokosea huwa hawaadhibiwi bali hutetewa.

Kulingana na Maccoby na Martin (1983) sio aina tatu tu za malezi wanazotumia walezi bali kuna mbinu zingine wanazotumia walezi. Wanaeleza kuwa kuna malezi ya kutojihusisha au malezi ya kutelekeza ambapo mzazi hajihusishi na maendeleo ya mtoto wala hana malengo yoyote ya siku zijazo ya mtoto huyo. Haangalii kama mtoto yupo au hayupo, alienda shule au hakwenda, alikula au hakula. Wengine wa wazazi hawa huwakataa hata watoto wao. Cherry (2012) anaeleza kuwa njia ya kuwalea watoto hutofautiana katika familia. Kuna familia ambazo hutumia mbinu ya kimabavu na zingine hutumia mbinu ya kudekeza. Tofauti hizi zinatokana na itikadi za jamii fulani, maumbile, usuli wa wazazi, kiwango cha elimu, utabaka na dini. Anaeleza kuwa kuna wazazi ambao

hutumia mbinu ya kimabavu ambayo inahitaji mtoto kufuata sheria kali alizowekewa na mzazi. Kwa upande mwingine, kuna watoto ambao wana hiari ya kufanya walitakalo.

Suala la malezi ya watoto ni mojawapo ya masuala nyeti katika jamii. Hii inatokana na ukweli kuwa watoto ndio msingi wa jamii. Watafiti wengi wamelishughulikia suala hili katika kitengo cha kishoshiolojia. Isitoshe, Waandishi wengi wameandika kuhusu suala hili kwa kuwa ni mojawapo ya masuala ibuka katika jamii. Pia, fasihi ni zao la jamii na msanii hupata hamu ya kuandika kutokana na mambo anayopitia katika mazingira yake. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu ili kueleza tajriba mbalimbali za maisha ya wanajamii. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fasihi inawasilisha hali, maingiliano na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake. Fasihi huwasilisha maudhui yenye mguso kwa wanajamii kupitia kwa lugha iliyojaa mvuto. Wanafafanua kuwa msanii ni zao la jamii na hujaribu kuwasilisha matukio ya jamii kama yanavyopatikana katika jamii hiyo. Maudhui anayowasilisha hutokana na hali halisi zinazomzunguka za kitamaduni, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Hakuna fasihi inayoibuka katika ombwe tupu. Kila fasihi ni zao halisi la jamii na inaonyesha kuwepo kwa jamii hiyo. Masuala ambayo yanaibuliwa katika riwaya za *Dunia Mashaka Makuu* ya L. Omar (2004) na *Tumaini* ya C. Momanyi (2006) ni mambo yanayopatikana katika jamii. Ingawa kazi hizi ni za kubuni zinaeleza ukweli kuhusu maisha.

### 1.1 Suala la Utafiti

Utafiti huu ulieleza, kufafanua na kuchanganua riwaya mbili za Kiswahili kwa lengo la kuonyesha jinsi waandishi hawa wanavyosawiri suala la malezi. Suala la malezi ya watoto ni muhimu na la kimsingi katika jamii. Malezi ya watoto huathiri jinsi jamii inavyokua na kuendelea. Changamoto wanazopitia watoto wengi katika jamii hutokana

na mbinu walizotumia wazazi wao kuwalea. Makuzi na maendeleo bora ya mtoto pia huchangiwa na jitihada za wazazi au walezi kumjenga mtoto kuelekea kufanikisha matamanio yake. Suala la malezi ya watoto halijashughulikiwa katika fasihi. Riwaya zilizotumiwa katika utafiti huu ni *Tumaini* ya C. Momanyi (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* yake L. Omar (2004). Riwaya hizi mbili zinaonyesha masuala ya kiuchumi na kijamii yanayoathiri malezi ya watoto na athari ya mbinu za malezi zinazotumiwa na wahusika. Isitoshe, riwaya hizi zinadhihirisha jamii zenye tofauti za kimazingira, kiuchumi na kitamaduni ambazo zinaathiri malezi ya watoto. Utafiti huu ulilenga kubainisha wazi mtazamo wa waandishi hawa kuhusu malezi ya watoto. Riwaya ya Kiswahili imekuwa ikisawiri maisha ya jamii kwa njia tofauti. Ni katika muktadha huu ambapo utafiti huu ulishughulikia usawiri wa aina za malezi katika riwaya teule. Utafiti huu ulinuia kuchunguza jinsi asasi na hali za kijamii zinavyoathiri malezi ya watoto pamoja na kubainisha athari zinazotokana na malezi wanayopata watoto katika riwaya hizi.

### 1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

(a) Je, mbinu zipi za malezi ya watoto katika jamii zinazobainika katika riwaya ya *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004)?

(b) Ni asasi na hali gani katika jamii zinazochangia katika malezi ya watoto katika riwaya ya *Tumaini* (2006) ya C. Momanyi na *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ya L. Omar?

(c) Mbinu za malezi zina athari zipi kwa watoto na jamii katika riwaya ya *Tumaini* (2006) ya C. Momanyi na *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ya L. Omar?

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

(a) Kueleza mbinu za malezi zinazobainika katika riwaya ya *Tumaini* ya C. Momanyi (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* ya L. Omar (2004).

(b) Kuchunguza asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto katika riwaya ya *Tumaini* ya C. Momanyi (2006*)* na *Dunia Mashaka Makuu* ya L. Omar (2004)

(c) Kubainisha athari za malezi katika riwaya ya *Tumaini* ya C. Momanyi (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* ya L. Omar (2004).

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Mwandishi wa kazi yoyote ya fasihi huwa na dhima ya kuelimisha, kuonya na hata kukashifu maovu yaliyopo katika jamii. Hivyo, huandika masuala yaliyomo kwenye jamii kama vile ukosefu wa kazi, ufisadi, dhuluma, malezi ya watoto miongoni mwa mengine. Hivyo basi, utanzu wa riwaya una dhima muhimu katika kukosoa, kutahadharisha na kuhamasisha jamii. Uhakiki wa riwaya za *Tumaini* ya Momanyi (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* ya Omar (2004) ulifanywa ili kuupa utanzu wa riwaya dhima yake inayostahili.

Utafiti huu pia ulitokana na ukweli kwamba malezi ya watoto ni suala nyeti sana ambalo linahitaji kushughulikiwa. Jamii yoyote haiwezi kuendelea pasipo watoto kupewa malezi mema. Watoto pia ni miongoni mwa viumbe muhimu katika jamii yoyote na wanahitaji malezi mema. Mashirika mbalimbali ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali yanaangazia suala hili kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, katika jamii zingine za Kiafrika, wasichana

wanapaswa tohara na kuozwa na wazazi wao ili wapate pesa. Hii inawafanya watoto kukosa elimu ambayo ni muhimu kwa maisha ya binadamu.

Sababu nyingine ni kuwa matini zilizoshughulikiwa katika utafiti huu ambazo ni *Dunia Mashaka Makuu* ya L. Omar (2004) na *Tumaini* ya C. Momanyi (2006) hazijawahi kuhakikiwa katika misingi ya nadharia ya uhalisia na hivyo utafiti huu ulidhamiria kuziba pengo hili.

Mada hii pia ilifaa sana hasa kwa wakati huu ambapo nchini Kenya nidhamu kwa watoto imedidimia na watoto wengi wametelekezwa. Imedhihirika katika vyombo vya habari kuwa watoto wengi wanajitoa uhai na kuwaua wenzao kwa sababu ya kutamauka, Wengine pia hutoroka nyumbani kwa sababu za kinyumbani. Utamaushi huu unatokana na mbinu za malezi walizotumia walezi. Aidha, utafiti huu ulimwezesha mtafiti kutoa mchango wake ili kufikia njia mwafaka za kukabiliana na changamoto za malezi.

**1.5 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza aina za malezi na kutathmini athari za aina hizo katika riwaya teule za fasihi ya Kiswahili. Baada ya usomaji wa vitabu mbalimbali vya fasihi kwa mfano, *Utengano* (1982), *Kidagaa Kimemwozea* (2012) na vinginevyo, mtafiti aliteua riwaya zifuatazo.

(a) *Tumaini* ya C. Momanyi (2006)

(b) *Dunia Mashaka Makuu* ya L. Omar (2004)

Kazi hizi ziliteuliwa kama sampuli tu na zilichangia ipasavyo katika kupata data ya utafiti huu. Pia zimeakisi hali ilivyo kwenye jamii ya sasa na hasa jamii ya Kenya ambapo

wazazi wengi wamewatelekeza watoto. Riwaya hizi pia zimeandikwa katika kipindi maalum na katika mazingira tofauti. Uchaguzi wa riwaya hizi pia uliongozwa na wazo kuwa mwandishi haandiki kutoka ombwe tupu. Lazima aangalie masuala muhimu yanayoikumba jamii yake. Fasihi pia ni kioo cha jamii ambacho humulika maovu na mazuri ya jamii.

Utafiti huu uliwahusisha watoto wa miaka kumi hadi kumi na minane wanaotegemea wazazi na walezi wengine. Ulijikita katika jinsia zote, wavulana na wasichana.

### 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Kuna tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa kuhusu malezi ya watoto. Baadhi ya tafiti hizi ni za kishoshiolojia na za fasihi. Utafiti huu ulihusisha usomaji wa tafiti mbalimbali zinazoshughulikia malezi ya watoto na fasihi ya Kiswahili inayoangazia masuala ya watoto.

#### 1.6.1 Tafiti za Kishosholojia

Hare na wengine (2011), katika utafiti wao unaohusu uhusiano wa kina mama na vijana, jinsi wanavyowakubali na kuwasiliana nao, waligundua kuwa kitu muhimu sana katika ujana ni kukubaliwa na wazazi na wanajamii wengine. Ilibainika kuwa vijana wanapokosa kukubaliwa na wazazi wao, hawawezi kufichua jambo lolote kwa wazazi wao. Hivyo, vijana hujitia katika shida ambazo wao wenyewe hawawezi kutatua. Hivyo basi, ni muhimu wazazi kuwakubali watoto wao na kuhakikisha kuwa wanashirikiana kwa kila jambo. Wanafaa kuwapa nafasi ya kujieleza na kutoa kauli fulani katika jamii. Ingawa utafiti huu unahusu vijana, ni muhimu kwa kuwa ulitusaidia kuelewa athari za

malezi ya watoto. Katika jamii, athari zinazowakumba watoto waliobaleghe ni sawa na zinazowakumba vijana.

Uhusiano kati ya dhuluma kwa watoto na dawa za kulevya umejadiliwa na Tomison (1996). Ameonyesha kuwa kuna uhusiano kati ya matumizi ya dawa za kulevya na dhuluma kwa watoto. Anatambua vyanzo mbalimbali vya dhuluma kama vile tabia za kibinafsi, matatizo ya kinyumbani na mambo mengine ya kijamii hutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Tomison (1996) alitambua aina mbalimbali za dhuluma kama vile kutowatunza watoto kabisa, mauaji na matumizi ya nguvu iliyopita kiasi. Utafiti huu unapendekeza mafunzo ya kijamii pamoja na kushirikishwa kwa mafunzo haya katika mitaala ya shule. Ingawa utafiti huu si wa kifasihi ulichangia pakubwa kuelewa mada hii. Masuala muhimu ya kijamii yanayoangaziwa katika utafiti huu kama vile dhuluma zinazowakumba watoto katika nchi ya Australia ndiyo yanayoshughulikiwa kisanii na waandishi wa riwaya teule. Baadhi ya dhuluma wanazopitia watoto hutokana na mbinu mbaya za kuwalea watoto hao. Tofauti ni kuwa utafiti huu ulifanywa katika mazingira, wakati na utamaduni tofauti. Pia, utafiti huu umeonyesha dhuluma kama mojawapo ya athari za malezi mabaya.

Wanjohi (2007) akitafiti kuhusu jukumu la wanaume katika malezi ya watoto katika jamii ya Wamaasai alichunguza usaidizi ambao kina mama hupata kutoka kwa waume wao na jinsi wanaume wanavyohusika katika malezi ya watoto chini ya miaka mitatu. Aliangazia vigezo vinavyowaathiri wanaume katika malezi ya watoto. Utafiti huu ulibainisha kuwa wanaume waliwalipia watoto karo za shule lakini hawakuhusika katika kuwapa chakula, kucheza nao na pia kuwasikiliza. Ilibainika kuwa utamaduni ni mojawapo ya kigezo kinachowafanya wanaume kutoshiriki katika malezi ya watoto wao. Utafiti huu ni

muhimu kwani ulitusaidia kuchunguza baadhi ya changamoto wanazopitia walezi katika malezi ya watoto. Pia, ulitusaidia kuchunguza baadhi ya asasi zinazochangia katika malezi ya watoto.

### 1.6.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Malezi ya Watoto Katika Fasihi

Uhakiki wa kiisimu wa riwaya za Suleiman Mohamed: *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1976) umechunguzwa na Osore (1994). Katika utafiti wake, ameonyesha kuwa uhakiki wa kiisimu unaweza kuinua kiwango cha uelewaji wa riwaya teule. Pia, akizingatia kipengele cha wahusika anaonyesha jinsi wahusika mbalimbali wanavyotendewa na kudhulumiwa na wahusika wengine. Baadhi ya wahusika wanaodhulumiwa na kutendewa ni watoto. Utafiti wa Osore ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu unaonyesha baadhi ya mambo wanayotendewa watoto katika riwaya hizo. Tofauti na utafiti huu aliangazia wahusika wote kwa jumla lakini utafiti huu ulichunguza wahusika watoto na mambo wanayopitia katika jamii yanayotokana na mbinu za malezi. Riwaya zilizohakikiwa pia ni tofauti.

Usawiri wa mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili katika ushairi wa Kiswahili umechunguzwa na Momanyi (1998). Katika utafiti wake, alionyesha asasi ya dini kama mojawapo ya asasi za kijamii zinazoathiri nafasi ya mwanamke kwa kumpa nafasi duni ikilinganishwa na mwanaume. Utafiti huu ni muhimu kwa utafiti wa sasa kwani ulitusaidia kuelewa baadhi ya asasi zinazochangia katika malezi ya watoto. Tofauti ni kuwa mtafiti alijifunga kumhakiki mwanamke muislamu lakini utafiti huu ulihakiki watoto wa jinsia zote wa miaka kumi hadi kumi na minane. Pia, alihakiki utanzu wa ushairi lakini utafiti huu umehakiki riwaya.

Mbatia (1998) katika makala yake Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile* anaeleza dhamira ya malezi kwa watoto kutoka kwa wazazi wao. Dhamira hii inaelezwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* iliyoandikwa na Kezilahabi (1971). Anaeleza kuwa wazazi wana jukumu kubwa katika kuwafanya watoto wao kuwa na tabia njema au mbaya kutokana jinsi wanavyowalea. Kwa mfano, Zakaria babake Rosa hakuwapa watoto wake idhini ya kuongea na mwanamume yeyote. Madhara ya malezi haya yanaonekana pale Rosa anaenda kusoma katika chuo cha ualimu na kupata uhuru wa kufanya mambo mengi. Uhuru aliopata ulimfanya apate shida nyingi na mwishowe aliamua kujiua. Maelezo ya Mbatia ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa yamedokeza dhamira ya malezi ya watoto katika jamii. Utafiti huu pia ulitusaidia kueleza athari za malezi katika riwaya za *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004).

Usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya tatu za Zainabu Burhani: *Mali ya Maskini* (1981), *Mwisho wa Kosa* (1987) na *Kipimo cha Mizani* (2004) umefanywa na Mavisi (2007). Mtafiti huyu anaeleza jinsi wahusika wa kike hukumbwa na dhuluma nyingi kutokana na tamaduni hasi za jamii husika. Anaeleza ya kwamba wanawake wana nafasi waliotengewa na jamii kutokana na maumbile yao. Wao hunyanyaswa na kukumbwa na madhila tele kutokana na itikadi dhalimu zinazoendelezwa na jamii husika. Utafiti huu ulitusaidia kuchanganua jinsi itikadi za jamii zinavyochangia katika malezi ya watoto.

Traore (2008) alichunguza suala la familia na jamii katika riwaya sita za Said Ahmed Mohammed: .*Asali chungu* (1978), *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano* (1980), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Tata za Asumini* (1990), *Babu Alipofufuka* (2001). Katika utafiti wake, alionyesha kuwa matatizo ya kifamilia na nafasi ya mwanamke ni mojawapo ya maudhui yanayosababisha matatizo makubwa kwa wahusika wa kike. Traore

(keshatajwa) alichunguza wahusika katika muktadha wa kifamilia katika jamii husika. Ameonyesha namna ambavyo mifumo ya kifamilia na kijamii inavyowaathiri wahusika kimawazo. Utafiti huu ulitusaidia kuchanganua jinsi mifumo mbalimbali ya kifamilia inavyoathiri malezi ya watoto.

Dhuluma dhidi ya watoto katika riwaya teule za Kiswahili imeangaziwa na Kavuria (2008). Katika utafiti wake, ameonyesha aina za dhuluma wanazopitia watoto hususan za kimwili na kiakili. Utafiti huu umeangazia suala hili kwa kina. Umeonyesha kuwa nyingi za dhuluma hutokana na kukosa kuwajibika kwa wazazi na walezi wengine. Utafiti huu ulitumia nadharia ya ukata tamaa na ushari iliyolenga kuchunguza jinsi dhana za kisaikolojia ambazo haziwezi kuonekana wazi pamoja na jamii zinaweza kuathiri tabia za watu. Nadharia hii inaeleza chanzo cha dhuluma. Inawaonyesha wadhulumu kama watu wenye akili timamu. Tofauti na utafiti wa Kavuria utafiti huu ulitumia nadharia ya uhalisia. Pia, ulichunguza njia zote za malezi ya watoto na jinsi zinavyowaathiri watoto. Hata hivyo, utafiti wa Kavuria una mchango kwa utafiti huu kwa kuwa unawahusu watoto ambao ni muhimu sana katika jamii. Pia, umeonyesha kuwa baadhi ya dhuluma wanazopitia watoto hutokana na malezi mabaya.

Vilevile Karanja (2008) alichunguza usawiri wa masuala ibuka katika hadithi za watoto. Katika utafiti huu, aliangazia masuala ibuka kama vile ubaguzi kwa misingi ya kijinsia, utumiaji wa dawa za kulevya, afya na UKIMWI, haki za watoto, suala la kuzorota kwa usalama, uadilifu, sheria na haki. Utafiti huu umegusia suala la malezi kama mojawapo ya masuala ibuka katika jamii. Tofauti na utafiti wa Karanja, utafiti huu uliangazia suala hili kwa kina kwa kuonyesha jinsi malezi yaa watoto yalivyoathiri jamii.

Utafiti kuhusu hali ya vijana katika *Vipanya vya Maabara*, cha Mbatia (2007) umefanywa na Naliaka (2012). Mtafiti huyu anaeleza matatizo yanayowakumba vijana katika jamii na chanzo cha changamoto ambazo zinawakumba. Kwa mfano, anaeleza chanzo cha vijana kubobea dawa za kulevya ni kukosa wazazi wa kuwaelekeza. Aidha, mtafiti huyu aliwahakiki wahusika wachache huku akiangazia chanzo cha changamoto zinazowakumba lakini kwa kifupi mno. Utafiti huu uliangazia kwa undani ili kutathmini hasa asasi zinazochangia katika malezi ya watoto. Kazi hii bila shaka ilisaidia pakubwa katika kuangazia athari za malezi kwa jamii ya *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004).

Vilevile Webukha (2014) alishughulikia jinsi wahusika mbalimbali wanavyodhihirisha matumaini katika hali ngumu za kisiasa na kitamaduni. Ameonyesha jinsi wahusika mbalimbali wanavyojikakamua kujitoa katika hali ngumu wanazopitia. Watoto ni miongoni mwa wanajamii ambao hukumbana na mambo mengi katika maisha lakini kuna wale ambao hawakati tamaa. Wengi wao huamini kuwa hata matatizo yanapokuwa mengi siku moja yataisha. Utafiti wa Webukha ni muhimu kwa utafiti huu kwani ulitusaidia kujua na kuelewa mambo yanayowaudhi na kuwafanya watoto wakose matumaini.

Suala la utamaushi wa wahusika wa kike katika riwaya za *Kiu* (1972) ya S. Mohamed na *Mwisho wa Kosa* (1987) ya Z. Burhani limefafanuliwa na Mulili (2014). Katika utafiti wake ameeleza tajriba za maisha wahusika wa kike wanazopitia. Pia, ameonyesha viwango vya utamaushi vinavyobainika katika riwaya teule. Ameonyesha asasi ya utamaduni kama mojawapo ya asasi zinazowafanya wahusika wa kike kukosa matumaini. Alitumia nadharia ya ufeministi wa kidhanaishi tofauti na utafiti huu ambao ulitumia nadharia ya uhalisia. Utafiti wa Mulili ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu

unawahusisha wahusika wa kike katika riwaya wakiwemo watoto. Tofauti iliyopo ni kuwa utafiti huu ulishughulikia malezi kwa watoto wote, wa kike na kiume. Ulionyesha kutamauka kama mojawapo ya athari za malezi mabaya.

Mayieka (2015) alichunguza masuala ibuka katika riwaya za kisasa: *Kidagaa Kimemwozea* (2012) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2012). Baadhi ya masuala ibuka aliyoangazia ni ulemavu, mapenzi na ndoa, ukiukaji wa haki za binadamu, ufisadi na kadhalika. Utafiti huu ulifaa zaidi kwani nadharia aliyotumia mtafiti ni sawa na iliyotumiwa katika utafiti huu. Tofauti ni kuwa mtafiti amezungumzia suala la masuala ibuka kwa ujumla ilhali utafiti huu ulifafanua malezi ya watoto kwa kina. Pia, riwaya zilizoteuliwa na mtafiti ni tofauti na riwaya zilizoteuliwa katika utafiti huu.

Mbali na hao, Munyoki (2015) alichunguza familia za Kiafrika katika njia panda katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) ya S. Mohamed. Katika utafiti wake, alionyesha jinsi usasa na ukale unavyoathiri familia nyingi. Pia, ameonyesha tofauti iliyoko kati ya familia za kisasa na kale. Utafiti wa Munyoki ulifaa zaidi kwa utafiti huu kwa kuwa familia ni mojawapo ya asasi zinazoathiri malezi ya watoto. Nadharia aliyotumia mtafiti ni sawa na nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ambayo ni ya uhalisia. Tofauti ni suala linalozungumziwa na riwaya zilizoteuliwa.

Mawazo na maoni ya watafiti tulioteua yana uhusiano mkubwa na utafiti huu kwa sababu yametaja baadhi ya mambo tuliyoshughulikia katika kazi hii. Tofauti iliyopo ni suala la utafiti ambapo utafiti huu ulijikita katika kuchunguza malezi ya watotokatika riwaya teule.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliaongozwa na nadharia ya uhalisia. Kwa mujibu wa Lawal na Maynard (1984) Nadharia hii iliasisiwa katika karne ya 19 na Gustave Flaubert (1850) na kufafanuliwa zaidi na E.Goffman (1952) aliyeishi kati ya mwaka (1922-1982). Watafiti wengine ambao wanatoa mchango wao ni Rene Wellek (1960), George Lukacs (1972) na Hegel G. (1979). Baadaye nadharia hii ilisambaa kule Uingereza, Urusi na Marekani. Kearns (1996) anaeleza kuwa uhalisia kama chombo cha kuchanganua na kutathmini watunzi ulianza kudhihirika kuanzia mwaka wa 1800 nyakati za mwandishi wa Kifaransa Gustave Flaubert. Dhana hii ya uhalisia ilianza kujitokeza zamani sana katika kipindi cha enzi za kati, baina ya 1100-1500 baada ya Kristo. Nadharia hii ilipitia mabadiliko mengi ya kimatumizi yaliyofanywa na wataalamu kama vile Emmanuel Kant (1790) na hata Schiller (1798). Waandishi wengine wanaohusishwa na nadharia hii ni Honore de Balzac na Emile Zola (1850). Nadharia hii ilizuka kama njia mojawapo ya kupinga ulimbwende. Matamanio ya kilimbwende yalikuwa ya kinjonzi zaidi yakilinganishwa na taabu zilizokuwa zikiwakabili watu. Walimbwende walikuwa wakijitungia mambo yasiyoweza kutimia.

Lukacs (1972), anaeleza uhalisia kama dhamira ya mwandishi. Mwandishi husukumwa na lengo la kusawiri uhalisi katika ukamilifu wake katika wakati fulani. Mwandishi anafaa kupenya chini ya picha ya kijuujuu na kudhihirisha mifanyiko na mabadiliko. Hivyo, kazi ya mwandishi inafaa kuusawiri ulimwengu kama changamano na wenye ukamilifu wa mandhari ya kawaida.

Madhumuni ya mwandishi kwa jamii ni kuwarudisha watu katika ulimwengu wao wa kawaida na kwamba ulimwengu utakaoumba uwe wa kweli (Larkin 1977). Jukumu la

msanii linafaa kuwa la kweli na linafaa kudhihirisha ukweli na hali halisi ya maisha. Ili kudhihirisha ukweli, msanii anafaa kutumia kipawa chake kuchora wahusika na mazingira yanayokubalika katika jamii ya wakati wake. Hii ni kwa kuwa mazingira huwa halisi na yanayoaminika.

Nadharia hii iliwekewa msingi na Hegel (1979). Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno uhalisia kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inawasilisha ulimwengu na maisha ya jamii ambako kuna mhusika anayetenda mambo kwa kuchochewa na mazingira anamoishi.

Uhalisia ulianza mwaka wa 1820. Haya ni kulingana na Msokile (1993). Nguzo ya nadharia hii ni wazo kuwa sanaa inafaaa iseme ukweli, iwe aminifu na ionyeshe hali hizo waziwazi. Ni mtazamo wa kifasihi unaochukulia kazi za kifasihi kama zinazoakisi sifa za kimsingi zinazohusishwa na uhalisi yaani hali halisi za maisha katika jamii husika.

Kulingana na Mbatia (2001), uhalisia ulizuka katika bara Ulaya katika karne ya kumi na tisa na kusambaa katika mataifa ulimwenguni. Wasanii wa uhalisia walijishughulisha kuutafuta na kuubainisha ukweli wa maisha. Waliamini kuwa ukweli huo uliweza kupatikana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Walisawiri mazingira halisi ya jamii kama ilivyo.

Wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida na wanaoweza kupatikana katika jamii halisi, huchunguza na kusimulia maisha yao na tajriba zao, husawiri na kuonyesha mazingira ya kawaida wakati wa kuandika kazi zao. Mwandishi kwa hivyo, anapaswa kuyaakisi maisha ya jamii katika ngazi ya kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa. Uhalisia hutilia mkazo uwasilishaji wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii na

anayeandika kwenye msingi wa tapo hili. Hivyo, mwanauhalisia hutilia mkazo wahusika katika hali za kawaida za maisha, matukio na mandhari ya kawaida kama yanavyojitokeza katika jamii. Wamitila (2002).

Ntarangwi (2004), anasema kuwa nadharia hii ina maana ya uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi na ilizuka katika karne ya kumi na tisa ili kupinga ulimbwende. Mwanauhalisia huamini ukweli unaozingatiwa ni ule unaoweza kuonekana na kudhibitishwa kwa tajriba. Hivyo basi, uhalisia huwa katika mambo yaliyopo ya matukio halisi kwa matokeo yanayoweza kudhibitika kuwa ya kweli. Imani ya mhalisia ni kuwa kazi ya fasihi inapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida wa kweli na halisi.

Wafula na Njogu (2007) wanasema uhalisia unahusishwa na kipindi maalum cha kihistoria katika jamii za Ulaya. Kipindi hiki kilianza mwanzoni mwa karne ya kumi na tisa nchini Ufaransa na kilihusishwa na waandishi Balzac, Stendhal na Flaubert. Waandishi hawa walisisitiza maelezo ya kikweli katika kazi zao na waliamini kuwa lengo la mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo. Uhalisia ulienea katika nchi nyingine za ulimwengu kutokana na mapinduzi yaliyosababisha kuzuka kwa mambo mapya katika nyanja mbalimbali za maisha. Matatizo yaliyofanana na mambo hayo ndiyo yaliyowafanya waandishi wengi kuukejeli ulimbwende na kuanza kuandika juu ya halisi ya maisha ya jamii. Wanasema kuwa mwandishi anapaswa kuitoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku. Uhalisia unapingana na aina yoyote ya majaribio. Vilevile wanaeleza kuwa dhana ya uhalisia ilianza kutumika takribani mnamo miaka ya 1790. Katika mwaka huo, Emmanuel Kant aliitumia istlahi ya udhahania kamilifu kama kinyume cha uhalisia. Kufikia mwaka wa 1798 wahakiki kama vile Schiller walikuwa

wakitumia maneno haya, udhanaishi na uhalisia kuashiria vinyume. Kutokana na historia hii, uhalisia imehusishwa na miktadha miwili. Kwanza, inatumiwa kutathmini hali au halia. Huu ni uhalisia wa maisha. Uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha.

Wahusika na wahakiki wengi waliotumia nadharia hii waliamini kuwa dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli kama ulivyo. Mwandishi anafaa kutoa picha ya jamii bila kuidunisha au kupiga chuku.

**Mihimili**

Nadharia ya uhalisia huongozwa na mihimili ifuatayo:

(a) Kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira. Mhimili huu ulionyesha jinsi waandishi wa riwaya teule walivyoweza kuwasilisha maudhui ya malezi katika jamii husika.

(b) Usawiri na uelezaji wa hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha kwa maana ya uigaji wa mazingira anayopatikana mwanadamu. Mhimili huu ulitusaidia kuchanganua matukio halisi yaliyowasilishwa na waandishi katika riwaya teule.

(c) Kazi ya msanii inapaswa kuonyesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao na jinsi wanavyohisi na kutenda wanapokumbana na hali fulani. Mhimili huu ulitusaidia kuchanganua athari za malezi wanayopata watoto katika jamii.

(d) Wahusika huwa halisi na lugha wanayotumia huwa rahisi na inayoeleweka. Mhimili huu ulitusaidia kuelewa wahusika iwapo ni wa kweli au ni wa kudhaniwa tu na iwapo lugha wanayotumia inaeleweka na wanajamii.

Mtafiti alitumia nadharia hii kama msingi wa uchunguzi wa riwaya teule kwani mambo yanayojitokeza katika riwaya ya *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ni ya kweli na vilevile ni mambo tunayokumbana nayo katika hali halisi ya maisha yetu ya kila siku.

### 1.8 Mbinu za Utafiti

#### 1.8.0 Utangulizi

Ili kujaza pengo katika utafiti huu mtafiti aliteua riwaya mbili za kisasa: *Tumaini* ya C. Momanyi (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* ya L. Omar (2004). Pia mtafiti alisoma tasnifu, majarida na magazeti ili kuliziba pengo hili.

#### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kuzingatia muundo wa kimaelezo ambapo data zilizokusanywa kutoka kwa riwaya teule zilielezwa. Mbinu zinatumiwa na wazazi kuwalea watoto katika riwaya teule, asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto pamoja na athari zitokanazo na mbinu za malezi wanayotumia wahusika zimeelezwa.

#### 1.8.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani. Mbinu hii ilitumika ili kupata data kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule. Maandishi mbalimbali yalipitiwa maktabani ikiwa ni pamoja na tasnifu, majarida, makala, magazeti na mtandao ili kupata data faafu ya mada ya utafiti. Data ilitokana na usomaji wa kina wa riwaya za *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004). Machapisho yote muhimu kuhusu utafiti huu yalitumika. Aidha, maoni na ujumbe wa wataalamu wengine kupitia kwa tahakiki zao ulitambuliwa.

### 1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Utafiti huu ulilenga vitabu mahsusi ambavyo vina vipengele muhimu vya kuchunguzwa. Vitabu hivi viwili *Tumaini* (2006) ya C. Momanyi na *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ya L. Omar vilichunguzwa. Riwaya hizi ziliteuliwa kimaksudi kwa sababu zinachangia suala la malezi ya watoto na athari ya malezi hayo. Waandishi wa vitabu hivi pia wameandika kazi zao katika kipindi mahsusi. Malezi ya watoto katika riwaya hizi ndiyo yaliteuliwa ili kuafikiana na malengo ya utafiti. Mtafiti alisoma riwaya teule kwa kina na kuteua data ambayo ilihusiana na maswali na malengo ya utafiti. Mihimili ya nadharia ya uhalisia ilimwongoza mtafiti kupata data inayohusiana na maswali na malengo ya utafiti.

### 1.8.4 Ukusanyaji wa Data

Mbinu ambayo ilitumika katika ukusanyaji wa data katika utafiti huu ni usomaji wa riwaya za *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004), tasnifu, majarida na machapisho yaliyoandikwa kuhusiana na mada ya utafiti. Aidha, mtafiti alisoma vitabu vya wataalamu mbalimbali vinavyotaja mambo ya malezi ili kuelewa zaidi kuhusu dhana hiyo. Katika usomaji huu, mtafiti alibainisha mbinu za malezi zinazotumiwa na wahusika, asasi na hali zinazowasukuma walezi kutumia mbinu fulani ya malezi pamoja na athari za mbinu hizi kwa watoto na walezi. Vitabu hivi vilimwezesha mtafiti kukusanya data na kuafikia malengo ya kazi hii. Pia, vilimwezesha mtafiti kujenga msingi bora na kulifahamu pengo la utafiti na yaliyoandikwa kuhusu mada.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data uliathiriwa na mbinu za ukusanyaji zilizotumika kupata data husika. Utafiti huu uliegemea data iliyokusanywa kutoka kwa usomaji wa riwaya, majarida na tasnifu mbalimbali maktabani. Mtafiti alisoma riwaya teule: *Tumaini* (2006)

na *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na kubainisha vipengele vinavyohusiana na malezi ya watoto. Uchanganuzi wa vipengele vya malezi ulikuwa wa maelezo. Mtafiti alieleza kwa kina mbinu za malezi ya watoto, asasi na hali zinazowafanya walezi watumie mbinu tofauti na athari za mbinu za malezi wanazotumia walezi. Pia, mtafiti alichanganua data kwa kuzingatia kigezo cha umri ambapo watoto wenye umri wa miaka kumi hadi kumi na minane waliangaziwa. Wazazi na walezi wengine pia waliangaziwa huku mtafiti akieleza lugha waliyotumia kwa watoto na pia matendo yao.

Data kutoka kazi za fasihi zilizoteuliwa ilichanganuliwa kulingana na maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia. Katika kufanya hivyo, mtafiti alitafuta data inayohusiana na malengo ya utafiti yenye vipengele vifuatavyo: Mbinu za malezi, asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto na athari za malezi ya watoto na kuilinganisha na hali halisi katika jamii.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kinadhari na utoaji mifano mahsusi kwa kuzingatia sura mbalimbali. Maelezo haya yalifafanua malezi kama suala kuu katika riwaya teule. Maelezo haya yalihusu kubainisha aina ya malezi yanayojitokeza katika kazi ya fasihi ambayo ni malezi ya kimabavu, malezi ya kimamlaka, malezi ya kudekeza, malezi ya kutojihusisha pamoja na malezi ya ushirikiano. Mtafiti alieleza kwa kutoa mifano ifaayo jinsi wahusika katika riwaya teule wanavyotekeleza aina hizi za malezi. Asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto katika riwaya teule pia zilielezwa. Hizi ni pamoja na; utamaduni, elimu, hali ya uchumi, jinsia na uana, asasi ya familia na ndoa na taasubi ya kiume. Isitoshe, athari za njia ya malezi yanayotekelezwa na wahusika katika riwaya teule zimeelezwa. Athari hizi ni pamoja na utengano katika

familia, Watoto kukumbwa na maradhi, utovu wa nidhamu, majuto, kutamauka kwa wahusika na matumizi ya dawa za kulevya. Athari hizi zimeelezwa kwa kina huku mtafiti akitoa mifano ifaayo. Uwasilishaji wa data ulifanywa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia.

### 1.8.7 Hitimisho

Sura hii imeangazia usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Katika sura hii, mtafiti ameonyesha kuwa utafiti huu umeongozwa na mihimili ya nadharia ya uhalisia. Pia, imedhihirika kuwa riwaya mbili za Kiswahili ambazo ni *Tumaini* (2006) ya C. Momanyi na *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ya L. Omar zimetumika kufanikisha utafiti huu. Utafiti huu pia ulifanywa maktabani. Sura inayofuata imechunguza mbinu mbalimbali za malezi ya watoto katika riwaya teule.

# SURA YA PILI

# MBINU MBALIMBALI ZA MALEZI YA WATOTO KATIKA RIWAYA TEULE

## 2.0 Utangulizi

Sura hii ilishughulikia mbinu mbalimbali wanazotumia wazazi kuwalea watoto wao katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006). Mhimili wa nadharia ya uhalisia ambao utaongoza utafiti huu ili kutimiza lengo hili ni: Usawiri na uelezaji wa hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha kwa maana ya uigaji wa mazingira anayopatikana mwanadamu. Nadharia hii imechaguliwa kwa kuwa riwaya zilizochaguliwa zinaangazia mambo yanayotendeka katika mazingira ya mwanadamu. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fasihi inapaswa kuwasilisha hali, maingiliano pamoja na mikinzano miongoni mwa binadamu na mazingira yake.

Suala la malezi ya watoto ni suala nyeti katika jamii yoyote. Watoto ndio msingi wa jamii yoyote na wanahitaji kutunzwa na kulindwa ipasavyo. Jamii yoyote haiwezi kuendelea iwapo watoto hawapewi malezi bora. Suala hili limekuwa likiangaziwa tangu jadi. Mbinu walizotumia walezi wa zamani zilikuwa tofauti na wanazotumia walezi wa kisasa. Santrock (2006) anaeleza kuwa malezi ya kijadi yalihusisha jamii nzima. Mzazi yeyote angemwadhibu na kumwelekeza mtoto iwapo angekosea tofauti na ilivyo sasa ambapo malezi ni ya mzazi binafsi. Mwenesi (2016) anaeleza kuwa malezi ya watoto nchini Kenya yamebadilika. Mabadiliko haya yanatokana na teknolojia za kisasa, mahitaji ya watoto pamoja na maingiliano ya jamii. Walezi wa kisasa wanahitaji kutumia mbinu mwafaka za malezi ili kuwaelekeza na kuwaongoza watoto.

Muhtasari wa riwaya ya *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Mkuu* (2004), utatolewa kabla ya kuchanganua mbinu mbalimbali za malezi ili matukio yaeleweke kwa urahisi.

### 2.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004)

Riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* ilichapishwa mwaka wa 2004. Mwandishi wa riwaya hii anaeleza mambo kadha wa kadha yanayomzunguka mwanadamu katika mazingira yake. Baadhi ya mambo anayoeleza ni uwajibikaji, ndoa na familia, elimu, wizi, malezi ya watoto na mengineyo. Hadithi inapoanza, Mzee Mashaka Makuu anamwita mkewe Bi.Nusura ili wazungumze. Mzee Mashaka hataki mkewe afanye kazi yoyote kwa kuwa ni mjamzito. Anamweleza kuwa anafaa kupumzika kwa kuwa kuna watumishi. Bi. Nusura anamweleza kuwa kazi ni muhimu na hawafai kuwaachia watumishi wafanye kazi zote. Bi. Nusura amechelewa kujifungua. Jambo hili linamtia wasiwasi sana mumewe kwa sababu ana hamu ya kupata mtoto wa kiume atakayerithi mali yake. Jambo hili halimfurahishi Bi. Nusura kwa sababu wana mtoto wa kike ambaye ni Yasibu.

Yasibu tu ndiye mtoto wa Bwana na Bi. Mashaka, kwa sababu hii Mzee Mashaka anamdekeza sana. Hataki afanye kazi yoyote nyumbani ila kudurusu masomo. Anakasirika sana anapoona Yasibu akitumwa na watumishi. Bi. Nusura anaona kuwa kumdekeza Yasibu ni kumpotosha.

Alfajiri moja, Bi. Nusura hakuwa na lingine la kutenda kwa kuwa wafanyakazi walifanya kazi zote. Anaamua kwenda zizini kuwasimamia wakamaji. Kwa bahati mbaya, anagongwa na ndama na kujifungua. Jambo hili linamkera sana Bwana Mashaka kwa kuwa kulingana na utamaduni wao, mtoto azaliwapo kwa njia hiyo huwa laana. Hata

hivyo, anamshughulikia mkewe Bi. Nusura vizuri. Siku ya saba inapotimia, kulingana na utamaduni wao mtoto anapewa jina Dunia.

Mzee Mashaka anaendelea kumdekeza Yasibu. Hakumruhusu kutangamana na wenzake. Pia, hakuwa na idhini ya kujiamuliwa mambo yake mwenyewe jambo ambalo linamkera Yasibu sana. Siku moja, anamweleza babake kuwa anataka uhuru kama wenzake. Babake bila kuwazia jambo hilo na kumshauri anamruhusu kufanya atakalo. Baada ya siku chache, Yasibu anaanza kubadilisha tabia. Yasibu anaanza kuchelewa kufika nyumbani. Jambo hili linamkera sana Bi. Nusura na kumweleza mumewe kuwa kumpa uhuru Yasibu sio jambo la busara. Baada ya siku chache, maendeleo ya Yasibu shuleni yanaanza kuzorota na kuanza kuwa wa mwisho darasani. Muda si muda Yasibu anatungwa mimba na Pazia. Jambo hili linamkasirisha sana Bwana Mashaka na kuchukulia kuwa ni nuksi za kuzaliwa kwa Dunia.

Bwana Mashaka anapogundua kuwa Yasibu ni mjamzito, anaajiri mkunga kwa siri ili amhudumie mwanawe kwa kuhofia majirani. Mwezi wa tisa unapofika, Yasibu anajifungua. Mashaka anampa mjukuu wake jina Yadhuru. Tangu siku hiyo, Bwana Mashaka hakuwa na uhusiano mwema na Yasibu. Mzee Mashaka anaacha kumsaidia na kumsetiri. Jambo hili linamhuzunisha Yasibu sana na kuamua kijiua. Kwa bahati nzuri, Mzee Mafusho anamuona na kumnusuru. Baada ya siku Chache, Yasibu anaamua kutoroka nyumbani.

Dunia naye anaamua kuacha shule. Mzee Mashaka anakasirika sana na kukosa kuzungumza naye. Baada ya siku kadha Dunia anabadilisha tabia yake na anarudi shule. Dunia anaendelea na Masomo yake kwa ufadhili wa mwalimu mkuu Bwana Busara.

Anaendelea na masomo yake na kuweza kuhitumu vyema katika mtihani wa darasa la nane. Bwana Mashaka anaposikia matokeo ya Dunia, anafurahi sana na kuandaa karamu kubwa. Dunia anamweleza rafikiye Pazia nia ya babake ya kumrudisha shule. Pazia anamchochea Dunia na kumwambia kuwa asikubali ahadi za babake kwa kuwa alikataa kumlipia karo za shuleya msingi. Siku ya karamu inapofika, Dunia anatumia vileo ili aweze kumwaibisha babake. Kwenye karamu, Bwana Mashaka anaonyesha kujuta. Anaeleza kuwa atamwezesha Dunia kuendelea na masomo hadi chuo kikuu.

Dunia kwa ushauri wa rafikiye Pazia, anasimama mbele ya hadhira na kusema kuwa hataendelea na masomo kwa kuwa babake hakuhusika kwa vyovyote vile kwa ufanisi wake. Watu wengi akiwemo mwalimu Busara wanamsihi aendelee na masomo lakini anakataa katakata. Mwishowe anaamua kutorokea mji wa Mwambao.

Dunia anakumbana na masaibu mbalimbali katika mji wa Mwambao. Kwanza, anaibiwa mkoba wake anapoenda kuoga. Anatoka nje akiwa uchi wa mnyama. Askari wanapomkuta wanamshika kwa kosa la kurandaranda nje. Pale jela, Dunia anakumbana na mateso ya kila aina. Dunia anajenga urafiki na mmoja wa wafungwa kwa jina Mpoto. Inasadifia kuwa siku ya Dunia ya kutoka jela ndio Mpoto anatoka jela. Mpoto alikuwa ameshikwa kwa kosa la wizi. Mpoto na Dunia wanaishi pamoja. Mpoto anamwingiza Dunia katika wizi na hazikupita siku nyingi bila wao kushikwa. Wanafungwa tena kwa kosa la wizi. Dunia anajuta sana kwa kuhusiana na Mpoto. Wanapomaliza kifungo chao, Dunia anaamua kurudi kwao Kibaoni na kumwomba babake msamaha.

Kwa upande mwingine, Yasibu anafika Mwambao na kupata watu waliomjali sana; Fakiri Pori na Maua Pori. Wanamtunza pamoja na mtoto wake Yadhuru kama dada yao.

Yasibu hakuridhika na malezi aliyopata kwa kina Fakiri. Anatamani sana kuolewa na tajiri mmoja katika mji wa Mwambao. Kwa sababu ya tamaa ya pesa, Yasibu anatorokea kwa tajiri huyu kwa jina Fadhili.Kutokana na uhusiano wao, Yasibu anapata mtoto mwingine kwa jina Majuto. Baada ya siku chache Fadhili anamfukuza. Yasibu anajiingiza katika anasa na starehe. Anatumia vileo vya kila aina. Baadaye, Yasibu anaamua kurudi kwa Fakiri. Anapofika, Fakiri anampokea kwa furaha. Maisha ya Fakiri na Maua yalikuwa yamebadilika. Baada ya Maua kupata kazi, walihamia mtaa wa kifahari. Baada ya siku mbili maradhi yanamjia Yasibu, Fakiri na dadake Maua wanampeleka hospitali ya gharama kubwa ili apate afueni lakini hazikupita siku nyingi Yasibu aliaga Dunia. Fakiri na dadake wanafanya ada zote za mazishi na kumzika. Baadaye wanawaandikia wazazi wa Yasibu waraka ili kuwajuza kuhusu kifo cha Yasibu.

### 2.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Tumaini* (2006)

Riwaya ya Tumaini ilichapishwa mwaka wa 2006. Hadithi inahusu utamaduni, na jinsi unavyoathiri malezi ya watoto. Mhusika mkuu katika riwaya hii ni Tumaini, mwanawe Mzee Masumbuko na Bi. Amina. Mzee Masumbuko anashikilia utamaduni sana na angefanya lolote ili kuulinda. Kulingana na utamaduni wa jamii hii, msichana alipaswa kutahiriwa na kuolewa. Mzee Masumbuko anaamua kumpasha tohara Tumaini akielekea darasa la nane. Jambo hili halimfurahishi Tumaini kwa kuwa anajua akipashwa tohara hataweza kuendelea na masomo badala yake angetafutiwa mume amuoe.

Hadithi inapoanza, Tumaini anatoka kwao usiku. Anafungua mlango taratibu ili asiwaamshe waliolala. Tumaini anaamua kutoroka kwa kuwa hakuwa na lingine la kufanya. Hii ni baada ya kumshawishi babake ili aweze kuelewa dhamira yake ya kuendelea na masomo lakini hakumwelewa. Mamake naye alikuwa kama bubu kwa

familia. Hangesema lolote kumpinga Mzee Masumbuko hivyo, hangemsaidia Tumaini. Anaamua kwenda kwa shangazi yake, Bi. Halima kwa kuwa alidhamini masomo na angemwelewa na kumsaidia.

Mzee Masumbuko anapogundua kuwa Tumaini ametoroka, anamfukuza mkewe Bi. Amina. Anamwambia akamtafute kwa kuwa wamepanga jambo hilo na Tumaini. Bi. Amina anaenda kwa kakake Yusuf kumtafuta Tumaini. Idi kakake Tumaini, anatumwa kwa Bi. Halima ili amtafute Tumaini. Idi anapofika kwa Bi. Halima, anamdharau Tumaini kwa kumwambia kuwa alitoroka ili asitahiriwe. Baada ya Bi. Amina kumkosa Tumaini kwa Yusuf anaamua kwenda kumtafuta kwa dadake Bi. Halima na kumpata huko. Bi. Amina na dadake wanapanga jinsi Tumaini ataweza kusoma bila kumfahamisha Mzee Masumbuko.

Bwana Masumbuko anaamua kumtafutia Tumaini mume mbali na kwao. Anaamua kumuoza bintiye mbali na kwao kwa kuogopa vitisho vya shemeji zake. Anamtembelea rafikiye wa zamani, Suleumani bin Mabruk ambaye alikuwa amejuana naye katika harakati za kibiashara.

Baada ya juma moja, Mzee Masumbuko anarejea nyumbani na kumjulisha mkewe kuwa baada ya siku tatu kungewasili wageni. Hakumweleza dhamira ya kuja wageni hao. Bi. Amina anaanza kujiandaa kuwapokea wageni hao kama alivyoshauriwa lakini akashuku kuwa kuna jambo na akamweleza dadake Bi. Halima na kakake Yusuf.

Siku ya wageni kufika inawadia, wazee wanakusanyika nyumbani kwa Mzee Masumbuko. Hakuwafahamisha nia ya kuja wageni hao. Wageni wanapofika wanaeleza kinagaubaga kuwa wameleta posa ya Mabruk ili kuendeleza uhusiano kati ya familia hizo

mbili. Kusikia hayo, Yusuf anaruka na kuuliza posa hiyo ilimhusu Mabruk na nani. Anapoelezwa kuwa ni ya Tumaini, anamgeukia Mzee Masumbuko kwa hamaki na kumuuliza kwa nini anamposa mtoto wao mchanga anayesoma shule.

Tumaini aliweza kuendelea na masomo yake. Alitia bidii masomoni. Anapomaliza mtihani wa darasa la nane, anaamua kutafuta kazi ili aweze kumsaidia shangaziye. Anapata kazi kama kijakazi kwa Chifu Andrea. Anafanya kazi kwa bidii na Bi. Selina anampenda sana. Chifu Andrea anaanza kumletea Tumaini zawadi. Jambo hili linamtia wasiwasi Tumaini kwani alikuwa ameonywa kuhusu tabia za chifu Andrea. Majuto, mwanawe Chifu Andrea anaanza kumnyemelea Tumaini na siku moja anataka kumshika kwa nguvu. Mambo haya yanamfanya Tumaini arudi kwa Bi. Halima.

Majibu ya mtihani wa darasa la nane yanatoka. Tumaini alikuwa amefuzu mtihani ule. Alikuwa miongoni mwa wanafunzi watano waliofaulu na kuletewa barua za kujiunga na shule ya upili. Wanafunzi hawa wangepata ufadhili. Babake anaungana na Chifu Andrea ili Tumaini aondolewe kwa orodha ya watakaopata ufadhili. Tumaini anagundua jambo hili, anabeba kijikaratasi chake kwa kikao ambacho kilikuwa kinajadili watakaopewa ufadhili na kupewa ufadhili.

Tumaini anajiunga na shule ya Milimani Mission school. Anajitahidi sana hasa katika masomo ya Sayansi kwani alitaka kuwa daktari. Kwa upande mwingine, binamuye Riziki anajiunga na chuo cha ualimu baada ya kidato cha nne. Shabani anawazomesha bila shida kwa sababu ya hazina aliyookota. Baada ya kuichimbia chini kwa mwaka mmoja, aliifukua na kutafuta wateja kwa siri. Aliuza bila matatizo akamsomesha mwanawe Riziki na Tumaini.

Kwa upande mwingine, dada zake Tumaini hawakupata elimu kwa sababu ya tamaa ya baba yao. Mashaka anafanya vyema katika mtihani wa darasa la nane lakini hakuendelea na masomo. Mzee Masumbuko alipokea mahari ya Mashaka, akamwoza kwa lazima kwa Mzee Lusimbo kama mke wa tatu. Mzee huyo alikuwa na umri mkubwa sawa na babake Mashaka hivyo hawakusikilizana kabisa. Rehema hakujiunga na darasa la nane kwani babake aliletewa posa na akaolewa.

Chifu Andrea hakujali malezi ya mwanawe Majuto. Majuto alikuwa mtukutu shuleni na hata alipofanya makosa babake alimtetea na kurudi shule. Athari ya hayo ni kuwa Majuto aliacha shule na kuanza tabia za wizi. Alivunja duka za watu na mwishowe alifungwa.

Tumaini anatia bidii masomoni. Wanapofanya mtihani wa kidato cha nne, Sifa, rafikiye anamtembelea Tumaini. Nia yake ni kuwa anataka wawe wapenzi na wafunge ndoa. Tumaini anakataa wazo hilo kwani anataka kuendelea na masomo yake. Bi. Maimuna, mamake Sifa anafurahishwa na jambo hilo na kwenda kwa Mzee Masumbuko ili aonane na Bi. Amina. Anamweleza mamake Tumaini kuwa ni jambo nzuri iwapo mwanawe Sifa angemuoa Tumaini. Bi. Amina anakasirishwa na jambo hilo na kusema kuwa mwanawe lazima aendelee na masomo.

Matokeo ya mtihani waliofanya Tumaini yanatangazwa. Tumaini alikuwa amefanya vyema zaidi. Tumaini anachaguliwa kujiunga chuo kikuu kusomea shahada ya udaktari katika taaluma ya matibabu. Sifa naye anachaguliwa kusomea shahada ya udaktari katika taaluma ya meno. Tumaini na Sifa wanaendelea kuwa marafiki. Wanaahidiana kwamba mapenzi yao watayaendeleza wakimaliza masomo. Riwaya hizi mbili zinaonyesha jinsi

jamii inavyowalea watoto, asasi na hali zinazochangia malezi ya watoto na athari za malezi hayo.

### 2.3 Mbinu za Malezi ya Watoto Katika Riwaya Teule

Waandishi mbalimbali wameshughulikia suala la malezi ya watoto. Kulingana na Deater, Ivy na Petrill (2006) mbinu za malezi ya watoto ni njia ambazo huwawezesha wazazi na watoto kushirikiana katika hali zote, ziwe za kiakili, kidini na kijamii. Mawazo haya yanaungwa mkono na Berk (2007) ambaye anasema kuwa mbinu za malezi ni njia ambazo humwezesha mtoto kuishi katika mazingira bora na kujenga uhusiano mwema na wazazi na wanajamii. Ngwiri (2008), anaeleza kuwa kupitia kwa mazungumzo na matendo ya wazazi kwa wanao, watoto huweza kujiamini na kutekeleza mambo kadha katika jamii. Hivyo, walezi wanafaa kutumia mbinu ambazo zitamwezesha mtoto kukua vyema.

Simiyu (2011) anaeleza kuwa mwandishi yeyote wa kazi ya fasihi hutoa mambo anayoandika kutoka kwa mazingira ya jamii fulani ambayo yeye ni mhusika kwa namna moja au nyingine. Kazi yake ya fasihi anayoiumba msanii hutokana na ufahamu wa msanii mwenyewe juu ya maisha na matukio ya jamii hiyo. Mwandishi hudondoa maudhui kutoka kwa jamii fulani. Hivyo basi, suala la malezi ya watoto ni jambo muhimu katika jamii yoyote na waandishi wengi wa fasihi wameliangazia suala hilo. Baadhi ya waandishi hao ni Omar (2004) na Momanyi (2006)

Katika riwaya za *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ya L. Omar na *Tumaini* (2006) ya C. Momanyi, mbinu wanazotumia walezi hutofautiana hata katika familia moja. Wazazi katika familia moja huweza kutumia mbinu zinazopingana. Kwa mfano, katika riwaya ya

*Dunia Mashaka Makuu* (2004), Mashaka anatumia mbinu ya kimabavu na mkewe Bi. Nusura anatumia mbinu ya kimamlaka kuwalea wanao. Walezi hawa pia hawashirikiani katika malezi ya watoto wao. Waandishi wa riwaya teule wameonyesha Mbinu mbalimbali za kuwalea watoto kwa mfano, Malezi ya kimabavu, malezi ya kimamlaka, malezi ya kudekeza, malezi ya kutojihusisha pamoja na malezi ya ushirikiano.

### 2.3.1 Malezi ya Kimabavu

Kwa mujibu wa Cherry na Steven (2017) malezi ya kimabavu ni mtindo wa malezi ambapo wakati wote wazazi huwa wakali. Mzazi anayetumia mbinu hii humdhibiti mtoto kwa ukali zaidi na kuonyesha mapenzi kidogo au kutoonyesha mapenzi kabisa. Malezi haya huwaacha watoto na majeraha mengi ya kimwili na kiakili tangu wakiwa wadogo mpaka wanapokuwa watu wazima. Baadhi ya wazazi wanaotumia mbinu hii huwapiga watoto wao na wengine huwapa adhabu kali zinazowafanya watoto kuwa na majeraha haya.

Wazazi wanaotumia mbinu ya mabavu huwa na matarajio makubwa kutoka kwa watoto wao. Katika mbinu hii, wazazi hutunga sheria kali ambazo lazima zifuatwe na watoto. Kulingana na Baumrind (1991) wazazi hawa hutaka watoto wao wawatii na hali yao katika jamii idumu bila kujali athari ya malezi haya kwa watoto wao. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004), Bwana Mashaka anatunga sheria ambazo watoto wake wangefuata. Kwa mfano, anaeleza Bi. Nusura kuwa Yasibu hafai kufanya kazi yoyote. Pia hangetoka nyumbani kwao ila tu anapoenda shule. Bwana Mashaka anadhibitisha kwa kuuliza;

> ...nimemuona Yasibu akitumwa humu nyumbani. Haifai! Watumishi wapo. Kazi yake nataka iwe ni kudurusu masomo ya kadiri yake tu basi! Asifanye kazi nyingine (Omar: 4).

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), Mzee Masumbuko anatunga sheria kali ambazo zilifaa kufuatwa na watoto wake. Mojawapo ya sheria ni kwamba wasichana wake wanapomaliza mtihani wa darasa la nane wangepashwa tohara na kuozwa. Hakuna msichana alifaa kukiuka sheria hii. Sheria hii ilikuwa tatizo kubwa kwa Tumaini kwa sababu alitaka kuendelea na masomo yake. Alijua kuwa babake hatakubaliana naye ila angepewa adhabu kali. Hivyo, anamua kutoroka nyumbani. Dada zake Tumaini, Mashaka na Rehema wanapashwa tohara na kuozwa hata kabla ya kuingia darasa la nane. Barua aliyoandikiwa Tumaini na Idi inadhibitisha haya:

> ...Tumaini alijushwa kwamba Rehema hakujiunga na darasa la nane kwani babake aliletewa posa na kisha Rehema akaolewa. Aliolewa na fundi wa baiskeli aliyeitwa Shauri. Mashaka aliamua kusoma lakini lilomkera Tumaini ni kwamba tayari huyu alikwisha tafutiwa mchumba. (Momanyi: 110-111)

Wazazi wanaotekeleza mbinu hii pia huwaadhibu watoto wao bila kuwaeleza sababu za adhabu hiyo. Wao hawawaelezi watoto njia ambazo wanafaa kufuata ili wawe na nidhamu bora. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu*, Bwana Mashaka anamwadhibu Dunia kwa kukosa kwenda shuleni. Hata Dunia anapobadilika na kuamua kurudi shule babake anakataa kumsamehe. Babake Dunia mara nyingi hakumuuliza alivyoendelea. Anapougua homa kali, babake anakataa kumpeleka hospitalini. Haya yanathibitishwa na maneno haya ya mwandishi:

> Dunia aliumwa na jambo jingine moyoni. Hakuelewa kwa nini babake, Bwana Mashaka hakumsamehe. Ijapo alimkosea babake kwa kukosa kwenda shuleni kwa miezi kadhaa na mambo mengine ya utovu wa adabu, hakuelewa ni kwa nini hangeulizwa ili akiri makosa na kuomba msamaha. Bwana Mashaka aliingia chumbani alimolala. Dunia kwa nadra na ni muda tu alipoingia kumhoji, kumhamrisha na labda kumkejeli pasi na sababu ya haja (Omar: 35).

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006) Mzee Masumbuko anawaadhibu wanawe bila kuwaeleza sababu za adhabu hiyo. Hakutaka mtu yeyote aingilie malezi ya watoto wake. Jambo hili lilimsononesha Tumaini sana anapoambiwa na kakake Idi kuwa babake ametayarisha gunia pamoja na majani ya upupu ili amwadhibu Tumaini kwa kutoroka nyumbani ili asipashwe tohara. Tumaini anamweleza Riziki:

> ...naam, upupu. Baba ana mazoea ya kutuadibu kwa kututia ndani ya gunia pamoja na majani ya upupu. Natumaini mnajua jinsi yanavyowasha. Baada ya kulifunga gunia ndi kwa kamba, ndipo anapomchapa anayeadhibiwa hadi fimbo ivunjike vipande vipande. Isipovunjika, nawambia ataendelea kuchapwa hadi mpita njia atokee kumkemea (Momanyi: 28 ).

Santrock (2006), anaeleza kuwa wazazi wanaotumia mbinu hii hawawapi watoto nafasi ya kuchagua kilicho kizuri na kibaya. Wao huwaaamulia watoto kile wanachotaka wafanye. Watoto wanapokosea pia hawapewi nafasi ya kujirekebisha. Wanachukulia kuwa mtoto hafai kukosea na wanakataa kuwasamehea watoto hata wanapobadilika. Katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004), Bwana Mashaka anawaamulia wanawe Yasibu na Dunia kila jambo. Kwa mfano, hakuwaruhusu wanawe kutangamana na wenzao. Aliona jambo hilo kama utovu wa nidhamu. Mwandishi anadhibitisha:

> Siku ambayo hakuenda shule kama leo Jumapili alitarajiwa alale hadi jua la utosini. Mara nyingi aliwaonea wivu watoto wa rika lake walipopita njia kuu karibu na kwao wakitoka mtoni. (Omar: 20)

Bwana Mashaka pia hakuwasamehe wanawe walipokosea. Yasibu anapopata mtoto nje ya ndoa babake anakataa kumsamehe. Uhusiano wake na Yasibu unakatika mtoto Yadhuru anapozaliwa. Anamkasirikia Yasibu kwa kuacha masomo wakati alikuwa akielekea darasa la saba. Maneno ya Yasibu kwa babake Bwana Mashaka yanadhibitisha:

> Baba, Sitarudia tena kosa hilo. Nishaakifishikwa nalo tendo hilo. Nilihadawa baba. Sikugundua mtego. Yasibu alizidi kutaradhia. Aa! Sioni kuwa naweza kukusamehe, Bwana Mashaka alisema. (Omar: 98)

Katika riwaya ya *Tumaini*, Mzee Masumbuko aliwaamulia wanawe kila jambo. Kwa mfano, anawapasha tohara wasichana wake Rehema na Mashaka bila idhini yao. Pia, anawatafutia wanaume wa kuwaoa. Jambo hili linamkasirisha Tumaini sana na anaamua kutoroka kwa sababu hakuelewa kwa nini babake hangempa uhuru wa kujieleza. Barua ya Idi kwa Tumaini inaeleza hivi:

> Katika barua hiyo, Tumaini alijushwa kuwa Rehema hakujiunga na darasa la nane kwani babake aliletewa posa na kisha akaolewa (Momanyi: 103).

Tumaini anapopita mtihani wa darasa la nane, babake anakataa kumlipia karo za shule ya upili. Zaidi ya hayo, anahusiana na Chifu Andrea ili Tumaini atolewe kwa orodha ya wanafunzi waliostahili kupewa ufadhili. Mzee Masumbuko anaona kuwa Tumaini alimkosea kwa kukataa kupashwa tohara na kuolewa na mume aliyemchagulia. Mwandishi anaeleza:

> ...babake msichana yule hakutaka apewe usaidizi wowote. Alisema (Momanyi: 103)

Mambo wanayotekeleza wahusika katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006) ni mambo halisi yanayofanyika katika jamii kama unavyoeleza mhimili wa nadharia ya uhalisia. Kwa mfano, utafiti uliofanywa na Ashiono (2013) katika kaunti ya Mombasa eneo la Kisauni unaonyesha kuwa baadhi ya wazazi hutumia mbinu ya mabavu kuwalea watoto. Wazazi hawa hutunga sheria kali ambazo ni lazima watoto wazifuate. Wasipofuata sheria hizo huadhibiwa vikali. Anaeleza kuwa asilimia kubwa ya wanaotumia mbinu hii ni kina baba. Utafiti huu unaonyesha kuwa watoto wanaopata malezi ya aina hii hawafanyi vyema shuleni ikilinganshwa na watoto wanaolelewa kwa

mbinu ya kimamlaka. Pia, katika Gazeti la *Daily Nation* Bett (2016) anaeleza kisa cha msichana mmoja wa miaka kumi katika kaunti ya Marsabit aliyelazimishwa na babake kuolewa na mzee wa miaka arobainne. Msichana huyu anapashwa tohara kama njia ya kumtayarisha kuwa mke. Anapokataa kuozwa, babake anamfungia kwa nyumba ili asiweze kutoroka. Baadaye msichana huyu anaokolewa na polisi. Kulingana na utafiti uliofanywa na shirika la UNICEF (2016) katika kaunti ya Turkana, thuluthi moja ya wanawake waliolewa wako chini ya miaka kumi na nane. Ripoti hii inadhihirisha kwamba wengi wa wanawake hawa hulazimishwa kuolewa na hawapewi nafasi ya kujitetea.

### 2.3.2 Malezi ya Kimamlaka

Darling (2014) anaeleza kuwa malezi ya kimamlaka ni mtindo wa malezi ambapo wazazi hutoa maagizo bora na sheria bora zinazowashirikisha wazazi kikamilifu katika kuwalea watoto. Berk (2007) anaeleza kuwa wazazi wanaotumia mbinu hii huwa na mamlaka kwa watoto wao ila si kwa mabavu. Wazazi hutunga sheria na huwaeleza watoto sababu za sheria hizo. Pia, watoto hupewa nafasi ya kujieleza na kutoa hoja zao. Katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) kuna wahusika ambao wanatumia mbinu hii. Kwa mfano, Bi. Nusura anawasikiliza wanawe na kuwaelewa. Bwana Mashaka anapokataa kumsamehe Dunia na Yasibu, anamsihi mumewe awasamehe wanawe. Anaelewa kuwa watoto wanafaa kupewa nafasi ya kubadilika hata wanapokosea. Bi. Nusura anasema haya kudhibitisha:

> ...Sivyo hivyo hufanyavyo. Aa! basi tuseme huna tena huruma na mtoto huyu kana kwamba siye wewe uliyemzaa katika handaki hii ya ulimwengu?...tangu mtoto huyu awe mjamzito hadi akajifungua hatujakuwa na raha naye...na tuyatie kikomo sasa mambo hayo, tumpatie nafasi ya kupumua (Omar: 96).

Bi. Nusura anaposhindwa kumshawishi Yasibu arudi nyumbani, anamshauri Yasibu kabla ya kutoroka. Anamweleza Yasibu kuwa ingawa baba yao amewapuuza, yeye kama mamake hamruhusu kutoroka. Anamweleza kuwa anafaa ajali maisha kwani asipofanya hivyo huenda akaangamia. Bi. Nusura anamkaririia Yasibu Shairi na kusema:

> Johari za mtu ni mbili
> Akili na haya
> kuzikosa ni muhali
> Maisha usipoyajali
> Utaangamia! (Omar: 106- 107)

Mwalimu Busara pia anaendeleza mbinu hii ya malezi. Dunia anapotoroka shule na kuamua kurudi tena anampa nafasi ya kujirekebisha. Anamshawishi Bwana Mashaka amsamehe Dunia lakini anakataa. Mwalimu huyu anakubali Dunia aendelee na masomo kwa imani kuwa mtoto akipewa nafasi huweza kubadilika. Mwandishi anadhibitisha haya:

> ...Dunia aliishi kwa rehema za Mwenyezi Mungu, akapata riziki kwa kudoea kwa marafiki na wafadhili, ijapo nyumbani kwao vyakula vilidoda kwenye maghala. Huko kupata elimu kulikuwa kwa bahati nasibu. Hangeendelea kusoma shule thama na imani ya Mwalimu Mkuu, Bwana Busara (Omar: 102)

Shaban na mkewe Bi. Halima katika riwaya ya *Tumaini* walimlea mwanao Riziki kwa kutumia mbinu hii. Waliweza kumshauri mwanao vyema. Kwa mfano, wakati mwingi Shaban alipenda kumsomea Riziki mashairi au hadithi za kale kama vile *Mfalme na Binti Wake* au *Safari za Guliva*. Kupitia kwa babake, Riziki alijifunza mengi akawa mweledi sana katika masomo. Mwandishi anadhibitisha:

> ...alipenda kumsomea mwanawe Riziki mashairi au hadithi za kale kama vile *Mfalme na Binti Wake* au *Safari za Guliva*...Riziki alijifunza mengi akawamweledi sana katika masomo (Momanyi: 11).

Tumaini anapotoroka na kwenda kwa shangaziye Bi. Halima, wazazi hawa wanamtunza vyema. Wanamshauri na kumhakikishia kuwa angeendelea na masomo yake bila pingamizi yoyote. Bi Halima anamhakikishia Tumaini kwa kusema:

> Wakati huu tulio nao hakuna mzazi atakayemlazimisha binti yake kutahiriwa, la sivyo, atachukuliwa hatua za kisheria. (Momanyi: 25).

Babake Sifa, Mzee Majaliwa, pia anamhimiza mwanawe kutia bidii masomoni. Sifa ananunuliwa zawadi nyingi kwa kutia bidii masomoni. Tumani anasikitika kwa kuwa licha ya yeye kufaulu vyema katika masomo, babake hajawahi kumtuza hata siku moja. Mwandishi anadhibitisha haya:

> ...Alikumbuka jinsi Sifa alivyonunuliwa baiskeli na babake, Mzee majaliwa kwa sababu ya juhudi zake masomoni (Momanyi: 22).

Matukio katika riwaya za *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006) ni ya kweli na yanazingatia uyakinifu wa maisha kama unavyoeleza mhimili wa nadharia ya uhalisia kuwa msanii husawiri na kueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Kwa mfano, utafiti uliofanya na Maigallo (2015) katika kaunti ya Kiambu unaonyesha kuwa wazazi wengi hutumia mbinu ya kimamlaka kuwalea watoto wao. Wao hutunga sheria na kuwaeleza watoto sababu ya sheria hizo. Watoto pia hushauriwa na wazazi wao. Utafiti huu unaonyesha kuwa asilimia sabini na nane ya kinababa hutumia mbinu ya kimamlaka na asilimia themanini na saba ya kina mama hutumia mbinu hii.

Katika gazeti la *The People Daily*, Wachira (2017), anaeleza kisa cha mzee mmoja katika kaunti ya Kiambu aliyechukua jukumu la kuwalea watoto wake wawili wa kike baada ya kifo cha mama yao. Anaeleza kuwa kuwalea wasichana waliobaleghe sio kazi rahisi lakini anatia juhudu kuwalea. Jambo la kwanza analofanya ni kuwa rafiki wa watoto wake. Anawashauri na kusikiliza maoni yao. Msichana wake anapofikia umri wa

miaka kumi na mitano anampeleka mahali ambapo angepewa mawaidha badala ya kumpasha tohara. Hii inadhihirisha kuwa mambo anayoandika mwandishi huzingatia uyakinifu na uhakika wa maisha.

### 2.3.3 Malezi ya Kudekeza.

Getao (2016) anaeleza kuwa malezi ya kudekeza ni aina ya malezi ambapo wazazi huepuka migogoro na mapambano yoyote na watoto wao. Walezi wanaotumia mbinu hii huwapenda watoto wao kupita kiasi. Watoto hufanya mambo yanayowafurahisha bila wazazi wao kujali athari za mambo hayo. Mbinu hii hutumiwa sana na wazazi wenye ufanisi wa kifedha, ambao mara nyingi huwaona watoto wao kama warithi wa mali yao.

Kulingana na Santrock (2007), walezi wanaotumia mbinu hii huwapenda watoto wao kupita kiasi. Hawatungi sheria zozote za kuwaongoza watoto wao. Wao huwaacha uhuru wafanye watakalo. Ngwiri (2008) anaeleza kuwa kuna tofauti kati ya wazazi wanaotumia mbinu ya kudekeza na wanaotumia mbinu ya kupendelea. Anasema kuwa wazazi wanaotumia mbinu ya kudekeza hawaweki sheria zozote za kuwaongoza watoto wao. Watoto hufanya watakacho. Wazazi wanaotumia mbinu ya kupendelea nao huwaharibu watoto kwa kuwapa vitu ambavyo hawavihitaji. Bwana Mashaka katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* anaendeleza mbinu hii. Anamuacha bintiye Yasibu ajiamulie atakacho. Hataki Yasibu afanye chochote nyumbani ila tu kudurusu masomo. Anaamini kuwa kazi zote nyumbani zinafaa kufanywa na wafanyakazi. Yasibu anaposema kuwa anataka uhuru, babake anampa uhuru wa kufanya atakacho bila kufikiria athari ya uhuru huo. Mzee Mafusho anathibitisha kwa kusema:

> ...lingekuwa jambo mwafaka lau mngemruhusu ntoto wenu asaidiane na watumishi katika baadhi ya kazi. Kumbana haikuwa sawa. Hapa ndipo wazazi wengi wanapoteleza katika kulea. Kushindwa kuchipima chiasi cha kumwatia mtoto. Ijapo kaifai kumbana ntoto, kumdekeza pia kaifai. (Omar: 43).

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), Mzee Masumbuko anaendeleza malezi haya kwa mwanawe Idi. Anamdekeza kwa sababu ni wa kiume. Hakutaka mtu yeyote aingilie malezi ya Idi. Idi alipenda sana kuwatukana dada zake kwa kuwa aliwaona kama watumishi tu pale kwao. Hata Tumaini anapolalamika kuhusu tabia za Idi, babake anamtetea na kusema kuwa alifaa kuwa na moyo mgumu kama yeye kwa sababu ni mtoto wa kiume. Chifu Andrea pia anatumia mbinu hii kumlea mwanawe Majuto. Mara kadha Majuto anafukuzwa shule kwa sababu ya utovu wa nidhamu lakini Chifu Andrea anamtetea mwanawe huku akitumia cheo chake. Chifu Andrea pia anawahonga watu waliolalamika kuhusu Majuto ili asitiwe mbaroni. Mwandishi anadhibitisha:

> ...Maji yalipozidi unga, alihiari kuwahonga walalamishi ilimradi wasimtie Majuto kifungoni. Kijana huyu aliengwaengwa na wazazi wake, huku akitimiziwa kila alilotaka. Kwa sababu ya kudekezwa, alijawa na wingi wa tabakuri. (Momanyi: 71).

Aina hii ya malezi inatumiwa sana na walezi wa kisasa. Wao hujihusisha sana na mambo wanayopenda watoto bila kujali athari ya mambo hayo. Hivyo basi, kama inavyoeleza mihimili ya nadharia ya uhalisia kuwa kazi ya msanii huwasilisha ukweli kama ulivyo katika jamii, kuna visa vinavyodhihirisha haya. Kwa mfano, Wambui (2010) anaeleza kisa cha mzazi mmoja katika eneo la Kiambu ambaye hakutaka mtu yeyote aingilie malezi ya watoto wake. Mzazi huyu anakasirika sana wanawe wanapoadhibiwa na dadake wakikosea. Anasema kuwa ni bora kuwaacha watoto wajiamulie wanachotaka ili waweze kujitegemea. Kulingana na mlezi huyu, watoto wanapoelekezwa na kuadhibiwa, hushindwa kupambana na changamoto za maisha.

### 2.3.4 Malezi ya Kutojihusisha

Awasthi (2017) anaeleza kuwa malezi ya kutojihusisha ni aina ya malezi ambapo wazazi hawawashughulikii wanao. Anaeleza kuwa wazazi huepuka majukumu ambayo wanafaa kuwatimizia watoto wao. Katika mbinu hii pia, wazazi hawajihusishi na maendeleo ya watoto wala hawana malengo yoyote kwa watoto wao.

Baumrind (1991) anaeleza kuwa wazazi wanaotumia mbinu hii ya malezi huwatelekeza watoto wao. Hawachangii kwa vyovyote vile katika malezi ya watoto wao. Anaeleza kuwa kuna sababu zinazowafanya wazazi kuwatelekeza watoto wao. Hizi ni pamoja na kukosa muda na watoto wao, matatizo ya nyumbani na matumizi ya dawa za kulevya. Anaendelea kusema kuwa baadhi ya wazazi hutumia mbinu hii ili watoto wao waweze kujitegemea. Baadhi ya wazazi wanaotumia mbinu hii husema kuwa watoto wanapofanyiwa kila kitu na wazazi wao baadaye huwa wavivu.

Katika aina hii ya malezi, mzazi hajihusishi na maendeleo ya mtoto wala hana malengo yoyote ya mtoto. Katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004), Bwana Mashaka anakosa kujihusisha na malezi ya wanawe Dunia na Yasibu. Mwanzoni, anawashughulikia wanawe vyema lakini wanapokosea anapuuza majukumu yake kama mzazi. Kwa mfano, Yasibu anapoacha shule kwa sababu ya ujauzito, babake anamkasirikia sana na kukosa kuzungumza naye. Hakujali alichokula au alivyoendelea pamoja na mwanawe Yadhuru. Jambo hili linamkera Yasibu sana na kuamua kutoroka. Mwandishi anasema:

> Mzee huyu hakuwa na uhusiano na Yasibu. Alimkasirikia Yasibu kwa kuacha masomo wakati akielekea darasa la saba.Yasibu alishindwa kwa nini babake aliacha kumsaidia na kumsetiri. (Omar: 94)

Dunia pia anakumbwa na tatizo sawa na Yasibu. Anapoacha shule kwa sababu ya utovu wa nidhamu, babake anamlaumu kwa kusema kuwa kuzaliwa kwake kulikuwa nuksi kwa familia yake. Dunia anapobadilisha mwenendo wake babake anakataa kumsamehe. Anakataa kumlipia karo za shule na hakujali alikolala au alikokula. Alipokuwa mgonjwa babake hakushughulika naye. Mwandishi anasema:

> Bwana Mashaka pia hakumwuliza Dunia akiingia wala akitoka, alichokula wala alichokitapika. La zaidi ni kuwa karo za shule nazo hakumlipia. Dunia alitamani apate nafasi ya kuzungumza na mzee wake mambo mengi ya shuleni na yale ya nyumbani lakini baba mtu hakudiriki. (Omar: 35)

Mzee Masumbuko anaendeleza malezi haya katika riwaya ya *Tumaini* (2006). Tumaini anapokataa kupashwa tohara na kuolewa kulingana na tamaduni zao, mzee huyu anajitenga kabisa na malezi yake. Anapofaulu katika mtihani wa darasa la nane anashirikiana na Chifu Andrea ili Tumaini asipewe ufadhili jambo ambalo hakufanikiwa kufanya. Mzee Masumbuko pia anakataa kuandamana na mkewe katika sherehe ya Tumaini ya kufaulu kwa mtihani wa kidato cha nne aliyoandaliwa na Bi. Halima na Shaban. Mkewe Bi. Amina anapomshawishi, anamkemea na kumwambia kuwa akiendelea kumkera na mambo ya Tumaini atahakikisha kuwa hata hiyo karamu ya mwanawe hataenda. Mzee Masumbuko anasema:

> "Tuma alinikana siku ile aliyonyanyua mguu na kuhama hapa. Kwa hivyo, yeye si mwanangu."Aende asiende kwangu fahuwa. Mtoto wa kike kama yeye hawezi kuwa fahari kwangu ati kwa sababu amesoma. Fahari yangu ni kumwoza nipate tu mahari yangu kwa sababu elimu yake haitanisaidia chochote. (Momanyi:151).

Waandishi wa riwaya ya *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004) wameeleza ukweli kama ulivyo katika mazingira ya kawaida kama inavyoeleza nadharia ya uhalisia. Kwa mfano, mbinu hii ya malezi inadhihirika katika nchi ya Kenya. Wawira (2013),

anaeleza kuwa katika kaunti ya Embu mkoa wa Manyatta, baadhi ya wazazi hutumia mbinu ya kutojihusisha. Katika utafiti wake, ameonyesha kwamba asilimia tano ya kina baba hawajihusishi na malezi ya watoto wao ikilinganishwa na asilimia mbili ya kina mama ambao hawajihusishi na malezi ya watoto wao.

Katika kaunti ya Kakamega, Mzee mmoja anashtakiwa kwa kuwapuuza wanawe ambao ni vilema. Tunaelezwa kuwa mzee huyu alimkemea na kumfukuza bibiye kwa sababu alijifungua watoto vilema. Watoto hawa hakuwa na uwezo wa kuketi, kusimama na kutembea (Amalemba, 2017). Katika kaunti ya Nyeri wanawake wawili wanafungwa kwa kutelekeza wanao. Jambo hili linawafanya watoto kuugua kwa kukosa lishe bora. (Wangui, 2017).

### 2.3.5 Malezi ya Ushirikiano

Scroeder na Mowen (2014), wanafafanua malezi ya ushirikiano kama mbinu ya malezi ambapo wazazi wote hushirikiana katika malezi ya watoto wao. Wanaeleza kuwa katika mbinu hii wazazi hutunga sheria za kuwaongoza wanao pamoja bila kupingana. Wanajamii pia huchangia katika malezi ya watoto. Hivyo, malezi ya watoto katika mbinu hii si ya mtu mmoja ila ni ya jamii nzima.

Brooks (2012), anaeleza kuwa wazazi ndio huchangia pakubwa katika malezi ya mtoto. Anasema kwamba ingawa watoto wale wakubwa kwa umri, shangazi, na wajomba wana jukumu la kuwalea watoto, wazazi binafsi ndio wanao jukumu kubwa. Anaendelea kusema kuwa malezi ya watoto yanahitaji ushirikiano wa taasisi mbalimbali ili mtoto akue katika maadili, nidhamu na hatimaye kuwa raia mwema kwa taifa lake. Maelezo ya Brooks (2012) yanaungwa mkono na Cherry (2018) ambaye anaeleza kuwa kila

mwanajamii anahitaji kushiriki katika malezi ya watoto ili watoto waweze kupata malezi mema.

Oburu (2011) anaeleza kuwa malezi ya watoto katika familia ambazo wazazi hawaheshimiani ni kama ndoto. Anasema kuwa watoto katika familia nyingi hutatizika kwa sababu ya kukosa ushirikiano katika familia. Mtoto mara nyingi huhitaji mazingira yenye utulivu ili kukua kimwili, kihisia na kiakili. Anaeleza kuwa Nchini Kenya kuna viwango vya kutengana na talaka nyingi. Talaka hizi zinawafanya watoto kukosa malezi mema kutoka kwa wazazi wote.

Wanyama (2015), anaeleza kuwa malezi ya watoto siku hizi ni ya wazazi binafsi. Analinganisha malezi haya na ya jadi ambapo jamii nzima ilichangia katika malezi ya watoto. Anasema kuwa kila mtu mzima alikuwa mzazi wa mtoto yeyote na angeweza kumwadhibu mtoto huyo iwapo angekosea. Siku hizi ukijaribu kumwadhibu mtoto ambaye si wako huenda ukashtakiwa.

Mbinu ya ushirikiano ni muhimu sana katika malezi ya watoto. Wazazi na walezi wanafaa kushirikiana katika kuwalea watoto wao ili watoto wapate malezi mema. Ushirikiano unajitokeza katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) kupitia wahusika Mzee Mafusho na Mwalimu Busara. Mzee Mafusho alimshauri Bwana Mashaka kuhusu malezi ya watoto wake. Bwana Mashaka anapoona kuwa mbinu zake hazifui dafu anaamua kushirikiana na Mzee Mafusho katika malezi ya wanawe. Kwa mfano, Kila alipokumbwa na jambo katika kuwalea watoto wake na familia yake alimwendea rafiki yake Mzee Mafusho. Mwanawe Yasibu anapokaidi amri zake,

anamweleza Mzee Mafusho ili amsaidie kutatua jambo hilo. Bwana Mashaka anamweleza Mzee Mafusho:

> Mwanangu Yasibu hataki tena kutii amri zetu wazazi wake. Mwanangu Dunia amesusia masomo. Hataki hata kuishuhudia milango ya shule licha ya huko kusoma. Mzee Mafusho, mimi mwenzio nimo kwenye kizungumkuti cha mambo. Aa! Basi natukitafute chanzo cha ukaidi wa wano chisha tutafute tiba ya ukaidi huu. (Omar: 42-43)

Mwalimu Busara pia anashirikiana na Bwana Mashaka katika malezi ya Dunia. Dunia anapoamua kurudi shule baada ya kususia kwa muda, Mwalimu huyu anamshawishi Mzee Mashaka amsamehe Dunia na kumlipia karo za shule. Bwana Mashaka anapokataa kumlipia Dunia karo za shule, Mwalimu Busara anamruhusu kuendelea na masomo hadi darasa la nane. Mwandishi anadhibitisha:

> ...Pale Bwana Mashaka alipokoma kulipa karo za mtoto wake, Mwalimu mkuu, Bwana Busara akamdadisi kuhusu jambo hilo. Aliyoyajibu hayakumridhisha Bwana Busara. Sababu za hakuwa na pesa za kuchezea kwa mtoto laghai. Mwalimu Busara alihiari Dunia aendelee na masomo si huruma kwa Bwana Mashaka bali kwa kumsitikia Dunia mwenyewe. (Omar: 81)

Wahusika Bi. Halima, Shaban, Yusuf na Bi. Amina wanaonyesha ushirikiano katika malezi ya watoto katika riwaya ya *Tumaini*. Wote wanashirikiana kuhakikisha kuwa Tumaini amepata malezi yaliyofaa na ametimiza ndoto yake. Kwa mfano, Mzee Masumbuko anapomweleza Bi. Amina kuwa anatarajia wageni, Bi. Amina anajawa na wasiwasi kwa kuwa alijua nia ya mumewe ni kumtafutia Tumaini mume. Anamjulisha dadake Bi. Halima, Shaban, mumewe Bi. Halima na kakake Yusuf. Wote wanafika nyumbani kwa Mzee Masumbuko na kupinga uovu aliokusudia kutenda wa kumuoza Tumaini. Yusuf anasema:

> Sielewi kwamba Mabruk anataka kumposa nani hapa!..yaani Masumbuko umewaleta wageni kutoka huko kumposa mtoto wetu mchanga anayesoma shule? Hii ni aibu gani? (Momanyi: 62)

Shaban na mkewe Bi. Halima wanashirikiana kumlea mtoto wao Riziki. Riziki alikuwa mmoja wa watoto wa kike waliobahatika kupata elimu kwa sababu ya ushirikiano wa wazazi wake. Aliweza kusoma akapata shahada ya ualimu. Wazazi wake walipinga vikali tohara za watoto wa kike na ndoa za lazima. Mwandishi anadhibitisha:

> Riziki alikuwa mmoja wa wale waliobahatika. Hii ni kwa sababu wazazi wake waliuona umuhimu wa kumsomesha mtoto wa kike. Shaban na mkewe Bi. Halima walikuwa mstari wa mbele kupinga ndoa hizo za lazima. Waliamua kumsomesha binti yao Riziki kwa kadri ya uwezo wao. (Momanyi: 15)

Tumaini anapofaulu mtihani wa kidato cha nne shaban na mkewe wanamtayarishia dhifa ya kufana kwa matokeo yake mazuri. Wanawaalika Yusuf, Bi. Namvua, shangaziye Tumaini na wazazi wake. Wote wanaungana pamoja kumpongeza Tumaini kwa matokeo mazuri isipokuwa Mzee Masumbuko. Katika sherehe hii, Yusuf anamkashifu Mzee Masumbuko kwa sababu ya vitendo vya kinyama alivyomtendea binti yake. Anamhakishia Tumaini kuwa atafanya awezalo kuona kwamba babake hataweza kutinga juhudi hizo. Mwandishi anadhibitisha:

> Yusuf alipopewa fursa ya kuongea, alimshtumu Mzee Masumbuko kwa sababu ya vitendo vya unyama alivyomtendea binti yake. Alimhakikishia Tumaini kwamba atafanya kila awezalo kuona kwamba mzazi huyo hataweza kutinga juhudi zake tena. (Momanyi: 152)

Tumaini anapoondolewa kwa orodha ya waliopewa ufadhili, anaenda katika kikao hicho na kumweleza D.O na Afisa wa Elimu. D.O anamwonya Mzee Masumbuko kutoingilia elimu ya mwanawe Tumaini na iwapo angeingilia angefunguliwa mashtaka. Chifu Andrea pia anaonywa kutoshirikiana na wazee kama Masumbuko ili kuzorotesha elimu ya mtoto wa kike. Mwandishi anadhibitisha kwa kusema:

> Mzee Masumbuko alifika kwa D.O ambaye alimuonya kutoingilia elimu ya mwanawe Tumaini. Endapo angeenda kinyume na haya, basi angefunguliwa mashtaka...Chifu Andrea alionywa kutoshirikiana na wazee kama Masumbuko kuzorotesha elimu ya watoto wa kike. (Momanyi: 104)

Malezi ya aina hii ni ya kweli na yameshuhudiwa humu nchini. Haya ni sawia na nadharia ya uhalisia inayoeleza kuwa waandishi hueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Kwa mfano, kuna kisa cha wazazi wawili ambao walikuwa na watoto watatu. Wazazi hawa hawakuwa na ushirikiano katika kuwalea watoto wao. Kila mzazi aliwatungia watoto sheria zake ambazo wangefuata. Pia, hawakujadili maendeleo ya watoto wao. Baadaye mtoto mmoja alishindwa kufuata sheria hizi na kuasi. Muiruri (2014). Katika kaunti ya Mombasa eneo la Bombululu, watoto watatu waliokolewa na wanajamii baada ya kurushwa katika dimbwi la takataka na wazazi wao. Wazazi hawa walikuwa wanafuata maagizo ya mganga ambaye alikuwa amewaambia kuwa wakifanya hivyo watatajirika. Jambo hili liliwahuzunisha majirani sana na kupiga ripoti katika kituo cha polisi na watoto wakaweza kuokolewa. Njoka (2017).

### 2.3.6 Hitimisho

Sura hii ililenga kuonyesha mbinu za malezi zinazotumiwa na wahusika katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006). Vigezo vilivyotumiwa ni visa, matukio na mandhari yanayojitokeza katika vitabu hivi. Baadhi ya mbinu za malezi zilizoangaziwa katika sura hii ni mbinu ya kimabavu ambapo wazazi huwatungia watoto sheria kali ambazo wanafaa kufuata. Malezi ya kimamlaka pia yameelezwa ambapo wazazi huwapa watoto mamlaka ila si kwa mabavu. Malezi ya kudekeza na kutojihusisha pia yameelezwa. Mbinu ya ushirikiano pia imeangaziwa ambapo wazazi hushirikiana katika malezi ya watoto wao. Sura hii imeonyesha kuwa ili wazazi waweze kuwalea watoto vyema lazima pawe na ushirikiano kati ya wazazi wote na wanajamii. Nadharia ya

uhalisia imetumika kuonyesha jinsi masuala yaliyoshughulikiwa na waandishi hujitokeza katika hali halisi. Hii ni kwa sababu mwandishi haandiki kutoka ombwe tupu. Msukumo wa kuandika hutokana na mambo yanayotendeka katika jamii. Uchanganuzi huu umegusia lengo la utafiti huu ambalo ni kubainisha mbinu za malezi zinazojitokeza katika riwaya teule.

Sura itakayofuata itaangazia asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto na mambo yanayoathiri mbinu wanazotumia wazazi kuwalea watoto wao.

# SURA YA TATU

# ASASI NA HALI ZINAZOCHANGIA KATIKA MALEZI YA WATOTO KATIKA RIWAYA TEULE

## 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili mbinu za malezi wanazotumia walezi katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006) zilichunguzwa. Mbinu wanazotumia walezi katika riwaya hizi ni pamoja na mbinu ya kimabavu, mbinu ya kimamlaka, mbinu ya kudekeza, mbinu ya kutojihusisha na mbinu ya ushirikiano.

Katika sura hii, mtafiti amechunguza asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto. Haya ni mambo ambayo yanawachochea walezi kutumia mbinu tofauti katika malezi ya watoto wao. Mhimili wa nadharia ulitumiwa kuchanganua sura hii ni: Wahusika huwa halisi na lugha wanayotumia huwa rahisi na inayoeleweka. Kulingana na Wamitila (2005), wanauhalisia hujifunga kwenye wahusika wa kawaida na wanaoweza kupatikana katika jamii halisi. Huyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao. Wanauhalisia pia huonyesha mandhari na mazingira ya kawaida wakati wa kuandika kazi zao. Mwandishi hivyo basi, anafaa kuyaakisi maisha ya jamii katika ngazi ya kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa. Mwandishi huwajenga wahusika wake katika hali za kawaida za maisha, matukio na mandhari ya kawaida katika jamii.

Kulingana na Baumrind (1991) kila mzazi huwa na njia tofauti za kuwalea watoto wake. Njia hizi hutofautiana kutoka mzazi mmoja hadi mwingine. Tofauti hizi, zinatokana na utamaduni wa jamii husika, kiwango cha elimu cha wazazi, uana na jinsia, na familia.

Fabrizao (2017) anaeleza kuwa kila mzazi huwa na matarajio makubwa kwa mtoto wake na hutumia mbinu mbalimbali za malezi ili kuhakikisha kuwa watoto wamefanikiwa maishani. Anaendelea kusema kwamba, ingawa wazazi hujitahidi kutumia mbinu za malezi zinazofaa kuwalea watoto wao, mbinu hizi huchochewa na mambo mbalimbali katika jamii. Kwa mfano, uwezo wa kiuchumi wa wazazi, elimu, utamaduni na familia.

Utafiti huu kuhusu asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto katika riwaya teule za *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006) umeshughulikia utamaduni, familia, jinsia, elimu, ubinafsi na tamaa ya wahusika, hadhi au cheo cha wahusika, ulevi wa wazazi na taasubi ya kiume kama mambo yanayoathiri mbinu wanazotumia walezi kuwalea watoto wao.

### 3.1 Asasi ya Kitamaduni

Kulingana na Santrock (2007) utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mitazamo yao na tajriba zao za kuendesha maisha zinazowatofautisha na jamii nyingine. Anaeleza kuwa ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na jamii kukithi utashi na maendeleo yake. Kulingana na Santrock (keshatajwa), malezi ya watoto yaliathiriwa na utamaduni na itikadi za jamii husika. Hii ni inatokana na kuwa kila jamii huwa na utamaduni wake.

Julie (2017) anaeleza kuwa utamaduni hubadilika kutoka jamii moja hadi nyingine. Anaeleza kuwa mabadiliko ya kitamaduni huathiri mbinu wanazotumia wazazi kuwalea watoto wao. Tofauti hizi zinatokana na kuwa kila jamii huwa na mbinu mahsusi na kanuni za kuwalea watoto wao. Kanuni hizi huathiri maadili, tabia na mbinu zinazotumiwa kufunza maadili hayo.

Mowin (2018) anaeleza kuwa utamaduni wa jamii husika huathiri mbinu wanazotumia wazazi kuwalea watoto wao. Anasema kuwa jinsi mzazi alivyokua, maadili aliyopata kutoka kwa jamii yake na mila na desturi za jamii hiyo huathiri jinsi anavyowalea watoto wake. Hivyo, malezi ya watoto hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kwa sababu utamaduni huwa tofauti kutoka jamii moja hadi nyingine.

Katika riwaya za *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006), utamaduni ni mojawapo ya asasi zinazoathiri mbinu wanazotumia wazazi kuwalea watoto wao. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) utamaduni umeathiri malezi ya watoto. Bwana Mashaka anachukulia kuzaliwa kwa Dunia kama laana kwa familia yake. Sababu ni kuwa Dunia alizaliwa wakati mamake alipigwa na ng'ombe nusura aage dunia. Kila wakati tatizo linapotokea katika familia yake humlaumu mtoto huyo. Sababu ni kuwa jamii hii iliamini kuwa mtoto anayezaliwa kwa mkasa hubashiri laana katika familia. Kwa mfano, Dunia anaposusia kwenda shuleni Bwana Mashaka anakataa kumshughulikia kwa vyovyote. Anasema kuwa Dunia ni nuksi kwa familia yake. Mashaka anamweleza mzee Mafusho:

> "Eeh Mzee Mafusho, mtoto huyu alisusia kusoma bila sababu yoyote dhahiri. Huo ndio ugomvi wangu halisi wa mimi naye, hata simshughulikii kwa jambo lolote. Akirejea nyumbani ni sawa na asiporejea ni sawa. Isitoshe, usisahau itikadi zetu. Mtoto azaliwaye kwa mkasa haleti baraka nyumbani. Usisahau mtoto huyu alizaliwa pale mamake alipopigwa pembe na ng'ombe, nusura kuaga dunia. Amekuwa na vituko kadha wa kadha nyumbani licha ya huku kukataa kwake kusoma."(Omari: 68-69)

Mzee Mashaka anakataa kumpeleka Dunia hospitali kwa kusema kuwa anajifanya. Anamkemea kwa kukosa kuamka asubuhi. Anapoelezwa na Bi. Nusura kuwa Dunia ni mgonjwa anasema kuwa anajifanya na kumkumbusha mkewe kuwa Dunia si wa heri kwa

kuwa kuzaliwa kwake kulikuwa kwa nuksi. Hamtimizii mahitaji yake ya kimsingi kwa kushikilia ushirikina.

Bwana Mashaka anakataa kumsamehe mwanawe hata anapobadilisha mienendo yake. Haamimi kuwa Dunia amebadilika. Ingawa kwa Bwana Mashaka kulijaa vyakula tele, Dunia anakula kwa marafiki wake. Mzee huyu anakataa katakata kumlipia karo za shule. Hivyo, Dunia anasoma kwa hisani ya Mwalimu Busara. Dunia anashangaa kwa nini babake hangemsamehe na kumchukulia kama watoto wengine. Anaona kwamba mambo yote yanatendeka kwa kudura za mwenyezi Mungu na ni ushirikina kwa mwanadamu kuziamini desturi na itikadi zinazomsahau Mungu. Mwandishi anasema:

> ...Dunia aliishi kwa rehema za mwenyezi Mungu, akapata riziki kwa kudoea kwa marafiki na wafadhili, ijapo nyumbani kwao vyakula vilidoda kwenye maghala. Huko kupata elimu kulikuwa kwa bahati nasibu. Hangeendelea kusoma shule thama na imani ya mwalimu mkuu Bwana Busara...Kwa nini babangu hanisamehe? Ni nani asiyekosea? Ni nani atakayemzindua mzee huyu aubaini ukweli? Dunia alijiuliza (Omari: 101-102).

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), mwandishi ameonyesha utamaduni kama mojawapo ya asasi zinazoathiri malezi ya watoto. Mwandishi amemjenga Mzee Masumbuko kama mmoja wa wahusika wanaozingatia utamaduni kwa kina. Anaweza kufanya lolote ili kulinda utamaduni wa jamii yake. Mojawapo ya itikadi za jamii ya Tumaini ni kupashwa tohara. Jamii hii ilichukulia jambo hili kwa uzito sana.  Kulingana na utamaduni wa jamii hii, pindi msichana alipobaleghe alifaa kupashwa tohara na kuolewa. Itikadi hii iliathiri malezi ya watoto wa kike kwa sababu mara tu wasichana walipopashwa tohara waliolewa na kuacha masomo ambayo ni muhimu kwa maisha ya mtoto. Kwa mfano, Tumaini anapoelekea darasa la saba, babake anapanga jinsi atakavyopaswa tohara. Jambo hili

linamtatiza Tumaini sana na ndipo anaamua kutoroka na kwenda kwa Bi. Halima kwa kuwa alikuwa na hamu ya kuendelea na masomo. Mwandishi anasema:

> Tumaini alikuwa amekamilisha darasa la saba katika shule ya msingi ya Kivulini....hakuwa na matumaini ya kuyabadilisha mawazo ya babake kuhusu kuendelea na masomo ya darasa la nane. Matumaini yake yalizidi kufifia babake alipoanza kufanya mipango ya kumpasha tohara. (Momanyi: 14).

Mzee Masumbuko pia anawatengea wanawe majukumu ili kuwatayarisha kwa maisha ya utu uzima kulingana na utamaduni wa jamii yake. Kwa mfano, wasichana walifaa kupashwa tohara na kuolewa. Hivyo, hakutaka kuelezwa wala kuelekezwa na yeyote yule kuhusu malezi ya wanawe. Hakumsikiliza hata mkewe Bi. Amina. Shaban na Bi. Halima wanapomshauri kuhusu malezi ya Tumaini anawakemea na kuwaambia kuwa hawatamfundisha kuwalea watoto wake. Masumbuko anawaambia Shaban na mkewe Bi Halima:

> "Nisikilizeni, kisha mnisikilize kwa makini. Mimi ni mtu na hamsini zangu. Sijashindwa kuwalea wanangu. Tuma...Tuma hatakuwa msungo kama huyo binti yenu kwa kumficha huko kwenu"....haya nielelezeni mlilolijia lakini kama ni juu ya tohara ya Tumaini, hiyo ni lazima (Momanyi: 39).

Malezi ya Idi pia yanaathiriwa na utamaduni. Idi aliwadharau dada zake kwa kila jambo. Tabia hii alikuwa amesoma kwa babake aliyedharau wanawake. Idi hangewasaidia dada zake kufanya kazi za nyumbani kwa sababu aliamini kuwa kazi za nyumbani kama kuchochea moto mekoni au hata kuteka maji zilikuwa kazi za wanawake kulingana na desturi na mila za jamii yao. Itikadi hizi pia zilimtwaza mtoto wa kiume na kumtweza mtoto wa kike. Kwa mfano, Idi anaendelea na masomo yake hadi shule ya upili lakini dada zake Rehema na Mashaka wanaacha kusoma wakielekea darasa la saba na kuolewa

licha ya kuwa walikuwa na hamu ya kuendelea na masomo. Mwandishi anadhibitisha haya:

> Tumaini alielewa kwamba hii ndiyo maana alipokuwa akimwambia amsaidie kuchochea moto mekoni au hata kuteka maji, alimjibu kuwa ile ilikuwa kazi ya wanawake. Tumaini alihisi babake alikuwa akimpotosha Idi kwani ulimwengu wasasa umebadilika. Kizazi kipya sasa kimeanza kudadisi desturi na mila zilizokuwa zinatinga maendeleo hasa ya mtoto wa kike (Momanyi: 29).

Utamaduni ni asasi inayoathiri malezi ya watoto. Suala hili ni la uhalisia na linatukia katika mazingira halisi. Kama mihimili ya nadharia ya uhalisia inavyoeleza kuwa wahusika huwa wa kweli na lugha wanayotumia hueleweka kwa urahisi, wahusika katika riwaya teule ni wa kweli. Kwa mfano, utafiti wa UNICEF (2017) unaonyesha kuwa katika jamii ya Wamaasai ndoa za mapema zinachochewa na mila na desturi za jamii hiyo ambazo zinamdunisha mtoto wa kike ikilinganishwa na wa kiume. Kulingana na utamaduni huu, wasichana wanafaa kuozwa ili kuiletea jamii faida. Kisa hiki cha watoto wa kike wa Wamaasai kinalingana na kisa cha Tumaini katika riwaya ya *Tumaini* (2006) anayepangiwa kupashwa tohara na kuozwa. Dada zake Tumaini pia wanapaswa tohara na kuolewa kulingana na utamaduni wa jamii yao. Hivyo, suala la kitamaduni linalotukia katika riwaya teule ni la kiuhalisia.

### 3.2 Asasi ya Familia na Ndoa

Conlon, Ginn na Lounsbury (2015) wanaeleza kuwa familia ni muhimu kwa mtoto. Mazingira ya nyumbani hujenga tabia za mtoto akiwa mdogo na hata katika maisha ya baadaye. Anaeleza kuwa familia humwezesha mtoto kushirikiana na wanajamii, humwadhibu anapokosea na pia humfunza maadili. Familia humpa mtoto usaidizi wa kimwili na hata kiroho. Utafiti uliofanywa na Shabas (2016) unaonyesha kuwa mabadiliko ya kijamii yameathiri uhusiano uliokuwapo kati ya mtoto na wazazi wake.

Anaeleza kuwa siku hizi wazazi wengi hawana nafasi ya kuhusiana na watoto wao. Watoto huachiwa wafanya kazi ambao wakati mwingine hawawaongozi watoto inavyofaa na kuwapa mwelekeo wa maisha.

Familia ni muhimu katika malezi ya watoto. Jinsi wazazi wanavyohusiana huathiri jinsi mtoto anavyokua. Kuna wazazi ambao hupanga sheria watakazotumia kuwalea watoto wao kwa pamoja ilhali katika familia zingine kila mzazi hutumia sheria zake kuwalea watoto. Katika familia kama hizo, watoto huchanganyikiwa na kukosa ni sheria zipi wanafaa kufuata kwa kuwa baadhi ya sheria hupingana. Katika riwaya teule, familia ni mojawapo ya asasi zinazoathiri malezi ya watoto. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004), Bwana Mashaka na mkewe Bi. Nusura hawashirikiani katika malezi ya watoto wao. Bwana Mashaka anapuuza ushauri wa mkewe kila wakati. Kwa mfano, Mzee Mashaka anapompa Yasibu uhuru wa kufanya atakalo, Bi. Nusura hafurahishwi na jambo hili. Anamweleza mumewe kuwa si jambo la busara kumwachia mtoto afanye atakalo lakini Bwana Mashaka anampuuza. Bwana Mashaka anamweleza kuwa Yasibu hafai kufanya kazi yoyote nyumbani ila kudurusu vitabu. Bi. Nusura alionya:

> Basi huko ni kumdekeza mtoto. Huko ni kumfurisha mtoto kichwa. Utamharibu mtoto akiwa mdogo. Kumbuka udongo uwahi uli maji. "Haidhuru!" Bwana Mashaka alijibu. (Omari:25).

Bi. Nusura pia anamsihi mumewe awasamehe wanawe wanapokosea lakini Bwana Mashaka anakataa. Kwa mfano, Yasibu anapoacha shule kwa sababu ya ujauzito babake anakataa kumsamehe. Anakataa kumsaidia na kumsetiri. Bi. Nusura anamweleza mumewe kuwa ni vizuri kuwasamehe wanao kwa sababu hawatapata wazazi wengine na

binadamu hukosea. Bwana Mashaka anakataa kusikiliza ushauri wa mkewe na kusema kuwa watoto wake wamemkosea. Bi. Nusura anasema:

> "Una nini mume wangu? Wewe ni mkuu. Mbona huyachukui mambo kikuu? Faida ya uzee huo ni ipi basi ikiwa wakosa hekima na busara?...tuseme huna tena huruma na mtoto huyu kana kwamba siye wewe uliyemzaa ukamleta katika handaki hili la ulimwengu?...tangu mtoto huyu awe mjamzito hadi akajifungua hatujakuwa na raha naye. Ameniaibisha. Watoto hawa wameniasiri na kunivunja moyo kwa kususia elimu. (Omari: 97).

Dunia anapougua homa kali, Bi. Nusura anamsihi mumewe amsamehe na kumpeleka hospitali. Anasikitishwa na jinsi mumewe anavyomkemea Dunia katika hali hiyo. Haelewi kwa nini mumewe amekosa huruma kwa mwanawe. Mzee Mashaka anakataa kumpeleka Dunia hospitali na kusema kuwa anajifanya.

Bi. Nusura na Bwana Mashaka wanalaumiana watoto wao wanapokosa nidhamu. Bwana Mashaka anamlaumu mkewe watoto wao wanapoharibika. Anamwambia kuwa yeye ndiye amefanya watoto hao waache masomo. Bwana Mashaka anasema:

> "Watoto hawa hawangeharibika hivi thama na wewe...Ati nini" Mimi nimewaharibu watoto? Nifanye hivyo kwa kutarajia nini? Bibi Nusura alishangaa. Sijui. (Omari: 97).

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), asasi ya ndoa imechangia pakubwa mbinu za malezi wanazotumia wazazi. Ndoa ya Mzee Masumbuko na Bi. Amina ni mojawapo ya ndoa hizi. Mzee Masumbuko hakumhusisha mkewe katika malezi ya wanawe. Alifanya kile alichotaka na ushauri wa mkewe haukuwa na manufaa yoyote kwake. Bi. Amina hakutoa maoni yoyote kuhusu malezi ya watoto wake. Aliogopa adhabu ambayo angepewa iwapo angejaribu kupinga mipango ya Mzee Masumbuko. Bi. Amina anamweleza dadake Bi. Halima:

> Mimi binafsi nakubaliana na mawazo yako kabisa kuhusu tohara ya kike. Lakini nikiyatamka au kuonyesha waziwazi mbele ya Masumbuko nitakuwa ninaufyeka uwanja wa kuitayarisha talaka yangu (Momanyi: 33).

Shaban na mkewe Bi. Halima ni kielelezo cha ndoa iliyofaulu katika malezi. Wazazi hawa wanashirikiana katika kila jambo kumlea mwanao Riziki. Riziki alikuwa mmoja wa wasichana waliobahatika kupata elimu kwa sababu ya ushirikiano wa wazazi wake. Bi. Halima alikuwa mstari wa mbele kupinga tohara za kike. Aliweza kufanya hivi kwa sababu ya ushirikiano wake na mumewe. Kwa mfano, Tumaini anapotorokea kwao, Shabani na mkewe wanaenda kwa Mzee Masumbuko kumweleza kuwa tohara ya kike sio nzuri na halikuwa jambo la busara kumlazimisha Tumaini kupashwa tohara iwapo anataka kuendelea na masomo. Bi. Halima anamweleza Bi. Amina:

> Tutakuja huko nyumbani kwenu, mimi na Shaban. Tutamweleza Masumbuko dhahiri shahiri kusudio letu, na hatutaogopa kumkabili. Wakati wa magharibi, Shaban na mkewe waliwasili kwa Mzee Masumbuko kumweleza kuwa haikuwa vyema kumpasha tohara Tumaini (Momanyi: 34).

Zaidi ya hayo, Tumaini alipojiunga na familia ya Shaban na Bi. Amina, aliweza kusoma hadi chuo kikuu kwa sababu ya ushirikiano wao. Walezi hawa waliweza kufurahia matokeo yake na kumnunulia jozi ya viatu. Shaban pia alitenga muda mwingi kumsaidia na kumwelekeza Tumaini katika kazi zake za ziada kutoka shuleni. Mwandishi anasema:

> Shaban na mkewe waliyafurahia matokeo hayo ya Tumaini wakamzawadia jozi ya viatu. Zawadi hii ilimsisimua sana Tumaini ambaye kamwe hakuwa amenunuliwa zawadi hapo mbeleni kwa sababu ya kufaulu kwake shuleni...Shaban mara nyingi alichukua muda wake mwingi hususan nyakati za magharibi, kumsaidia na kumwelekeza Tumaini katika kazi zake za ziada (Momanyi:45).

Shaban na Bi. Halima pia wanamhakikishia Tumaini kuwa atasoma bila shida yoyote. Wakati Mzee Masumbuko anashirikiana na Chifu Andrea kuhakikisha kuwa Tumaini hatapata ufadhili, Bi. Halima anamweleza Tumaini kuwa asiwe na wasiwasi kwani

wamepanga mipango ya jinsi watakavyosoma na binamuye Riziki. Bi. Halima anamweleza Tumaini:

> Ma Mdogo, hivi mtanisomesha bila usaidizi wa baba na mama? Tumaini alimuuliza.Hayo yasikutie wasiwasi. Tulikwambia kwamba tutagharamia elimu yako, ama sivyo? Bi. Halima aliuliza. Wewe ufanye bidii tu masomoni kwani tayari tumepanga jinsi ya kukusomesha wewe na binamu yako Riziki (Momanyi: 67).

Wahusika waliotumiwa na wandishi wa riwaya teule ni wa kiuhalisia na lugha wanayotumia ni rahisi kama inavyoeleza nadharia ya uhalisia. Mambo wanayowasilisha ni ya kweli kama yalivyo katika mazingira halisi. Kwa mfano, utafiti uliofanywa na shirika la UNICEF (2016) unaonyesha kuwa wasichana wengi waliojihusisha na ukahaba katika eneo la Kibera kaunti ya Nairobi wanatoka katika familia ambazo hazina kina baba au wazazi wote hawapo ikilinganishwa na watoto waliolelewa na wazazi wote. Utafiti huu pia unaonyesha kuwa katika familia ambazo mlezi ni mmoja, mlezi huyu hutenga muda mwingi kuhakikisha kuwa watoto wamepata mahitaji ya kimsingi na kusahau kuwaelekeza na kuwaongoza watoto. Utafiti huu pia unaeleza kuwa katika familia ambazo wazazi wote wapo, mzazi mmoja huchukua jukumu la kuwaelekeza na kuwaongoza watoto iwapo yule mwingine hayupo. Haya ni sawia na jinsi Shaban na Mkewe Bi. Halima katika riwaya ya *Tumaini* (2006) walivyoshirikiana kuwalea wanao Tumaini na Riziki tofauti na ilivyokuwa katika familia ya Mzee Masumbuko na Bi. Amina ambao hawakushirikiana katika malezi ya watoto wao.

### 3.3 Asasi ya Elimu

Downey (2015) anaeleza kuwa walezi walioelimika hutumia mbinu tofauti na wale ambao hawana elimu. Anasema kuwa wazazi hawa huwaelewa watoto, huhusika katika maendeleo ya mtoto na huwatia moyo wanapofanya jambo fulani. Wengi wa watoto

ambao wazazi wao wameelimika huweza kufanya vyema shuleni na hufanikiwa maishani.

Asasi ya elimu ni mojawapo ya asasi ambazo zimeathiri mbinu wanazotumia wazazi kuwalea watoto wao katika riwaya teule. Wahusika mbalimbali wameonyesha jinsi elimu inavyoathiri malezi ya watoto katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004). Wahusika hawa ni kama Bwana Mashaka na Mwalimu Busara. Bwana Mashaka alidhamini elimu sana. Kwake, mtoto hangekuwa mtoto wake bila elimu. Kwa mfano, anamweleza mkewe kuwa mwanao Yasibu hafai kufanya kazi yoyote nyumbani ila tu kudurusu vitabu. Kazi zote zinafaa kufanywa na watumishi. Jambo hili halimfurahishi Bi. Nusura kwa sababu anaona kuwa mumewe anamdekeza Yasibu. Anafuatilia maendeleo ya Yasibu shuleni na hafurahii matokeo yake yanapozorota. Hivyo, anamshauri kuhusu umuhimu wa elimu. Bwana Mashaka anasema:

> Kata jongoo kwa meno upate elimu. Elimu ni mali mwanangu. Baada ya mimi kuelewa faida ya elimu, siwezi kumvumilia mtoto anayeikataa elimu (Omari: 31).

Bwana Mashaka anakatiza uhusiano wake na wanawe baada ya kususia masomo. Dunia anapokosa kuhudhuria masomo kwa miezi kadhaa babake anakataa kuzungumza naye. Anabadilisha mbinu ya kuwalea watoto wake na kuwa na chuki kwao. Dunia anapoamua kubadilika na kurudi shule babake anakataa kumlipia karo za shule. Hamshughulikii kwa vyovyote. Bwana Mashaka anamweleza Mzee Mafusho:

> Eeh! Mzee Mafusho, mtoto huyu alisusia kusoma bila sababu yoyote ya dhahiri.Huo ndio ugomvi wangu halisi wa mimi naye, hata simshughulikii kwa jambo lolote.Akirejea nyumbani ni sawa na asiporejea ni sawa. (Omari: 68)

Haikuwa tofauti kwa Yasibu, Yasibu ambaye alidekezwa na babake alikosa amani nyumbani kwao baada ya kupata ujauzito na kuacha masomo. Babake ambaye

alimdekeza anabadilika na kukosa kumsetiri. Yasibu anahuzunishwa sana na jinsi babake alivyobadilika. Hakuelewa kwa nini babake aliacha kumsaidia na kumsetiri. Anashangaa kwa nini babake hangemvumilia muda alipoteleza na kumwonyesha njia bora ya kufuata. Mwandishi anadhibitisha:

> Mzee huyu hakuwa na uhusiano mzuri na mwanawe Yasibu. Alimkasirikia Yasibu kwa kuacha masomo wakati alikuwa akielekea darasa la saba (Omari:81).

Mwalimu Busara pia ni kielelezo cha wahusika wanaodhamini elimu katika riwaya hii. Yeye Ndiye Mwalimu mkuu wa shule ya msingi ya Jitihada ambapo Dunia alisomea. Mwalimu huyu anachukua muda mwingi kuwashauri wanafunzi. Hakufurahishwa na mwanafunzi yeyote ambaye aliwakosea heshima wazazi na walimu wake. Aliwafananisha wanafunzi na sumba na kukariri kuwa walihitaji kuongozwa siku zote. Dunia anapoamua kurudi shule, Mwalimu Busara anamsihi Bwana Mashaka amsamehe Dunia na kumlipia karo za shule. Bwana Mashaka anapokataa kulipa karo za mtoto wake, mwalimu huyu anamhurumia Dunia na kukubali aendelee na masomo. Mwandishi anaeleza:

> Pale Bwana Mashaka alipokoma kulipa karo za mtoto wake, Mwalimu mkuu, Bwana Busara alimwita akamdadisi kuhusu jambo hilo. Aliyoyajibu Bwana Mashaka hayakumridhisha Bwana Busara. Sababu za ati hakuwa na pesa na kuchezea kwa mtoto laghai zilimkirihi mwalimu mkuu... mwalimu mkuu alihiari Dunia aendelee na masomo si kwa ajili ya huruma kwa Bwana Mashaka bali kwa kumsikitikia Dunia mwenyewe. Aliona ni soni kuacha kumpa mtoto elimu kwa sababu ya uyabisi wa roho wa babake (Omari: 81).

Shaban na Bi. Halima ni walezi walioelewa umuhimu wa elimu katika riwaya ya *Tumaini* (2006). Ingawa hawakufika mbali kwa masomo walijitahidi kumsomesha mwanao Riziki. Riziki alikuwa mmoja wa wasichana waliobahatika kupata elimu katika kijiji chao. Jambo hili linamtia moyo Tumaini na anapogundua kuwa babake amepanga kumpasha tohara na kumwoza anaenda kwa walezi hawa kwa sababu alijua kuwa watamwelewa na

kumsaidia. Shaban pia alipenda kupitisha muda mwingi akimsomea Riziki mashairi na hadithi za kale. Kupitia kwa hadithi na mashairi hayo, Riziki alijifunza mengi sana akawa mweledi katika masomo. Mwandishi anadhibitisha:

> Riziki alikuwa mmoja wa wale waliobahatika. Hii ni kwa sababu wazazi wake waliuona umuhimu wa kumwelimisha mtoto wa kike. Shaban na mkewe Halima walikuwa katika mstari wa mbele kupinga ndoa hizo za lazima. Waliamua kumsomesha binti yao Riziki kwa kadri ya uwezo wao na wakaipinga vikali dhamira ya mzee Masumbuko kumpasha bintiye tohara kisha kumwachisha shule ili aolewe. (Momanyi: 15).

Yusuf, mjomba wake Tumaini alielewa umuhimu wa elimu na kuidhamini. Anashirikiana na Shaban na mkewe kuhakikisha kuwa Tumaini ameendelea na masomo yake. Anamkashifu Mzee Masumbuko na kumwambia kuwa anataka kukatiza masomo ya Tumaini ili apate mahari. Pia, anapinga njama ya Mzee Masumbuko kumpasha tohara Tumaini kisha kumwoza. Kwa mfano, Mzee Masumbuko anapowaleta wageni ili aweze kumposa Tumaini, Yusuf anakasirika sana kwa sababu Tumaini alikuwa anaendelea na masomo. Mwandishi anadhibitisha:

> "Nani!"Yusuf aliruka na kusimama wima, mikono kiunoni. Aligeukia Mzee Masumbuko na kuuliza, Yaani Masumbuko umewaleta wageni hawa kutoka huko-sijui wapi- Mambrui kumposa mtoto wetu mchanga anayesoma shule? Hii ni aibu gani? (Momanyi: 61-62).

Mchango wa elimu katika malezi ya watoto ni suala la kweli na linapatikana katika mazingira halisi. Hivyo basi, maoni ya waandishi katika riwaya teule ni ya kiuhalisia. Utafiti uliofanya na Muyalo (2015) katika kaunti ya Meru, eneo bunge la Igembe North unadhihirisha kuwa suala hili ni la kiuhalisia. Utafiti huu unaonyesha kuwa, asilimia tisini na nne ya wazazi waliojihusisha na maendeleo ya watoto wao shuleni ni wale walioelimika. Utafiti huu pia, unaonyesha kuwa wengi wa watoto ambao wazazi wao hawajaelimika hawafanyi vyema katika masomo yao. Hii inatokana na kuwa wazazi wao hawajishughulishi na maendeleo yao shuleni. Kinoti (2017) anaeleza kuwa elimu ni

mojawapo ya asasi zinazoweza kuzuia ndoa za mapema kwa mtoto wa kike. Anatoa mfano wa utafiti uliofanywa na shirika la afya ambao ulionyesha kuwa asili mia sitini na saba ya wasichana wasio na elimu huolewa kabla ya kufika miaka kumi na nane ikilinganishwa na wasichana walio na elimu ambao wanatumia muda mwingi kwa masomo yao. Hivyo, hawaolewi mapema. Anaeleza kuwa serikali inafaa kutekeleza sheria zote zinazomlinda mtoto wa kike. Wazazi na jamii wanafaa kuelimishwa kuhusu athari za kuwaoza watoto mapema na umuhimu wa kumwelimisha mtoto wa kike.

### 3.4 Hali ya Jinsia na Uana

Kwa Mujibu wa Onyango na Muchiri (2016) jinsia inahusu wajibu na majukumu waliyopewa wavulana na wasichana na jamii. Watoto hawazaliwi na majukumu haya bali wanapewa majukumu haya na jamii. Kwa mfano, ni jukumu la mwanamke kuandaa chakula na kutunza nyumba ilhali wanaume huenda kutafutia familia zao. Kwa upande mwingine, wanaeleza kuwa uana ni sifa za kibiolojia zinazowafanya watu watambulike kama wanawake na wanaume. Uana ni mambo ya kimaumbile ambayo hayawezi kubadilika.

Kulingana na Mc Kinney na Renk (2008), katika familia nyingi, wazazi hutofautiana katika mbinu wanazotumia kuwalea watoto wao. Tofauti hizi hutokana na maumbile yao ya kuwa mke au mume na majukumu ambayo wametengewa na jamii. Anaeleza kuwa jamii inatarajia mwanamke achunge familia yake na mwanamume anafaa kuhakikisha kuwa familia yake ina mahitaji ya kimsingi na watoto wana nidhamu bora.

Craig (2006) anaeleza kuwa wanawake huwa na uhusiano mkubwa na watoto wao kuliko wanaume. Kulingana na utafiti huu, wanawake huonyesha huruma kwa watoto wao hata wakikosea ikilinganishwa na wanaume. Kulingana na Barton na Kirtley (2012),

mbinu wanazotumia kina mama kuwalea watoto wao huwa muhimu sana na huwa na athari kubwa mtoto anapokua ikilinganishwa na mbinu wanazotumia kina baba. Anaeleza kuwa kina baba na kina mama huwa na majukumu tofauti katika malezi hivyo hutekeleza mbinu hizi kwa njia tofauti. Riwaya za *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006), zinaonyesha jinsi jinsia na uana wa wahusika unavyoathiri malezi ya watoto. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004), Bi. Nusura hahusishwi katika malezi ya wanawe. Mzee Mashaka anapuuza ushauri wowote anaompa kuhusu malezi ya watoto wake kwa kuwa ni mwanamke. Bi. Nusura anamshauri Bwana Mashaka:

> Basi huku ni kumdekeza mtoto. Huko ni kumfurisha mtoto kichwa. Utamharibu mtoto akiwa mdogo. Kumbuka, udongo uwahi uli maji. Samaki mkunje angali mbichi, Bibi Nusura alionya. Haidhuru! Bwana Mashaka alijibu. Bi. Nusura alikithiri kumkumbusha mumewe huku machozi ya kimchangama kwa kupingwa mashauri hayo yenye mafunzo. (Omari: 25).

Bi. Nusura anaonyesha huruma kwa wanawe. Bwana Mashaka anapokataa kuwasaidia wanawe baada ya kuacha shule, Bi. Nusura anamsihi mumewe awasamehe Dunia na dadake Yasibu kwani wametubu lakini Bwana Mashaka anakataa. Anasema kuwa sio vizuri kuwalaumu wanao kwa kila jambo. Anapogundua kuwa mumewe hawajali wanawe tena anaamua kuwatetea. Bi Nusura pia anamhurumia Dunia sana na kumshughulikia anapokuwa mgonjwa. Anamlaumu mumewe kwa kuwa mkali kwa wanao. Bi. Nusura anasema:

> "Una nini mume wangu? Aa! Mbona umekuwa mkali kama chui! Haifai hivyo! Hivyo huoni Dunia ni muwele? Kwani muwele hutoka nje? Mlaani ibilisi. (Omari: 37).

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006) malezi ya Idi ni tofauti na ya Tumaini na dada zake. Idi hakufanya kazi nyingi nyumbani. Alipoambiwa na Tumaini amsaidie kufanya kazi

nyumbani alikataa na kumwambia kuwa yeye ni mtoto wa kiume. Mawazo haya ya Idi yalitokana na malezi aliyopata kwa babake. Babake alimlea kwa ukatili na ujeuri mwingi. Alimfunza kuwa jukumu la mwanamke ni kuolewa tu. Tumaini anamruhumia kakake kwa kuhofia iwapo ataweza kukabiliana na dunia inayobadilika. Mwandishi anadhibitisha haya:

> Tumaini alimwangalia kakake kwa muda huku akitikisa kichwa kwa masikitiko. Alielewa malezi ya Idi ni kielelezo halisi cha malezi ya babake. Kijana huyo mdogo tayari alijua kuwa wanawake ni vifaa tu vya utumishi nyumbani mwao...Tumaini alielewa kuwa hii ndiyo maana alipomwambia amsaidie kuchochea moto au hata kuteka maji, alimjibu kuwa ile ilikuwa kazi yawanawake. (Momanyi: 29).

Mzee Masumbuko hakutaka kuelekezwa na mtu yeyote kuhusu malezi ya Idi. Alipowakosea dada zake mzee huyu alimtetea na kusema kuwa ni mtoto wa kiume. Jambo hili lilimfanya Idi kuwa mkaidi na kuwadharau dada zake kila wakati ingawa alikuwa mdogo wao. Aliwaona dada zake tu kama watumishi pale nyumbani. Mara nyingi aliwaelekeza dada zake kauli kali kali kama vile kuwaambia wao ni kama bidhaa za uwekezaji pale nyumbani na walisubiri tu kuolewa ili wazazi wapate pesa za kumsomesha. Kauli hizi za Idi hazikumfurahisha Tumaini lakini alipomwambia babake kuhusu Idi alimkemea na kusema kuwa Idi ni mtoto wa kiume. Mwandishi anadhibitisha:

> Kauli za Idi zilimkera Tumaini kwa muda mrefu. Kila mara alimkabili na kumkumbusha babake kuwa lugha aliyotumia dhidi yao ilikuwa inamwathiri vibaya kaka yao mdogo. Babake alimkemea na kumkanya kutoingilia malezi ya Idi kwani yeye ni mtoto wa kiume, si wa kike. Aidha, alihitajika kuwa na moyo mgumu kama yeye ili kuyakabili maisha baadaye. (Momanyi:14).

Mzee Masumbuko hakuona faida ya kuwasomesha wasichana wake. Kwake mtoto msichana alifaa kuolewa ili apate mahari. Kwa mfano, dada zake Tumaini, Rehema na Mashaka wanapashwa tohara na kuolewa baada ya kumaliza darasa la saba. Ingawa Mashaka alikuwa na hamu ya kuendelea na masomo yake, babake hakumpa nafasi ya

kuendelea. Idi anaendelea na masomo yake bila pingamizi yoyote kwa kuwa ni mtoto wa kiume. Mwandishi anadhibitisha haya:

> Baada ya kufaulu mtihani wa darasa la nane, Idi alijiunga na shule ya upili ya Darajani, shule iliyokuwa mumo humo kijijini Mabujuni. (Momanyi: 114)

Watoto wa kiume waliweza kusoma bila matatizo yoyote. Walipofaulu mtihani, wazazi wao waliweza kufurahia matokeo yao na kuwanunulia zawadi. Wazazi pia waliwahimiza kusoma zaidi. Kwa mfano, Sifa na Yohana ambao walikuwa darasa moja na Tumaini waliweza kusoma bila kukumbwa na matatizo yoyote. Tumaini anakumbuka jinsi Sifa alivyonunuliwa baiskeli na babake Mzee Majaliwa, kwa sababu ya juhudi zake masomoni. Anajisitikia kwa sababu licha ya kufaulu vyema katika masomo, babake hakuwahi mnunulia zawadi yoyote. Anaanza kujiuliza kwa nini kazaliwa msichana. Mwandishi anaeleza:

> Alianza kuwasuhudia akina Sifa na Yohana ambao hawakuwahi kukumbwa na matatizo kama yake. Walikuwa hodari katika masomo na kila mara wazazi wao waliwahimiza kusoma zaidi. Alikumbuka jinsi Sifa alivyonunuliwa baiskeli na babake, Mzee Majaliwa kwa sababu ya juhudi zake masomoni. Alianza kujisikitikia alipofikiri kuwa licha ya yeye kufaulu vyema katika masomo, alikumpitikia wazo hata siku moja Mzee Masumbuko kumtunukia bintiye zawadi yoyote. Tumaini alianza kujiuliza kwa nini kazaliwa msichana (Momanyi: 22).

Mzee masumbuko anakataa kuhudhuria sherehe ya Tumaini baada ya kufuzu mtihani wa kidato cha nne. Anaposhawishiwa na mkewe anamweleza kuwa kwake elimu haina maana yoyote kwa mtoto wa kike. Anajawa na chuki kwa sababu Tumaini alikaidi amri zake kwa kukataa kupashwa tohara na kuolewa na mume aliyemtafutia. Mzee Masumbuko anasema:

> "Tuma alinikana siku ile aliyonyanyua mguu na kuhama hapa. Kwa hivyo, yeye si mwanangu, unaskia?" Aende asiende kwangu fahuwa. Mtoto wa kike kama yeye hawezi kuwa fahari kwangu ati kwa sababu amesoma. Fahari kwangu ni kumwoza tu nipate mahari yangu kwa sababu elimu yake haitanisaidia chochote (Momanyi:151-152).

Mzee Masumbuko ameonyeshwa kuwa mkali na mgumu katika malezi ya wanawe. Ukali wake unaonyeshwa Tumaini anapoamua kutorokea kwa Bi. Halima. Anatoroka usiku ndipo babake asimuone. Anaogopa adhabu ambayo angepata iwapo babake angegundua kuwa anatoroka ili asipashwe tohara. Mzee Masumbuko hakuwa na huruma kwa watoto wake. Alipoamua kuwaadhibu alimchapa anayeadhibiwa mpaka fimbo inavunjika. Mwandishi anaeleza:

> Tumaini aliufungua mlango taratibu ili asiwaamshe waliolala. Alijizuia hata kupumua akidhani kuwa pumzi zake zingemwamsha baba yake Mzee Masumbuko, ambaye bila kusita angemwadhibu vibaya (Momanyi: 1).

Suala la watoto wa kike kupewa malezi tofauti na wavulana ni la kiuhalisia. Utafiti wa UNICEF (2017) unaonyesha kuwa katika jamii nyingi za Kiafrika, wasichana wanadunishwa. Wavulana hupewa elimu na watoto wa kike huachwa katika familia moja. Jamii inaamini kuwa jukumu la msichana ni kuolewa ili alete faida kwa jamii. Jambo hili la watoto wa kike kudunishwa linalingana na kisa cha Idi katika riwaya ya *Tumaini* (2006) ambaye aliweza kusoma hadi shule ya upili na dadake zake kukosa kuendelea na masomo.

### 3.5 Hali ya Hadhi/ Cheo

Kulingana na Brown (2009), hadhi ni hali katika jamii ambapo watu hutofautiana kulingana na hali yao ya kiuchumi. Tofauti hizi huchochewa na cheo alicho nacho mtu, wadhifa wao katika jamii, kazi anayofanya, na pia mali aliyonayo. Tofauti hizi huweza kuleta migawanyiko katika jamii hivi kwamba kuna wale walio na hadhi ya juu na wale wa hadhi ya chini. Watu wenye hadhi ya juu huheshimika katika jamii kuliko wale wa hadhi ya chini.

Miller (2015) anaeleza kuwa wazazi hutofautiana kwa mbinu wanazotumia kuwalea watoto kwa mujibu wa hadhi au vyeo vyao. Anaeleza kuwa tofauti hizi zinatokana na utabaka, hadhi ya wazazi na vyeo vyao katika jamii. Anaeleza kuwa wazazi walio na hadhi ya juu katika jamii huwatunza na kuwasaidia watoto wao. Wengi wa wazazi hawa huwadekeza watoto wao kwa sababu kazi nyingi hufanywa na watumishi wa nyumbani. Miller (keshatajwa) anaeleza kuwa wazazi huwa na matarajio tofauti kwa watoto wao. Kwa mfano, wazazi walio na hadhi ya juu huwa na matarajio makubwa kwa watoto wao na hufanya juu chini kuhakikisha kuwa watoto wao wamefanikiwa maishani. Hii ni tofauti na wazazi walio na hadhi ya chini na maskini ambao hawatengi muda mwingi kuwashauri na kuwaelekeza watoto wao ila huchukua muda mwingi kuhakikisha watoto wamepata mahitaji ya kimsingi.

Hadhi ya mwanadamu ni muhimu sana katika maisha yake na huathiri mbinu anazotumia kuwalea watoto wake. Waandishi wa riwaya teule za *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006) wameonyesha jinsi wahusika wanavyodhamini hadhi zao katika jamii. Wanaweza kufanya lolote ili hadhi yao idumu. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) Bwana Mashaka anabadilisha njia za kuwalea watoto wake baada ya watoto hawa kukosa nidhamu. Kwa mfano, Yasibu anapopata mimba, ule uhuru aliokuwa amepewa na babake unakatizwa. Mwandishi anaeleza kuwa Mzee Mashaka hakumruhusu Yasibu atoke nyumbani. Alikaa nyumbani usiku na mchana. Mwandishi anaeleza:

> Basi Yasibu alilazimishwa kutawa. Wazazi wake walishikana wakawa itifaki moja, wakazisahau tofauti zao za kifikira, Yasibu asiweze kukaidi amri. Alivumbikwa nyumbani usiku na mchana kama ndizi zivumbikwazo ili ziive.Alipowalalamikia wazazi wake hakuna aliyemsikiliza hata kidogo (Omar: 78).

Mzee Mashaka pia aliajiri mkunga kwa siri ili amhudumie mwanawe nyumbani kwa kuhofia majirani. Aliogopa aibu kwa sababu alikuwa mzee mwenye heshima katika jamii yao. Isitoshe, Mzee Mashaka anakataa kuwasamehe watoto wake kwa sababu ya kususia elimu. Anasema kuwa wamemletea aibu katika familia yake. Bwana Mashaka anasema:

> "Ameniaibisha. Watoto hawa wameniaziri na kunivunja moyo kwa kususia elimu. Sasa Yasibu amekuwa mlezi badala ya mwanafunzi. Dunia naye hajiwezi kwakushiriki upuuzi (Omar: 97).

Yasibu anapoamua kutoroka nyumbani kwa sababu ya shida alizopitia mikononi mwa babake, mamake anamsihi arudi nyumbani. Anamweleza kuwa baba yao anawependa sana ila tu ni mshindani. Hataki kuonekana kushindwa wala kufuata mawazo ya mtu mwingine. Bi. Nusura anamwambia Yasibu:

> "Aa! Mwanangu mlaani ibilisi! Rudi nyumbani tafadhali. Baba yenu anawapenda nyinyi wanawe. Ila ya baba yenu ni kuwa ni mshindani. Hataki kuonekana kushindwa au kufuata mawazo ya mtu mwingine. Msishindane naye (Omar: 105).

Mwalimu Busara alitumia cheo chake kama mwalimu mkuu kuwashauri wanafunzi wa shule ya Jitihada. Wanafunzi walipokosea aliwapa adhabu kali hivyo walimuogopa sana. Anamhimiza Dunia kutia bidii katika masomo yake licha ya kuwa babake alikoma kumlipia karo za shule. Mwalimu huyu anaona ni jukumu lake kuhakikisha kuwa Dunia amepata elimu kwa sababu sio vizuri kuadhibu mtoto kwa sababu ya babake. Aliweza kufanya hivyo kwa sababu ya cheo chake. Mwandishi anadhibitisha:

> Dunia aliendelea na masomo si kwa ajili ya huruma kwa Bwana Mashaka bali kwa kumsikitikia Dunia mwenyewe. Aliona ni soni kuacha kumpa mtoto elimu kwa sababu ya uyabisi wa roho wa babake (Omar: 81).

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), Mzee Masumbuko anawalea wanawe kwa ukatili na ujeuri. Anafanya hivyo kwa kuzingatia utamaduni ambao umepitwa na wakati. Hakutaka kuwa mmoja wa wazee waliokiuka utamaduni katika jamii yake. Hangefanya chochote kuhakikisha kuwa binti zake wamepashwa tohara na kuolewa. Bi. Amina anamweleza Bi. Halima:

> "Halima,"Bi. Amina alianza kwa sauti ya chini, Masumbuko alinidokezea kwamba ikiwa Tuma hatakubali kutahiriwa, basi atafanya juu chini amuoze ili ajiepushie lawama na aibu katika ukoo wake. Alisema kuwa katika ukoo wake, hakuna msichana aliyeepuka tohara. Hakutaka binti yake awe wa kwanza kukataa (Momanyi: 32).

Majuto alikuwa mtundu shuleni. Aliwasumbua wanafunzi wengine shuleni pamoja na walimu. Kando na hayo, alipewa fursa ya kuendelea na masomo. Babake Chifu Andrea, alimtetea kila alipokosea. Chifu Andrea alitumia cheo chake na akakubaliwa fursa nyingine. Kwa mfano, Siku moja Majuto alishirikiana na wenziwe na kuvunja afisi ya mwalimu mkuu na kuiba madaftari ambayo waliuza. Wanafunzi hawa hawakufukuzwa shuleni kwa sababu ya hadhi na cheo cha chifu. Mwandishi anaeleza:

> Mara kadha Majuto alifukuzwa shule kwa sababu ya utovu wa nidhamu lakini Bwana Andrea alimtetea mwanawe huku akitumia cheo chake (Momanyi: 20).

Chifu Andrea anatumia cheo chake kumdekeza mwanawe Majuto. Kila alipokosea babake alimtetea. Hakuchukua jukumu lake kama mzazi kumrekebisha. Majuto alikuwa hasidi katika mtaa wa Miembeni. Alikuwa farisi katika wizi na ubakaji wa mabinti za watu. Wazazi wa mabinti hao walipomletea mashtaka kuhusu unyanyasaji wa majuto, aliwapuuza na kumtetea mwanawe. Wazazi wengine walipeleka mashtaka mahakamani lakini chifu aliyazima kwa kutoa hongo kwa mawakili na hata mahakimu ili watupilie mbali kesi hizo. Mwandishi anaeleza:

> Ingawa Chifu Andrea alifahamishwa juu ya wizi wa mwanawe, alijitia hamnazo. Maji yalipozidi unga, alihiari kuwahonga walalamishi ilmradi wasimtie Majuto kifungoni (Momanyi: 71).

Suala la hadhi na cheo kuathiri malezi ya watoto ni la kiuhalisia. Ochieng' (2019), katika gazeti la *Daily Nation* anaeleza kuwa wazazi walio na hadhi kubwa katika jamii huwafanyia watoto kila kitu na hawawaruhusu watoto kujitegemea. Anaeleza kuwa watoto hawa hawapewi nafasi ya kujifanyia kazi na jambo hili huwadhuru baadaye. Mzee Mashaka katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) anamdekeza mwanawe Yasibu hataki afanye kazi yoyote ila kudurusu vitabu. Jambo hili linamwathiri Yasibu baadaye.

### 3.6 Hali ya Ubinafsi na Tamaa ya Wahusika.

Kamusi ya TUKI (2013) inaeleza ubinafsi kama hali ya mtu kujifikiria na kujipenda yeye mwenyewe. Tamaa nayo imeelezwa kama hamu kubwa ya kupata kitu. Preston (2016), anaeleza kuwa wazazi wenye ubinafsi hawawapi watoto nafasi ya kujiamulia chochote katika maisha. Anaeleza kuwa wazazi hawa huwaona watoto kuwa dhaifu na hawahitaji kujiamulia chochote. Nia ya kuwaamulia watoto kila kitu ni kuwa wao huwa na matarajio makubwa kwa watoto wao.

Mbinu za malezi katika riwaya teule zinaongozwa na tamaa na ubinafsi wa wahusika. Katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2006), Bwana Mashaka anaongozwa na ubinafsi. Anashangaa iwapo kuna mtu yeyote anayefaa kumwongoza katika malezi ya watoto wake. Aliona kuwa ni yeye tu aliye na jukumu la kuwaongoza wanawe. Anapomdekeza Yasibu, Bi. Nusura anamuonya lakini anakataa kusikiliza ushauri wake. Isitoshe, watoto wanapokosa nidhamu anaanza kumlaumu mkewe. Anaona kwamba yeye hawezi kukosea kwa lolote. Bwana Mashaka anakataa kuwasamehe wanawe kwa

sababu ya ubinafsi. Baada ya wanawe kususia masomo, anakataa kuwaongoza na kuwasaidia. Hakuwafaa kwa chochote. Dunia anasoma kwa ufadhili wa Mwalimu Busara na kupata chakula kwa marafiki. Mwandishi anadhibitisha:

> Mwalimu mkuu, Bwana Busara alimwita akamdadisi kuhusu jambo hilo. Aliyoyajibu Bwana Mashaka hayakumridhisha Bwana Busara. Sababu za ati hakuwa na pesa za kuchezea kwa mtoto laghai (Omari: 81).

Mzee Masumbuko anaongozwa na tamaa na ubinafsi katika riwaya ya *Tumaini* (2006). Anawapasha tohara na kuwaoza binti zake ili apate mahari. Hajali maisha ya wanawe. Anakatisha elimu ya wasichana wake wakiwa wachanga. Kwa mfano, Mashaka alitaka kuendelea na masomo yake lakini babake hakumpa nafasi hiyo. Anapokea mahari ya Mashaka na kumwoza kwa lazima kwa Mzee Lusimbo kama mke wa tatu. Ndoa hiyo inamsababishia madhara makubwa ya kimwili na kiakili. Mzee Masumbuko hakujali afya ya binti yake kwa sababu ya tamaa ya pesa.

Mzee Masumbuko anataka kumwoza Tumaini ili apate mahari. Bi. Halima anaeleza kuwa kusudio la Mzee Masumbuko ni kumwoza Tumaini kwani alikuwa mroho wa pesa na alijua kiasi cha mahari ambayo angepata. Mzee Masumbuko pia anaeleza mkewe kuwa hana fahari na mtoto wa kike kwa sababu amesoma. Fahari yake ni amuoze apate mahari. Hivyo, malezi yake kwa watoto wake yanaongozwa na faida atakayopata kwa watoto hao bali sio mapenzi ya mzazi kwa wanawe. Mzee Masumbuko anasema:

> ...Fahari kwangu ni kumwoza tu nipate mahari yangu kwa sababu elimu yake haitanisaidia chochote (Momanyi: 152).

Ubinafsi wa wazazi unadhihirika hata katika ulimwengu halisi. Wako (2017) anaeleza kisa cha msichana mmoja wa miaka kumi na minne katika kaunti ya Narok aliyekatiza masomo yake na kuolewa. Babake anamuoza kwa sababu ya tamaa ya kupata mahari. Babake anapokea ng'ombe ishirini na sita na mbuzi kumi na kumuoza kwa mzee wa

miaka hamsini. Ubinafsi wa mzee huyu unalingana na ubinafsi wa Mzee Masumbuko katika riwaya ya *Tumaini* (2006) ambaye anakatiza masomo ya wanawe Rehema na Mashaka na kuwaoza wakiwa wachanga kwa sababu ya tamaa ya pesa. Pia, tamaa ya elimu inamfanya Bwana Mashaka kuwapuuza wanawe kwa sababu ya kuacha masomo. Hivyo basi, suala hili ni la kiuhalisia na wahusika waliotumiwa na waandishi ni wa kweli kama unavyoeleza mhimili wa nadharia ya uhalisia.

### 3.7 Hali ya Taasubi ya Kiume

Kulingana na Eagleton (1986) taasubi ya kiume ni mtazamo unaomyanyua mwanamume kwa kila jambo huku ukimtweza mwanamke. Katika mtazamo huu, mwanamume huwa kiongozi kwa kila jambo huku kazi ya mwanamke ni kufuata mwelekezo wa mwanamume na kufanya kazi ndogo ndogo nyumbani.

Bancroft na Silverman (2016) wanaeleza kuwa kuna familia ambazo kina baba hutawala. Wanasema kuwa katika familia hizi, maoni ya mama hayana umuhimu wowote. Wanaendelea kusema kuwa katika familia kama hizi, watoto huangamia kwa kukosa malezi mema. Wanasema kuwa wengi wa kina baba ambao huwadunisha kina mama katika malezi hutumia mbinu ya kimabavu. Wengine pia hukosa kuchangia kwa vyovyote vile katika malezi ya watoto na kuwalaumu wake wao watoto wanapokuwa na utovu wa nidhamu.

Katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2006), Bwana Mashaka anapinga ushauri wa mkewe Bi. Nusura. Anadunisha mawazo ya mkewe hata kama ni mazuri. Kwa mfano, Bi. Nusura anapomkosoa kwa sababu ya kumdekeza Yasibu, anamweleza kwamba hayo ndiyo malezi yanayofaa. Bwana Mashaka anamwambia mkewe kwamba mawazo yake hayana faida yoyote kwa wanao ila tu ni ya kubomoa. Baada ya Bi. Nusura kumwambia

awasamehe wanawe kwa sababu binadamu hukosea, anamkemea na kumwambia kuwa maneno yake ndiyo yanawadekeza watoto. Bwana Mashaka anamwambia Bi. Nusura:

> "Mara nyingine wanichosha na maneno yako haya ambayo hayana dalili ya kujenga isipokuwa kubomoa. (Omari: 98-99).

Mzee Masumbuko katika riwaya ya *Tumaini* (2006), anadunisha mawazo ya mkewe Bi. Amina. Watoto wake wanapoadhibiwa na Mzee Masumbuko, yeye husimama mbali na hadhubutu kusema lolote. Tumaini anamweleza Riziki kwamba lazima mamake yumo mbioni akimtafuta kwa sababu ya vitisho vya babake. Bi. Amina anaelewa kuwa kumpasha tohara Tumaini halikuwa jambo nzuri lakini hangeweza kupinga mawazo ya mumewe. Tumaini anasema:

> ...ametiwa ububu na baba kiasi cha kwamba hawezi kukanusha lolote baba alilonuia kutenda. Hana sauti.Yuko tu pale kuitikia kwa unyenyekevu amri kali kali kutoka kwa baba. (Momanyi: 30).

Mzee Masumbuko pia anadunisha ushauri wa mkewe. Tumaini anapofaulu mtihani wa kidato cha nne, Shaban na Mkewe Bi. Halima wanamwandalia sherehe. Bi. Amina anapomshawishi mumewe ahudhurie sherehe hiyo, Mzee Masumbuko anakataa. Bi. Amina anapojaribu kumwonyesha kwamba Tumaini ni mtoto wao na wanafaa kufurahia matokeo yake, Mzee Masumbuko anamkemea na kumwambia kuwa akiendelea kumpa nasaha hizo hata hiyo sherehe hatahudhuria. Mzee Masumbuko anatamka:

> Nasaha zako hizo ni bure kwangu kwani haziwezi hata kumshawishi paka. Na ukiendelea kunikera, nitahakikisha kwamba hata hiyo karamu ya mwanao hutaenda. (Momanyi: 152)

### 3.8 Hali ya Kiuchumi

Francese (2018) anaeleza kuwa uwezo wa kiuchumi wa wazazi huathiri mbinu watakazotumia kuwalea watoto wao. Anasema kuwa wazazi ambao wana kipato cha juu hutumia mbinu tofauti ikilinganishwa na wazazi maskini. Anaeleza kuwa wengi wa

wazazi tajiri hutunga sheria kali ambazo zinafaa kufuatwa na watoto. Hii inatokana na kuwa wana uwezo wa kutekeleza sheria hizo. Isitoshe, wazazi hawa pia hutumia mbinu ya kudekeza na watoto hupewa elimu bora zaidi. Kwa upande mwingine, watoto ambao wazazi wao ni maskini, hukosa elimu ama hupata elimu duni. Wazazi maskini pia hawana muda wa kukaa na kuwaongoza watoto. Muda mwingi hutumiwa kuwatafutia watoto mahitaji ya kimsingi.

Mbinu wanazotumia wazazi huathiriwa na hali yao ya kiuchumi. Mbinu za malezi katika riwaya teule zimeathiriwa na hali ya kiuchumi ya wazazi. Kwa mfano, Bwana Mashaka katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ni mlezi mwenye kipato cha juu hivyo, aliwaajiri watu wafanye kazi zote nyumbani. Wanawe hawakufanya lolote nyumbani kwa sababu kazi zote zilifanywa na watumishi. Kwa mfano, Yasibu hakufanya kazi yoyote nyumbani. Kazi zote zilifanywa na watumishi wa nyumbani. Kazi yake ilikuwa tu kwenda shule na kudurusu vitabu. Siku ambayo hakwenda shule kama Jumapili, alilala hadi jua la utosini. Jambo hili linaathiri malezi ya Yasibu kwani hakufanya kazi yoyote nyumbani. Bwana Mashaka anamwambia Bibi Nusura:

> Nilikuwa nimeghafilika kukwambia jambo linalonikera moyoni. Kwa siku chache zilizopita, nimemwona Yasibu akitumwa humu nyumbani. Haifai! Watumishi wapo. Kwa nini yeye atumwe na umri wake ni mdogo (Omari: 4).

Katika Riwaya ya *Tumaini* (2004), Chifu Andrea alitumia hali yake ya kiuchumi kuwahonga watu ili walisimfungulie mashtaka Majuto kwa maovu aliyotenda mtaani Miembeni. Hakuchukua jukumu lake kama mzazi kumshauri Majuto na kumwadhibu kwa sababu alijua atatumia uwezo wake wa kifedha kuwahonga mawakii na hata mwalimu mkuu. Hivyo, alimdekeza mwanawe. Nyumbani, Majuto Hakumsaidia mamake

Bi. Selina kufanya chochote. Kazi zote zilifanywa na watumishi. Jambo ili linamfanya kuwa kaidi na mtovu wa nidhamu. Mwandishi anaeleza:

> Ingawa chifu Andrea alifahamishwa juu ya wizi wa mwanawe, alijitia hamnazo, Maji yalipozidi unga, alihiari kuwahonga walalamishi ilimradi wasimtie Majuto kifungoni. Kijana huyu aliengwaengwa na wazazi wake huku akitimiziwa kila alilotaka. Kwa sababu ya kutendekezwa alijawa na wingi wa tabakuri. (Momanyi: 71).

Wahusika waliotumiwa na waandishi katika riwaya teule ni wa kweli kama inavyoeleza mihimili ya nadharia ya uhalisia. Suala hili linaungwa mkono na utafiti wa Kamau (2016) uliofanywa katika kaunti ya Embu ambao unaeleza kuwa wazazi wenye kipato kikubwa huchukua muda mwingi kuwaelekeza watoto wao na kuwasaidia. Wazazi hawa huwa na matarajio makubwa kwa watoto wao na hufanya juu chini kuhakikisha hakuna kinachotinga matarajio hayo. Bwana Mashaka katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) alikuwa mwenye mali nyingi. Alitumia hali yake ya kiuchumi kuhakikisha kuwa wanawe wamefaulu katika elimu. Kwa mfano, anawaajiri watumishi nyumbani ili watoto wake wasifanye kazi. Watoto wanapokosa kuendelea na masomo anakasirika na kukosa kuwasaidia.

### 3.9 Hali ya Ulevi

Elkins (2018) anaeleza ulevi kuwa uzoefu wa matumizi ya vileo mbalimbali ambavyo huathiri afya ya mwili ya binadamu, akili ya binadamu na pia uhusiano wa binadamu katika jamii.

Kulingana na Winter (2014), Wazazi ambao ni walevi hawana nafasi ya kushirikiana na watoto wao na kuwaongoza. Wazazi hawa hutumia muda mwingi katika mangweni na vilabu. Watoto waliolelewa na wazazi walevi hukosa mwelekeo mzuri katika maisha na wengi wao huwa watundu. Wazazi hawa pia huwadhibu watoto bila sababu yoyote.

Mawazo haya yanaungwa mkono na Buddy (2018) ambaye anaeleza kuwa wazazi ambao ni walevi hawahusiki katika maendeleo ya mtoto nyumbani na hata shuleni. Anaeleza kuwa wazazi hawa hawawalipii watoto wao karo za shule na wanapowalipia hawashirikiani na walimu kuhakikisha kuwa mtoto anaendelea vyema shuleni.

Mzee Masumbuko, katika riwaya ya *Tumaini* (2006) ni mhusika mlevi. Ulevi wake unaathiri jinsi anavyowalea watoto wake. Kila anapokunywa pombe huja nyumbani na kuwaadhibu wanawe bila sababu yoyote. Tumaini anamweleza Bi. Halima kuwa siku moja alimamsha Idi kwa mateke na ngumi. Sababu ni kuwa Mzee Masumbuko alitegwa na gunzi uani. Ulevi unamfanya Mzee Masumbuko kutohusiana vyema na wanawe. Wanawe walimuogopa na hawangemkaribia akiwa katika hali hiyo kwani angewachapa kwa kosa Ndogo tu. Mwandishi anadhibitisha:

> Baada ya kuchapa maji, mzee huyu alisepetuka huku akibwara maneno yaliyosheheni nishai za ulevi.Hapo ndipo wanawe walipomkimbia na kujificha kwani aliwapiga kwa kosa ndogo tu. (Momanyi: 13)

Mzee Masumbuko anataka kumwoza Tumaini ili apate pesa za kutumia ulevini. Anamkasirikia sana yeyote aliyepinga njama yake ya kumuoza Tumaini kwa sababu alikuwa amefisidi mapato yote ulevini. Ulevi ni suala ambalo limeathiri malezi ya watoto katika jamii. Hii ni sawia na unavyoeleza mhimili wa nadharia ya uhalisia kuwa mwandishi hueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu wa maisha. Kwa mfano, Utafiti uliofanywa na Wangui (2017) katika kaunti ya Muranga, unaonyesha kuwa wengi wa wazazi ambao hunywa pombe hawajali watoto wao. Watoto wengi hukosa kupata hata elimu ya msingi. Watoto hawa pia hawana wa kuwatia moyo na kuwafunza maadili kwani wazazi wao hupoteza muda mwingi ulevini. Mzee Masumbuko katika riwaya ya

*Tumaini* (2006) hana muda wa kushiriki na wanawe kwa sababu ya ulevi. Yeye huwadhibu bila sababu yoyote badala ya kuwaelekeza.

### 3.10 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti alishughulikia asasi na hali zinazoathiri mbinu wanazotumia wazazi kuwalea watoto wao. Mbinu za malezi huathiriwa na mambo kadha wa kadha katika jamii. Hivyo, Wazazi hutumia mbinu tofauti kuwalea watoto wao kutegemea asasi na hali inayoathiri malezi yao. Walezi katika riwaya teule wanatumia mbinu tofauti kuwalea wanao. Tofauti hizi zinatokana na mambo mbalimbali. Utamaduni ni mojawapo ya asasi inayoathiri malezi ya watoto katika riwaya teule. Baadhi ya walezi katika riwaya hizi wameathiriwa sana na utamaduni ambao kwa kiwango kikubwa umetatiza malezi ya watoto. Mbali na utamaduni, kuna asasi na hali zingine ambazo huathiri malezi ya watoto. Kwa mfano, asasi ya elimu, asasi ya familia, hali ya jinsia na uana, cheo cha wazazi, ubinafsi na tamaa ya wazazi, hali ya uchumi ya wazazi, taasubi ya kiume na hali ya ulevi.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uhalisia. Mihimili ya nadharia hii iliyotumika ni: Wahusika huwa halisi na lugha wanayotumia huwa rahisi pamoja na kuwa mwandishi husawiri na kueleza hali kwa kuzingatia uyakinifu na uhakika wa maisha. Uchanganuzi huu umegusia lengo la utafiti huu ambalo ni kuchunguza asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto katika riwaya teule. Sura inayofuata, mtafiti atashugulikia athari zinazotokana na mbinu za malezi wanayotumia walezi.

# SURA YA NNE

# ATHARI ZA MBINU ZA MALEZI KATIKA RIWAYA TEULE

## 4.0 Utangulizi

Sehemu hii inaangazia athari za mbinu za malezi wanazotumia walezi kwa watoto na walezi wenyewe. Athari hizi zote zimeangaziwa kwa kuzingatia riwaya teule. Mbinu ya malezi anayotumia mzazi huwa na athari tofauti kwa mtoto. Athari za malezi kwa watoto hutofautiana kulingana na mbinu ya malezi iliyotumiwa. Mihimili ya nadharia ya uhalisia iliongoza utafiti huu. Mhimili wa nadharia uliotumika katika sura hii ni: Kazi ya msanii inapaswa kuonyesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao, jinsi wanavyohisi na kutenda wanapokumbana na hali fulani. Kama ilivyojadiliwa katika sura ya pili, walezi hutumia mbinu mbalimbali kuwalea watoto wao. Mbinu hizi ni kama zifuatazo: Mbinu ya kimabavu, mbinu ya kudekeza, mbinu ya kimamlaka, mbinu ya ushirikiano pamoja na mbinu ya kutojihusisha. Kutokana na mbinu hizi, watoto huathiriwa kwa njia tofauti kulingana na mbinu ya malezi anayotumia mzazi. Athari za malezi huweza kuwa hasi au chanya.

Murphy na Johnson (2011) wanaeleza kuwa mbinu za malezi wanazotumia walezi huwa na athari kubwa kwa mtoto. Mbinu hizi huathiri jinsi mtoto anavyokua na hata maendeleo yake maishani. Wanaendelea kusema kuwa athari hizi zinaweza kuwa za kiakili, kimwili na pia jinsi mtoto anavyohusiana na wanajamii. Kulingana na Cherry (2019) kuna uhusiano kati ya mbinu wanazotumia walezi na athari za mbinu hizi kwa watoto. Anaeleza kwamba tabia wanazopata watoto kwa sababu ya mbinu ya malezi

wanayopewa na wazazi wao huwaathiri wanapokuwa watu wazima. Mbinu wanazotumia walezi katika riwaya ya *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004) zimewaathiri wahusika kwa njia tofauti. Athari hizi ni utengano baina ya wazazi na watoto, wasichana kupata mimba mapema, watoto kutumia dawa za kulevya, watoto kuwa na tabia za wizi na kufungwa jela, watoto kupata maradhi, watoto kukosa matumaini, watoto kuwa na utovu wa nidhamu, wazazi kujuta na kuzorota kwa elimu ya watoto. Kwa upande mwingine, watoto huendelea na masomo iwapo wazazi wanatumia mbinu mwafaka kuwalea.

### 4.1 Utengano katika Familia

Kulingana na Yaffe (2018), mbinu ya kimabavu huwa na athari hasi kwa watoto. Anaeleza kuwa watoto waliolelewa kwa mbinu hii mara nyingi huwa na wasiwasi katika maisha. Wasiwasi huu unatokana na adhabu wanayopata iwapo hawatafuata sheria zilizotungwa na wazazi. Anaeleza kuwa, watoto wengi hutoroka nyumbani ili kujinusuru. Hali hii imeshuhudiwa katika riwaya teule. Kwa mfano, Yasibu katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) anatoroka nyumbani kwao na kutengana na wazazi wake kwa sababu hangeweza kustahimili sheria zilizowekwa na babake baada ya kupata ujauzito. Mzee Mashaka hakumruhusu kutangamana na wenzake. Alikaa nyumbani kama mtawa. Kando na hayo, Mzee Mashaka anakataa kumsaidia kwa vyovyote vile. Kwa sababu hii, Yasibu anaamua kutorokea mjini Mwambao ili kutafuta mahali ambapo angepata amani. Hata anapoambiwa na mamake Bi. Nusura arudi nyumbani anakataa. Mazungumzo ya Yasibu na Bi. Nusura yanatudhihirishia:

> "Yasibu mwanangu, rudi kwenu. Babako akuomba urudi." Bibi Nusura alisema."Sirudi mama! sirudi! Utanisamehe mama kwa kukupinga." Niwache nikapotee na ulimwengu.Yasibu alisema, naye machozi yakimshuka. Aa! Mwanangu, mlani ibilisi! Rudi nyumbani tafadhali! "Vipi nirudi nyumbani kwa baba na baba hanitaki?" Baba hana haja nasi, si mimi, si kakangu Dunia.Niwie radhi mama. "Tuache tukauawe na ulimwengu kuliko mikononi mwa baba aliyetuzaa." Alisema Yasibu.( Omar: 105)

Yasibu anapofika mji wa Mwambao, anakutana na Fakiri na Maria Pori ambao wanamhurumia pamoja na mwanawe na kumsetiri. Yasibu hakutosheka na malezi ya Fakiri na dadake Maua. Anajawa na tamaa ya pesa na mienendo yake inabadilika. Anatoroka kwa kina Fakiri na kwenda kuishi na tajiri mmoja kwa jina Fadhili. Kutokana na uhusiano wake na Fadhili, anaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI ambao unasababisha kifo chake. Yasibu anatengana na familia yake kupita kwa kifo. Kifo cha Yasibu kinatokana na malezi aliyopata kwa babake. Mzee Mashaka anakataa kumsamehe baada ya kupata ujauzito na kumpa nafasi ya kujirekebisha. Mwandishi anadhibitisha:

> Siku mbili baada ya mazungumzo haya, maradhi yalimjia juu kama moto wa kifuu. Fakiri na dadake Maua walimpeleka hospitali ya gharama kubwa ili apate afueni lakini afueni isipatikane asilani. Fakiri alijitahidi kumtafuta Dunia amuarifu hali ya Yasibu lakini hakufua dafu. Hazikupita siku nyingi Yasibu aliaga dunia. (Omar: 201)

Kwa upande mwingine, Dunia pia anatengana na wazazi wake. Anaamua kutoroka nyumbani baada ya kukaidi amri ya babake kuwa angemlipia karo za shule ya upili. Baada ya kufanya mtihani wa darasa la nane, Dunia anapita mtihani huo vyema. Jambo hili linamfurahisha Bwana Mashaka ambaye anamwandalia karamu kubwa na kusema kuwa atamlipia karo za shule ya upili. Dunia anakaidi mawazo ya babake na kusema kuwa hataendelea na masomo. Anaeleza kuwa babake anadanganya kuwa atamlipia karo za shule kwa sababu alikataa kumlipia karo za shule ya msingi. Dunia alisoma kwa fadhili za Mwalimu mkuu. Dunia anaongeza kuwa babake alimchukia na kumpuuza.

Anaeleza kwamba hata chakula mara nyingi alisaidiwa na marafiki. Jambo hili linamkasirisha Bwana Mashaka. Baada ya hayo, Dunia anaamua kutoroka kwani hawangeweza kuishi pamoja na babake. Mwandishi anaeleza:

> Dunia alibaini mambo yamezidi kuingia tata. Nyumbani kwao hakutakalika tena na ni lazima atoroke aende kokote, potelea mbali! Alielewa ni lazima apate wasaa aketi chini amwandikie mamake waraka na ayakinie mamake ataupata waraka huo siku ile atakayotoroka. (Omar: 141)

Utengano pia unajitokeza katika riwaya ya *Tumaini* (2006). Tumaini anaamua kutoroka kwao nyumbani ili aweze kutimiza ndoto yake ya kuendelea na masomo. Anaamka usiku wa manane na kubeba kifurushi cha nguo ili asionekane na mtu yeyote. Hakutaka hata kutazama nyuma kwa sababu nyumba yao ilimkumbusha machungu mengi aliyopitia. Tumaini alikuwa amejaribu kumweleza babake nia yake ya kuendelea na masomo yake lakini Mzee Masumbuko hakumsikiliza. Mzee Masumbuko alimweleza kuwa lazima angefuata sheria zake na kupashwa tohara na baadaye angeolewa kulingana na utamaduni wao. Tumaini anasikitishwa na jambo hili kwa sababu hakuelewa kwa nini babake alishikilia utamaduni ambao ulimdunisha mtoto wa kike. Hivyo, anaamua kujinusuru kutokana na tamaduni hizi kwa kutoroka kwao. Tumaini anawaza:

> Aliwaza jinsi alivyojaribu kumshawishi babake ili aweze kuelewa dhamira yake lakini akawa haambiliki hasemezeki. Kushindana naye hakungefaa chochote, kwa hivyo akaamua kuchukua hatua aliyochukua ya kutoroka. (Momanyi: 5).

Majuto mwanawe Chifu Andrea katika riwaya ya *Tumaini* (2006) pia anatengana na wazazi wake. Anatengana na wazazi wake anapofungwa jela kwa miaka minne. Majuto anafungwa kwa sababu ya tabia zake za wizi. Alipowaibia wenzake shuleni babake alimtetea na akarudi shule. Aliendelea kuwaibia watu vijijini na siku moja walivunja duka la Mhindi pamoja na rafiki zake. Uhalifu huu unawafanya washikwe na kufungwa

kifungo cha miaka minne. Jambo hili linamsononesha sana Bi. Selina ambaye hakuwa na mtoto mwingine. Kufungwa kwa Majuto kunatokana na malezi aliyopewa na wazazi wake. Chifu Andrea hakumrekebisha mwanawe badala yake alimdekeza na kumtetea alipokosea. Mwandishi anaeleza:

> Baada ya majuma mawili, Tumaini alifahamishwa na Ba Mdogo kuwa akina Majuto walipewa kifungo cha miaka minne kila mmoja na kazi ngumu. Walihamishwa na kupelekwa kufungwa katika jela mbali sana na kwao. Tumaini alimsikitikia sana Bi. Selina ambaye majonzi mengi yalizorotesha afya yake. (Momanyi: 149).

Utafiti uliofanywa na Omondi (2015) unaonyesha kwamba asilimia kubwa ya watoto wanaorandaranda mitaani, hutoroka nyumbani kwa sababu ya shida wanazopitia nyumbani. Wengi wa watoto waliohojiwa katika kaunti ya Trans Nzoia wanaeleza kuwa hawakupata mahitaji ya kimsingi. Jambo hili linawaathiri sana na kuamua kutoroka. Kisa hiki kinalingana na kisa cha Yasibu na Dunia katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ambao wanatoroka kwao kwa sababu ya kutelekezwa na wazazi wao.

### 4.2 Mimba na Ndoa za Mapema kwa Wasichana

Kulingana na Brown (2018) mimba za mapema zinatokana na watoto kukosa ushauri mwema kwa wazazi wao. Anaeleza kuwa wazazi wanapokosa kuwaongoza watoto wao, watoto hutafuta suluhu kwa marafiki wao ambao wakati mwingine huwapotosha. Naye Dinorah (2015) anaeleza kuwa kina baba wanafaa kuonyesha upendo kwa wasichana walio baleghe kwa sababu wanapokosa kuwapenda, wasichana hawa hutafuta upendo kwa wanaume na mwishowe hutungwa mimba wakiwa wachanga. Anaendelea kusema kwamba bali na kupendwa, wazazi wanafaa kuzungumza na watoto wao, kuwaongoza, kutunga sheria zinazofaa kwa kujenga mipaka na kutowaruhusu kufanya watakavyo.

Anaeleza kuwa kuwachapa watoto hawa sio mbinu nzuri kwa sababu wakati mwingine watoto hupinga mbinu hiyo.

Mimba za mapema kwa wasichana katika riwaya teule zinatokana na mbinu ya malezi wanayotumia wazazi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) Yasibu anapata mimba akiwa darasa la saba. Yasibu anatungwa mimba na Pazia baada ya babake Mzee Mashaka kumpa uhuru wa kufanya atakalo. Hapo awali Yasibu alikuwa amefungiwa nyumbani. Hakuruhusiwa kutangamana na wenzake jambo ambalo linamhuzunisha sana na akamwomba babake amruhusu kutangamana na wenzake. Mzee Mashaka bila kuwazia jambo hili anamruhusu kufanya atakalo bila kumpinga. Mzee Mashaka anamweleza Bi. Nusura:

> Ni bora tumwache Yasibu afanye lile apendalo nyumbani humu. Tusimpinge wala tusimzuie sana. Hilo ni shauri langu, wasemaje? Alisema na kuuliza Bwana Mashaka. Hiyo ni busara kweli? Bibi Nusura alimuuliza kwa mshangao. "Naam, naona ni busara.Ndivyo alivyotaradhia." Mumewe alijibu. (Omar: 24).

Baada ya Yasibu kupewa uhuru wa kufanya atakalo, tabia na mwenendo wake unabadilika. Heshima kwa wazazi wake ilitoweka hususan kwa mamake. Aghalabu alirudi nyumbani wakati giza lishatanda. Mzee Mashaka anamweleza Yasibu:

> Nasikitika kusema ubaradhuli na dharau zimekuwa kwako ni kama ada. Huna adabu kwa sisi wazazi wako tuliokuzaa. Watufanya si lolote wala si chochote. (Omar: 31)

Yasibu hakuambiwa chochote tena na wazazi wake. Anakaidi amri zote anazopewa na wazazi wake. Pia, anahusiana kimapenzi na Pazia rafikiye Dunia ambaye anamwahidi kuwa atamuoa. Baadaye, afya ya Yasibu inaanza kubadilika. Alitapika kila wakati na uvivu ukamzidi. Bi. Nusura aliyaona mabadiliko haya na akamuuliza mwanawe. Mwandishi anaeleza:

> Bibi Nusura aliyaona mabadiliko ya mwanawe, akayapeleleza kwa makini sana hadi akatambua yalivyobashiri na yasivyobashiri mambo mazuri kabisa! Alipomdadisi mwanawe kuhusu aliyemletea janga hilo alishtuka kuambiwa ni Pazia rafikiye Dunia. (Omar: 75).

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006) mbinu zinazotumiwa na wazazi kuwalea watoto wa kike zinachangia kuolewa kwa wasichana wakiwa wachanga. Mbinu hizi zinachochewa na utamaduni ambao unamtweza mtoto wa kike. Tumaini anakumbuka kisa cha Zena ambaye alibebwa na vijana makatili kwa amri za babake na kupelekwa kwa Mzee Chumo kama mke wa nne. Kilichomshangaza Tumaini ni kwamba hakuna aliyemsaidia Zena kwa sababu lilikuwa jambo la kawaida. Elimu ya Zena inakatizwa anapoolewa. Mwandishi anaeleza:

> Hapo Zena angejitokeza mbele ya kaumu akiwa na mume wake Mzee Chumo. Hata kama hakuyafurahia yote yale kutokana na lazima za wazazi kuolewa, angelazimika kutia tabasamu la bandia ili mradi afurahishe umati. ( Momanyi: 50)

Dada zake Tumaini, Rehema na Mashaka wanakosa kuendelea na masomo yao baada ya kumaliza shule ya msingi. Mzee Masumbuko alipokea mahari ya Mashaka akamwoza kwa lazima kwa Mzee Lusimbo kama mke wa tatu. Ingawa Mashaka alipita mtihani wake wa darasa la nane, na alikuwa na hamu ya kuendelea na masomo yake hakuweza kuendelea kwa sababu ya tamaa ya babake. Alipashwa tohara na baadaye akaolewa. Rehema naye alikosa kujiunga na darasa la nane. Babake aliletewa posa akaolewa na Shauri, fundi wa baiskeli. Barua ya Idi kwa Tumaini inaeleza haya:

> Tumaini alijushwa kwamba Rehema hakujiunga na darasa la nane kwani babake aliletewa posa kisha Rehema akaolewa. Aliolewa na fundi wa baiskeli aliyeitwa Shauri. Mashaka aliamua kusoma lakini lililomkera Tumaini ni kwamba tayari huyu alikwisha tafutiwa mchumba. Hivyo, baada ya elimu ya msingi yeye pia angeolewa. (Momanyi: 111)

Suala la watoto kuolewa mapema ni la kiuhalisia. Watoto walioozwa huathiriwa kiakili na kisaikolojia kwa sababu mara nyingi huolewa na watu wasiowafahamu na ndoto zao za maisha hukatizwa. Ojiambo (2018) anaeleza kuwa sababu za wasichana wengi kuolewa mapema huchochewa na mbinu za malezi zinazotumiwa kuwalea. Malezi ya watoto hawa huathiriwa na tamaa na tamaduni za jamii ambazo humtweza mtoto wa kike. Zena na dada zake Tumaini katika riwaya ya *Tumaini* (2006) wanapashwa tohara na kuozwa kutokana na tamaa ya baba yao na utamaduni wa jamii hiyo. Jambo hili linawafanya wakose kuendelea na masomo ambayo ni muhimu katika maisha ya mtoto.

### 4.3 Wizi na Watoto Kufungwa Jela

Johnson (2016) anaeleza kuwa wazazi wanafaa kutumia mbinu zifaazo kuwalea watoto wao ili kupunguza visa vya uhalifu na kufungwa jela kwa watoto wengi**.** Anaeleza kuwa watoto waliolelewa kwa kutumia mbinu ya kimabavu huwa watiifu kwa kufuata sheria zilizotungwa na wazazi wao na pia kuogopa adhabu watakayopata iwapo hawatafuata sheria hizo. Pia, anaeleza kuwa watoto waliolelewa kwa mbinu ya kimabavu wakati mwingine hukaidi amri walizotungiwa na kuwa na utovu wa nidhamu. Anaendelea kusema kuwa ni nadra sana kupata visa vya uhalifu kwa watoto ambao wamelelewa kwa njia ya kimamlaka. Visa vingi vya uhalifu hutoka kwa watoto waliolewa kwa mbinu ya kudekeza na kutojihusisha. Jambo hili linatokana na kuwa wazazi huwaachia watoto uhuru wa kufanya watakalo na wengi hujiingiza kwa matendo yasiyofaa.

Hirschi (2009) anaeleza kuwa mbinu za malezi wanazotumia wazazi huwa kichocheo cha watoto kufanya maovu na kufungwa jela. Anaeleza kuwa wazazi ambao hawafuatilii maendeleo ya watoto wao na kuwaongoza huchangia pakubwa katika kufanya maovu na

kufungwa jela kwa watoto. Anaendelea kusema kuwa matumizi ya adhabu kali huwafanya watoto kuzoea adhabu hizo na kuendelea kufanya maovu na baadaye kufungwa jela.

Watoto wengi wanapokosa malezi mema hufanya uhalifu na kufungwa. Katika riwaya teule kuna visa vya watoto kufungwa jela kwa sababu ya kuvunja sheria. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu*, (2004) mhusika Dunia anafungwa jela. Dunia anapokosa kustahimili matatizo aliyokumbana nayo kwao nyumbani ikiwa ni pamoja na kupuuzwa na babake, anatorokea mji wa Mwambao. Katika mji wa Mwambao, anakumbana na madhila tofauti tofauti. Kwanza, anapoenda kuoga, mkoba wake unaibiwa. Anatoka nje akiwa nusu uchi na kushikwa na askari ambao wanamshuku kuwa jambazi. Mazungumzo ya Dunia na askari yanadhihirisha:

> Sisi ni askari. Jina lako ni nani? Naitwa Dunia. Dunia Mashaka. Wafanya nini hapa saa hizi Dunia, tena ukiwa nusu uchi? Wewe ni jambazi! Leo ni leo utalala korokoroni. Dunia aliambiwa. (Omar: 163)

Pale gerezani, Dunia anajenga uhusiano na mmoja wa wafungwa kwa jina Mpoto. Mpoto alikuwa amefungwa kwa kosa la wizi. Mpoto anamweleza Dunia kwamba alianza tabia ya wizi akiwa na miaka kumi na miwili. Mpoto anasikitishwa na kufungwa kwa Dunia. Anamweleza kuwa amesikia tetesi kwamba Dunia alikataa shule. Mpoto anamwambia Dunia kwamba angekuwa na wa kumwelimisha hangekuwa pale gerezani. Alikosa wa kumwelimisha baada ya wazazi wake kuaga dunia kwa ugonjwa usiokuwa na tiba hivyo, akaamua kujiingiza katika wizi ili kukidhi mahitaji yake.

Inasadifia kuwa siku ya Dunia kutoka gerezani baada ya kifungo cha miezi sita ndiyo Mpoto alikuwa anatoka. Dunia na Mpoto wanakodisha chumba kimoja. Mpoto anamfunza Dunia matendo ya wizi. Siku moja walienda kuiba. Kwa bahati mbaya Mpoto alishikwa na Dunia akanusurika kwa muda mfupi. Dunia alikodisha chumba kingine ili asipatikane lakini hazikupita siku nyingi bila yeye kushikwa. Alifungwa miezi minne. Kachero anamwambia Dunia:

> Kijana Dunia Mashaka, mimi ni kachero Koho. Kutoka sasa wewe ni mahabusu na litakuwa jambo la fahari kubwa kwangu nikikupiga risasi lau utajaribu kutoroka. Inua mikono yako. Dunia hakushindana, akifahamu kuwa siku za mwizi ni arubaini na arubaini yake ndiyo hiyo imetimu. (Omar: 205).

Majuto katika riwaya ya *Tumaini* (2006) alifanya uhalifu wa kila aina. Kwa sababu ya uhalifu huu, alifungwa jela mara kadhaa. Uhalifu wa Majuto unatokana na malezi aliyopata kutoka kwa wazazi wake. Chifu Andrea alitumia mbinu ya kutojihusisha na kudekeza. Chifu Andrea alipofahamishwa kuhusu wizi wa mwanawe alimtetea kila mara. Wakati mwingine aliwahonga walalamishi ili wasimtie Majuto kifungoni. Mwandishi anaeleza:

> Ingawa chifu Andrea alifahamishwa juu ya wizi wa mwanawe, alijitia hamnazo. Mambo yalipozidi unga, alihiari kuwahonga walamishi ilmradi wasimtie Majuto kifungoni. Kijana huyu aliengwaengwa na wazazi wake huku akitimiziwa kila alilotaka. (Momanyi: 71)

Majuto aliendelea na tabia yake ya wizi kwa sababu ya kutetewa na wazazi wake na mwishowe alifungwa. Kwa mfano, siku moja walienda kuvunja duka la Mzee Karim na kumkaba koo mkewe kisha wakatoroka na kisanduku cha mali. Mzee Karim alipiga ripoti katika kituo cha polisi na wezi hao wakaanza kutafutwa. Baada ya siku chache, polisi waliwapata wezi hao. Polisi walianza kuwafyatulia risasi na kwa bahati mbaya risasi

ilimpata Majuto kwenye muundi akaanguka. Alitiwa pingu na kupelekwa hospitalini akiwa bado ana pingu mikononi. Mwandishi anaeleza:

> Majuto alitiwa pingu na kupeleka hospitalini. Akiwa bado ana pingu mkononi, alifungwa mnyororo mrefu katika mguu ule mwingine. Kisha mnyororo huo ukafungwa kwenye kitanda. Polisi wawili wakiwa na bunduki walimlinda alikolala. (Momanyi: 43)

Suala la kufungwa jela ni la kiuhalisia. Watoto wanaofungwa jela huathiriwa sana. Utafiti uliofanywa na Mwanjala (2015) katika kaunti ya Taita Taveta unaonyesha kuwa visa vingi vya watoto kufungwa jela vinatokana na wazazi kuwatekeleza watoto wao na kutojihusisha katika malezi ya watoto wao. Utafiti huu unaonyesha kuwa watoto wengi hupata athari kubwa za kiakili na kufanya maovu ambayo hawakupangia.

### 4.4 Utovu wa Nidhamu

Kulingana na Zubaida (2009) utovu wa nidhamu unahusisha mambo yafuatayo: Kutoroka shuleni, kutowaheshimu wazazi na walimu, kutukana wengine, wizi na tabia zingine ambazo hazikubaliwi katika jamii. Anaendelea kusema kuwa utovu wa nidhamu kwa watoto unatokana na mbinu za malezi wanazotumia wazazi kuwalea watoto wao. Watoto ambao hudekezwa na wazazi wao huwa na utovu wa nidhamu kwa sababu wanaelewa kwamba hata wakifanya jambo mbaya wazazi wao watawatetea ikilinganishwa na watoto ambao wamelelewa kwa mbinu ya kimamlaka. Watoto wanaolelewa na mbinu ya mamlaka huongozwa vyema na wazazi wao na kuadhibiwa wanapokosea hivyo hudumisha nidhamu kwa kuogopa adhabu.

Watoto wengi hukosa kudumisha nidhamu shuleni na hata nyumbani kwa sababu ya mbinu za malezi wanazotumia wazazi. Katika riwaya teule, kuna visa vya watoto kukosa nidhamu. Visa hivi vinatokana na mbinu za malezi wanazotumia walezi.  Katika riwaya

ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) Yasibu anakosa kuwaheshimu wazazi wake baada ya kupewa uhuru wa kufanya atakacho na babake. Yasibu anaanza kurudi nyumbani usiku na kutotii wazazi wake. Mzee Mashaka anapogundua kuwa tabia za Yasibu zimebadilika, anamtungia sheria zingine na kumpa mawaidha. Yasibu anakaidi amri hizo na kupinga lolote analoambiwa na babake. Mazungumzo ya Yasibu na Mzee Mashaka yanadhihirisha:

> "Hakuna cha baba!" Amri zangu zisikilize kwa makini na usizikinze. Sikuruhusu tena kutoka pasi na kuaga. Sitaki zaidi mwanangu ila uniambie tu: Baba mimi natoka. Pili ukitoka shuleni sharti ukimbilie nyumbani...Bwana Mashaka alisema. Ba, n'muhali mimi kuyakiri hayo. Yasibu alisema huku akisimama, kajaliza, Siwezi tena hali hiyo. "Usinipinge!" Bwana Mashaka alikipuka. Yasibu aligeuka akampa mgongo babake huku akinong'ona. "Ni afadhali mtu anywe sumu afe kuliko adhabu hiyo."(Omar: 31).

Dunia pia anakosa nidhamu anapomwaibisha babake katika sherehe ya kufaulu kwake. Utovu huu wa nidhamu unatokana na Bwana Mashaka kumpuuza. Bwana Mashaka anapokataa kumsaidia Dunia, Dunia anapata usaidizi kwa rafiki yake Pazia. Pazia anamshauri asikubali ahadi za babake za kumlipia karo za shule ya upili kwani alikuwa amekataa kumlipia na kumsetiri hapo awali. Bwana Mashaka anaomba msamaha kwa kujawa na chuki na kukosa kumsaidia na kumlipia karo za shule. Dunia anakataa katakata kumsamehe na kusema kuwa hataendelea na masomo hata baada ya kushauriwa na mamake na walimu wake.

Idi katika riwaya ya *Tumaini* (2006) anakosa kudumisha nidhamu. Hana heshima kwa dada zake. Idi anakosa kuwaheshimu dada zake kwa sababu ya malezi aliyopata kwa babake. Aliwaona dada zake kama watumishi tu pale nyumbani. Kila mara aliwaambia wao ni bidhaa za uwekezaji na walihitaji kuolewa. Tumaini alipomweleza babake kauli

za Idi, Mzee Masumbuko alimkemea na kumkanya kutoingilia malezi ya Idi kwani yeye ni mtoto wa kiume na alihitaji kuwa na roho ngumu kama yeye.

Majuto pia anakosa kudumisha nidhamu nyumbani na shuleni. Utovu wa nidhamu unatokana na kudekezwa na babake. Majuto aliwasumbua wenzake darasani. Tumaini anakumbuka jinsi Majuto alivyoadhibiwa na mwalimu na kuambiwa apige magoti nje somo lilipokuwa likiendelea. Majuto alianza kugonga darasa kwa kurusha mawe. Pia, alifukuzwa shule mara kadha lakini babake alimtetea akitumia cheo chake akakubaliwa fursa nyingine. Kwa mfano, siku moja Majuto pamoja na mwenzake Kijungwe walivunja afisi ya mwalimu mkuu na kuiba vitabu ambavyo walimuuzia Bwana Karim aliyekuwa na duka kubwa. Wazazi wao walilazimika kulipa gharama ya mali yote iliyoibiwa. Mwandishi anaeleza:

> Mara kadha Majuto alifukuzwa shule kwa sababu ya utovu wa nidhamu lakini Bwana Andrea alimtetea mwanawe huku akitumia cheo chake na Majuto alikubaliwa fursa nyingine. (Momanyi: 21)

Nyumbani hali haikuwa tofauti kwa Majuto. Aliwaangaisha mabinti za watu kwa kuwabaka na kuiba mali ya watu. Watu walipomlalamikia chifu, alimtetea mwanawe. Tumaini anapofanya kazi kwao, Majuto anajaribu kumbaka lakini Tumaini anajinusuru. Tumaini anasema:

> "Nikaribie uone ikiwa wewe kweli ni mwanamume. Unadhani mimi ni kama wale unaowavizia mitaroni!"(Momanyi:89).

Suala la utovu wa nidhamu ni la kiuhalisia. Mhimili wa nadharia ya uhalisia unaeleza kuwa kazi ya msanii inapaswa kuonyesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao. Wahusika mbalimbali katika riwaya teule wanakumbwa na hali tofauti tofauti wanapoathiriwa na malezi wanayopata. Kwa mfano, huzuni, wasiwasi

na hata woga.  Jambo hili si tofauti katika hali ya kawaida. Kwa mfano, Kwamboka (2018) anaeleza kuwa utafiti uliofanywa katika kaunti za Embu, Nakuru, Kisii, Nyamira na Kericho unaonyesha kwamba utovu wa nidhamu kwa watoto unatokana na wazazi kukosa nafasi ya kuwashauri watoto na kuwaachia walimu wajibu huo. Anaeleza kuwa utovu wa nidhamu unasababisha migomo mingi katika shule za upili ambayo inawaletea watoto shida nyingi kama vile, maafa, uharibifu wa mali na pia kupoteza muda mwingi wa masomo. Migomo hii huathiri watoto kiakili na hata kifya. Kwa mfano, wanafunzi wengi hupoteza bidhaa nyingi, hujeruhiwa na hata hujawa na woga.

**4.5 Watoto kukumbwa naMaradhi**

Anzilotti (2017) anaeleza kuwa watoto wengi hupata magonjwa ya zinaa kwa sababu ya kukosa ushauri mwema kutoka kwa wazazi. Anaeleza kuwa ni jukumu la wazazi kuwaelimisha watoto kuhusu magonjwa hayo ili wajiepushe na mienendo ambayo inawafanya wapate magonjwa hayo.

Wahusika katika riwaya teule wanakumbwa na maradhi mbalimbali. Bwana Mashaka anakataa kumsamehe Yasibu baada ya kutungwa mimba na Pazia. Hivyo, Yasibu anaamua kutoroka kwao na kwenda mji wa Mwambao. Katika mji wa Mwambao, Yasibu anabadilisha mienendo yake. Kwa mfano, anajiingiza katika anasa na starehe za dunia. Katika harakati zake mjini Mwambao, anapatana na tajiri mmoja kwa jina Fadhili. Fadhili anampa zawadi nyingi na kumwahidi kuwa atamuoa. Yasibu anafurahi sana na kuolewa na Fadhili. Katika uhusiano wao, Yasibu anapata mtoto mwingine kwa jina Majuto. Mbali na kupata mtoto, Yasibu anaambukizwa ugonjwa wa UKIMWI ambao unasababisha kifo chake. Mazungumzo ya Yasibu na mpakaji viatu rangi yanadhihirisha:

> Namtaka mwenye nyumba hii. Nimekuja nikutane na Bwana Fadhili. Yasibu alijibu. Kwani huna habari mama kuwa Fadhili alifariki mwezi jana?" Aa! Sina habari amefariki kwa maradhi gani? Yasibu aliuliza kwa masikitiko. Alifariki kwa maradhi yasiyo na tiba. Mpakaji viatu rangi akaeleza.Yasibu alishtushwa na habari hizi. Mama ee! Maskini mimi Yasibu. Aa, kilichompata ngwena na kiboko n'chicho," alijiambia kwa jitimai. (Omar: 185).

Utafiti uliofanywa na Lake (2015) unaonyesha kuwa asilimia kubwa ya watu walio na ugonjwa wa UKIMWI ni vijana walio kati ya miaka kumi na tano na kumi na tisa. Utafiti huu unaonyesha kuwa mojawapo ya sababu zinazowafanya vijana kuambukizwa ugonjwa wa UKIMWI ni ukosefu wa ushauri kutoka kwa wazazi na walimu. Utafiti huu unaeleza kuwa ni vyema wazazi wajihusishe katika malezi ya watoto wao ili kuwapa ushauri unaofaa na kuwaelekeza. Utafiti huu pia unaonyesha kuwa watoto wanapopata ugonjwa wa UKIMWI huathirika kiakili na hata kimwili. Hii ni sawia na mhimili wa nadharia ya uhalisia ambao hueleza kuwa hali ya kisaikolojia ya wahusika huathirika wanapokumbana na jambo fulani. Kwa mfano, Yasibu anapoambukizwa ugonjwa wa UKIMWI na Fadhili, anaathirika kimwili na hata kiakili.

### 4.6 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Sharma (2015), anaeleza kuwa kuna uhusiano kati ya mbinu za malezi wanazotumia wazazi na matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa watoto. Anaeleza kuwa watoto wanaoshauriwa na kuelekezwa na wazazi wao vyema hawatumii dawa za kulevya. Anasema kuwa watoto wengi hutumia dawa za kulevya ili waweze kusahau madhila yanayowakumba nyumbani. Hivyo basi, wazazi wanafaa kuwa na uhusiano mwema na watoto wao ili wawaelewe na kuwasaidia iwapo kuna tatizo.

Watoto wanapokosa malezi mema huanza kutumia dawa za kulevya ili kujiliwaza kutokana na matatizo wanayopitia nyumbani. Katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu*

(2004), Dunia anaanza kutumia vileo baada ya babake Bwana Mashaka kukataa kumsamehe na kumsetiri. Mzee Mashaka anapokataa kumshugulikia mwanawe Dunia, Dunia anatafuta usaidizi kwa rafikiye Pazia. Pazia naye hakusita kumsaidia kwa sababu hapo awali Dunia alikuwa amemsaidia. Kutokana na uhusiano wake na Pazia, Dunia alianza kutumia vileo vya kila aina. Cha kushangaza ni kuwa Pazia aliwatafutia, kuwakusanyia na kuwapatia rafiki zake wa chanda na pete lakini yeye hakutumia vileo hivi.

Dunia anapofaulu mtihani wake wa darasa la nane babake anaandaa karamu ya kukata na shoka ili kusherekea matokeo ya mwanawe. Kabla ya sherehe, Dunia anaenda kwa rafiki yake Pazia kumweleza mipango ya babake. Pazia anamweleza kuwa babake Bwana Mashaka anamdanganya kwa sababu alikuwa amempuuza kwa muda mrefu. Pazia anamshauri Dunia kuwa asikubali ahadi za babake kwani ni za uwongo. Kando na hayo, anampatia Dunia vileo ili aweze kumpinga vizuri babake katika karamu. Pazia anamweleza Dunia:

> Ndivyo hasa Dunia! Washa sigara uburudike, uyafukuze mawazo. Nyaka!" Pazia alisema huku akimrushia Dunia msokoto wa sigara kali. Dunia alinyaka. Pazia aliendelea kusema, "siku hiyo ya hadhara Dunia, haifai uwe kichwa kikavu, utashindwa na mambo. Ni lazima siku hiyo ujitie vikali kichwani ndipo utakapokuwa imara. Nitahakikisha siku hiyo umewaka. Poa?" Poa kabisa!" Dunia alijibu. (Omar: 129)

Shida wanazopitia watoto nyumbani huwafanya watoto kutumia dawa za kulevya. Utafiti uliofanywa na Ombere (2014) katika kaunti ya Nairobi, unaonyesha kuwa watoto wengi huanza kutumia dawa za kulevya baada ya kutelekezwa na wazazi wao. Baadhi ya dawa wanazotumia ni sigara, pombe na bangi. Watoto wengine pia huanza kutumia dawa za kulevya baada ya kuwaona wazazi wao wakitumia. Hivyo, watoto huwaiga wazazi kwani

wazazi ndio kielelezo kwa watoto. Suala hili ni la kiuhalisia kwani Dunia katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) anaanza kutumia vileo na sigara baada ya babake kumtelekeza. Anafanya hivi ili asahau shida alizokuwa akipitia nyumbani.

### 4.7 Kuzorota kwa Elimu ya Mtoto

Kulingana na Kipyegon (2017), elimu ndiyo msingi wa maisha. Hivyo, watoto wanahitaji mazingira bora katika familia zao ili waweze kufanya vyema masomoni. Ufanisi wa elimu kwa mtoto huchangiwa na aina ya malezi anayopata kutoka kwa walezi wake. Hii inatokana na hali kwamba mzazi ndiye mwalimu wa kwanza wa mtoto na jinsi atakavyomlea huchangia pakubwa katika maendeleo ya mtoto huyo.

Wazazi wengi hufurahia wanao wanapofanya vyema katika masomo yao. Jambo hili huwafanya watie bidii kuhakikisha kuwa wanao wamepata elimu inayofaa. Hata hivyo, kuna wazazi ambao hawashughuliki na elimu ya watoto wao kwa kuwa aidha hawaoni umuhimu wa elimu au hawana muda wa kuwasaidia watoto wao. Elimu ya mtoto pia inaathiriwa na mbinu za malezi wanazotumia walezi. Mbinu hizi huweza kuwa na athari hasi au chanya kwa elimu ya mtoto. Waandishi wa riwaya teule wameonyesha jinsi mbinu za malezi wanazotumia walezi zinavyoathiri elimu ya mtoto. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004), elimu ya wahusika Dunia na Yasibu inaathirika kwa sababu ya mbinu za malezi zinazotumiwa na wazazi wao. Bwana Mashaka anapompa Yasibu uhuru wa kufanya atakalo, tabia na mienendo ya Yasibu inabadilika na maendeleo yake shuleni yanazorota. Mwishowe, Yasibu anahusiana na Pazia ambaye anamtunga mimba na kisha kuacha masomo yake akiwa darasa la saba. Mazungumzo ya Mzee Mashaka na Yasibu yanadhibitisha haya:

> Mabadiliko ya afya yako yamenipendeza tangu nilipokupa idhini ya kujiamulia mambo yako mwenyewe. Ingawa mambo mawili au matatu hivi yanitia wasiwasi moyoni. Mambo gani ba? Yasibu alimkatiza kauli. Maendeleo yako shuleni yamezorota. Nashangaa kuona mwanafunzi aliyezoea kushika rakamu ya pili alipoikosa ya kwanza katika mtihani sasa akiibuka rakamu ya ishirini dhidi ya wanafunzi ishirini na watatu. (Omar: 30).

Baada ya Yasibu kujifungua, anakosa nafasi ya kuendelea na masomo yake kwa sababu ya ugumu wa babake. Mzee Mashaka anakataa kumsamehe mwanawe kabisa na hata kumsetiri. Anajawa na uhasama mwingi ambao unamfanya Yasibu kutoroka na kukumbana na matatizo mengi.

Kwa upande mwingine, Dunia pia hakuendelea na masomo yake. Kwanza, Dunia anamkosea babake kwa kukataa kwenda shule lakini baada ya muda mfupi anabadilisha msimamo wake na kuamua kurudi shule. Mzee Mashaka anakataa kumsikiliza na kusema kuwa kuzaliwa kwake Dunia kumeleta nuksi nyingi katika familia yake. Mzee Mashaka anashawishiwa na Mwalimu mkuu Bwana Busara amsamehe Dunia lakini anakataa. Dunia anasoma kwa ufadhili wa Mwalimu Busara na anafanya vyema katika mtihani wake wa darasa la nane. Jambo hili linamfurahisha sana Mzee Mashaka ambaye anaahidi kuwa atamsomesha Dunia hadi chuo kikuu. Dunia kwa ushauri wa Rafikiye Pazia anasimama na kusema kuwa hataendelea na masomo kwa sababu babake alimpuuza na akakataa kumlipia karo za shule. Anaeleza kuwa babake hana nia nzuri naye. Usemi wa Dunia unamkasirisha Mzee Mashaka ambaye anataka kumchapa hadharani. Dunia anabaini kuwa nyumbani kwao hakungekalika tena hivyo anaamua kutoroka. Dunia anaeleza:

> Sijamfahamu baba tofauti na mtu aliyenichukia na kunipuuza. Hata chakula mara nyingine nilisaidiwa na marafiki. Karo za shule nazo sikulipiwa na baba. Nilisoma kwa fadhili za mwalimu mkuu wa shule. Sina hamu ya kusoma. Sina hamu maana sioni faida yake. Siwezi kumfadhili baba fadhili ambazo hakunifadhili. (Omar: 137)

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), dada zake Tumaini, Rehema na Mashaka wanakosa kuendelea na masomo yao kwa sababu ya mbinu za malezi alizotumia Mzee Masumbuko. Mzee Masumbuko hakuwa na uhusiano mwema na wanawe hasa wa kike. Alichukulia kwamba watoto wa kike walifaa kupashwa tohara na kuolewa. Mtazamo huu ulitokana na itikadi za jamii yao. Ingawa Mashaka alifanya vyema katika masomo yake, alikosa kuendelea na masomo yake na kuolewa. Idi, mwanawe Mzee Masumbuko aliweza kuendelea na masomo hadi kidato cha nne kwa sababu ni mtoto wa kiume.

Majuto anakosa kuendelea na masomo kwa sababu ya kudekezwa na wazazi wake. Chifu Andrea alimdekeza na kumtimizia kila alichotaka. Hata alipowaibia wenzake shuleni, babake alimtetea kwa mwalimu mkuu. Mwishowe, alikosa kuwatii wazazi wake na walimu na kufukuzwa shule. Mwandishi anaeleza:

> Kijana huyu aliengwaengwa na wazazi wake huku akitimiziwa kila alilotaka. Kwa sababu ya kutendekezwa, alijawa na wingi wa tabakuri. Mwishowe hakuwatii wazazi hata walimu wake. Baada ya kufukuzwa shule, alikuwa tisho mitaani. (Momanyi: 71)

Kwa upande mwingine, Wazazi wanapotumia mbinu zinazofaa kuwalea watoto wao, Watoto huweza kufanya vyema katika masomo. Katika riwaya ya *Tumaini* (2006) kuna mifano ya wahusika ambao wamefaulu katika elimu kwa sababu ya mbinu za malezi zilizotumiwa kuwalea. Wahusika hawa ni Riziki, mwanawe Shaban na Bi. Halima, Tumaini na Sifa mwanawe mzee Majaliwa. Riziki, mwanawe Shaban na Bi. Halima aliendelea na masomo yake. Hii ilitokana na mbinu walizotumia walezi wao. Shaban na Bi. Halima walimlea mwanao kwa kutumia mbinu ya kimamlaka na ushirikiano.

Walimshauri na kumwongoza kila wakati. Kutokana na Malezi haya, Riziki aliendelea na masomo na akajiunga na chuo cha ualimu. Ufanisi wake ulitokana na jinsi wazazi wake walivyojitolea kuhakikisha kwamba hakuna kilichomzuia kuendelea na masomo yake. Mwandishi anaeleza:

> Shaban aliweza kumsomesha Tumaini bila shida kwa sababu ya ile hazina aliyookota. Baada ya kuichimbia chini kwa mwaka mmoja, aliifukua, na kutafuta wateja kwa siri. Alifanikiwa kuuza bila matatizo, akawa na pesa za kutosha za kumsomesha bintiye Riziki ambaye alijiunga na chuo za ualimu baada ya kidato cha nne. (Momanyi: 114)

Baada ya Tumaini kwenda kwa shangaziye Bi. Halima, aliendelea na masomo hadi chuo kikuu. Shaban na Bi. Halima walimlea kama mwanao Riziki. Mara nyingi Shaban alimsomea Tumaini vitabu vya Shaaban Robert kuhusu utu wa binadamu na tabia bora. Aghalabu alimkumbusha umuhimu wa kutia bidii katika maisha ya binadamu na kumhimiza kutia bidii masomoni. Kutokana na malezi hayo, Tumaini alifaulu mtihani wa kidato cha nne na kujiunga na chuo kikuu kusomea udaktari. Tumaini anamweleza Sifa:

> "Nami naenda kusomea udaktari katika mawanda ya matibabu mbalimbali," alitamka Tumaini. (Momanyi: 155)

Sifa, rafikiye Tumaini, aliendelea na masomo yake kwa sababu ya malezi aliyopewa na wazazi wake. Babake, Mzee Majaliwa alimhimiza kutia bidii masomoni na kumnunulia zawadi kila alipofaulu. Kwa mfano, kuna wakati ambapo babake alimnunulia baiskeli alipofaulu. Baadaye anafaulu katika mtihani wa kidato cha nne na kujiunga na chuo kikuu kusomea udaktari katika taaluma ya meno.

Utafiti uliofanywa na Kombo (2015) unaonyesha kuwa maendeleo ya elimu kwa mtoto hutokana na mbinu za malezi wanazotumia wazazi. Wazazi ambao hujihusisha na elimu ya mtoto na kushirikiana na walimu hufanya vyema kuliko watoto waliotekelezwa na

wazazi wao. Katika kaunti ya Nairobi wanafunzi waliofanya vyema ni wale waliofuatiliwa na wazazi wao na kuwaongoza. Kisa cha watoto hawa kinalingana na kisa cha Tumaini na Riziki katika riwaya ya *Tumaini* (2006) ambao wanafaulu katika masomo yao kupitia kwa juhudi za wazazi wao.

### 4.8 Majuto kwa Wazazi

Crow (2018) anaeleza kuwa wazazi wengi hujuta baada ya kutumia mbinu fulani ya malezi. Majuto haya yanatokana na athari za mbinu walizotumia hasa athari mbaya. Wengi wa wazazi huanza kujuta kwa nini hawakutenga muda mwingi kwa watoto wao. Kuna wale hujuta kwa kuwatungia watoto sheria kali ambazo hazikuwasaidia maishani.

Katika riwaya teule, wahusika mbalimbali wanajuta baada ya kutekeleza mbinu tofauti za malezi. Majuto haya yanatokana na kutofanikiwa maishani na athari mbaya za mbinu hizo za malezi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004), Bwana Mashaka anajuta baada ya wanawe kutoroka na Yasibu kuaga dunia. Anajilaumu kwa kutowasikiliza wanawe na kufuata mawazo ambayo hayakusaidia jamii yake. Anawaomba wanawe wamsamehe kwa kukosa kuwaelewa na kuwapa nafasi ya kujirekebisha. Bwana Mashaka anawaza:

> Nimeidhalilisha jamii yangu kwa kufuata mawazo yasiyo na msingi katika maisha. Mwanangu Yasibu nisamehe kuzimu uliko. Moyo wangu mgumu ulikunyima nafasi ya kujirekebisha. Mwanangu Dunia nawe nisamehe. Mimi sina budi kukusamehe leo hapa ulimwenguni na kesho huko mbinguni. Mimi babako sikujaribu kukuelewa. (Omar: 222).

Bi. Selina, mamake Majuto katika riwaya ya *Tumaini* (2006) anajuta kwa sababu ya malezi waliyompa mwanao. Anasikitika sana mwanawe anapopigwa risasi kwenye muundi kwa sababu ya wizi. Majuto anapelekwa hospitali na kulindwa na askari wawili

ili asitoroke. Anapotoka hospitalini anafungwa kifungo cha miaka minne jambo ambalo linamsononesha sana mamake. Kwa upande mwingine, Chifu Andrea, babake Majuto anakataa kwenda kumwona hospitalini kwa sababu ya kujuta kwa kumdekeza mwanawe. Mwandishi anaeleza:

> Bi. Selina alifananisha sauti ya mwimbaji huyo na ile ya mumewe. Alihisi kama yeye ndiye aliyekuwa akimwimbia Majuto mle hospitalini, kisha kumkumbusha kuwa hakuyatia maanani yale waliyokuwa wakimwambia. (Momanyi: 145)

Suala la wazazi kujuta baada ya kutumia mbinu fulani za malezi ni la kiuhalisia. Bossio (2018) anaeleza visa vya wazazi ambao hujuta kwa sababu ya kutumia mbinu za malezi ambazo huwadhuru katika maisha ya baadaye. Kwa mfano, mzazi mmoja anajuta kwa kuwa mkali kupita kiasi kwa mtoto wake na kutomwelekeza vizuri. Jambo hili linamfanya mtoto huyo kuwa mtovu wa nidhamu.

### 4.9 Watoto kutamauka

Kwa mujibu wa Panagloti, Gooding na Tarrier (2012), kutamauka ni hali ya kiakili ambayo humfanya mtu kukosa matumaini katika maisha na inaweza kuathiri jinsi anavyojichukulia yeye mwenyewe na anavyochukulia ulimwengu mzima. Kulingana na Hudson (2013) watoto hukosa matumaini maishani kwa sababu ya kukosa malezi mema. Anasema kuwa wazazi wanapowatelekeza watoto katika umri mdogo huwafanya wakose matumaini maishani. Hudson (keshatajwa) anaendelea kueleza kuwa wazazi wanaotenga muda mwingi kwa watoto wao, huwapa watoto matumaini hata wanapokumbana na changamoto za maisha. Hivyo, wazazi wanafaa kujihusisha katika malezi ya watoto ili kuwapa moyo wa kutia bidii katika kila jambo.

Watoto katika riwaya teule wametamauka kwa sababu ya mbinu za malezi wanazotumia wazazi wao. Utamaushi huu hutokea kwa wazazi ambao wanatumia mbinu ya kimabavu kuwalea watoto na mbinu ya kutojihusisha. Katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004), Yasibu anatamauka baada ya kupata ujauzito. Baada ya kujifungua, babake Bwana Mashaka anakosa kujihusisha kwa malezi yake na kumtekeleza. Jambo hili linamtamausha na kuamua kujiua lakini kwa bahati nzuri anapatana na Mzee Mafusho ambaye anamnusuru. Mwandishi anaeleza:

> Kwa vyovyote vile sharti nitekeleze lililonileta huku msituni, alijiambia Yasibu, akisimama shinani pa mkuyu, yu tayari kuuparaga hadi kileleni ajirushe na kuyakata maisha yake. Mara alisikia sauti ya mzee Mafusho akiimba kwamahadhi ya kupendeza, akiwa mbali shambani, akijipa ari ya kuendelea kung'ang'ana na jembe. (Omar: 94)

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), Tumaini anakosa matumaini nyumbani kwao. Hii ni baada ya babake kupanga njama ya jinsi atakavyopashwa tohara na kuolewa. Ukosefu wa matumaini nyumbani kwao unamfanya Tumaini kutoroka kwao usiku wa manane bila kuhofia usalama wake. Anabeba kifurushi cha nguo pamoja na vitabu vyake vya shule kwa kuwa tumaini lake lilikuwa kuendelea kusoma. Anaenda kwa mamake mdogo Bi. Halima kwani yeye angemwelewa na kumpa matumaini katika maisha. Mwandishi anaeleza:

> Hakutaka kutazama nyuma kwani nyumba yao ilimkumbusha mengi machungu. Alifululiza kwa mchapuko kwenye ujia ulioelekea kulia na papo hapo alikutana na simba, mbwa wao. (Momanyi: 1)

Zena pia ni mhusika aliyetamauka. Tofauti na Tumaini, Zena hakuweza kujinasua kutoka kwa utamaduni uliomkandamiza na kuvunja matumaini yake katika maisha. Zena alikataa kuolewa lakini wazazi wake wakamuoza kwa lazima. Wazazi wa Zena waliwatuma vijana ambao walimbeba na kumpeleleka kwa Mzee Chumo kama mke wa

nne. Zena aliwaita wapita njia wamsaidie lakini hakuna aliyemsaidia. Hivyo, aliolewa na mzee asiyempenda na kukatiza elimu yake. Tumaini anawaza:

> Juhudi za Zena kujiopoa ziliambulia patupu kwani vijana hao mabarubaru walimshinda nguvu. Lililomshtua na kumshangaza Tumaini ni jinsi wapita njia walivyokataa katakata kumsaidia Zena wakati alipowaita huku akilia waende kumsaidia...Alimhurumia Zena ambaye alitawishwa, akaingizwa unyagoni na kufunzwa kunga za utu uzima. Haya yalimfanya akose kwenda shule ili asubiri kuolewa na Mzee Chumo. (Momanyi: 50)

Mutani (2019) katika gazeti la *Taifa Leo* anaeleza kisa cha vijana wawili katika kaunti ya Kakamega ambao wanamuua kijana mwenzao na baadaye wanaamua kujiua. Anaeleza kuwa sababu ya vijana hawa kufanya kitendo hicho ni kusukumwa na hali katika jamii. Anaeleza kuwa watoto wengi hukua wakiwa watupu kiroho hivyo hujipata wamevunjika moyo au kutamauka maishani. Wengine huona ni heri wafe au waondoe mtu ambaye ni kikwazo katika maisha yao. Nchini Kenya pamekuwa na visa vingi vya watoto kujiua na kuwaua wenzao. Kulingana na ripoti ya Chepkoech (2019) katika gazeti la *Daily Nation*, visa hivi vinatokana na ukosefu wa mshikamano kati ya watoto na wazazi, mizozo ya kinyumbani na upweke nyumbani. Anaeleza kuwa wazazi hawatengi muda wa kuwashauri watoto wao. Hivyo, watoto wanapokumbana na changamoto za maisha wanashindwa kustahimili na hivyo kujiua. Visa hivi vinalingana na kisa cha Yasibu katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) ambaye anamua kujitoa uhai baada ya wazazi wake kukosa kumsaidia. Anavunjika moyo na kuamua kujiua lakini Mzee Mafusho anamnusuru.

### 4.10 Hitimisho

Katika sura hii athari zinazotokana na mbinu zinazotumiwa kuwalea watoto zimeelezwa. Imebainika kuwa mbinu mbalimbali za malezi huwa na athari tofauti kwa watoto. Kila mbinu huwa na athari yake kwa watoto. Mbinu hizi huwaathiri watoto kwa njia nzuri au mbaya. Baadhi ya athari zinazojitokeza katika sura hii ni; watoto kuambukizwa magonjwa ya zinaa kwa mfano, UKIMWI, watoto kuwa na utovu wa nidhamu, wazazi kujuta, matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto, ndoa za mapema kwa watoto wa kike, Watoto kutamauka, kuzorota kwa elimu, na maendeleo ya elimu wazazi wanapotumia mbinu inayofaa kuwalea watoto.

Athari hizi zimechunguzwa kwa kina ikibainika kuwa walezi wengi wanatumia mbinu zisizofaa kuwalea watoto ambazo huwaathiri watoto katika maisha. Walezi wengi huongozwa na utamaduni na tamaa katika kuwalea watoto wao bila kuwazia jinsi maisha ya watoto wao yatakavyokuwa baadaye.

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya uhalisia. Mhimili wa nadharia hii uliotumika ni: Kazi ya msanii inapaswa kuonyesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao, jinsi wanavyohisi na kutenda wanapokumbana na hali fulani.

Sura inayofuata itashughulikia hitimisho la utafiti huu. Itahusisha muhtasari wa sura, matokeo ya utafiti kulingana na malengo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 5.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa utafiti mzima kuanzia sura ya kwanza hadi ya tano. Vile vile, Imeshughulikia matokeo ya utafiti ambayo yalitokana na uchanganuzi wa malengo ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti. Mbali na hayo, sura hii imeeleza changamoto zilizomkumba mtafiti wakati wa utafiti pamoja na mapendekezo ya utafiti. Mchango wa utafiti huu pia umeelezwa.

## 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza taswira ya malezi ya watoto katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006). Katika utafiti huu, mtafiti alijikita katika kuchunguza mbinu za malezi zinazotumiwa na walezi, asasi na hali zinazochangia malezi ya watoto na athari zinazotokana na mbinu za malezi. Ili kufanikisha utafiti huu, mihimili ya nadharia ya uhalisia ulitumiwa kuchunguza malengo ya utafiti.

Lengo la kwanza lilikuwa kuchunguza mbinu na aina ya malezi yanayotumiwa na walezi katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006). Lengo hili limetimizwa kwa kuwa utafiti huu umebainisha mbinu mbalimbali zinazotumiwa na walezi kuwalea watoto wao. Baadhi ya mbinu zilizobainishwa ni mbinu ya kimabavu ambapo mzazi humdhibiti mtoto kwa ukali na huonyesha mapenzi kidogo kwa watoto. Watoto wanapokosea pia hupewa adhabu bila kuongozwa. Mbinu nyingine ni mbinu ya kimamlaka ambapo wazazi huwapa mwelekeo bora na kuwashirikisha watoto kikamilifu

katika malezi. Mbinu ya kudekeza pia imeelezwa. Katika mbinu hii, wazazi huepuka migogoro yoyote na watoto na huwapenda kupita kiasi. Imebainika kuwa kuna wazazi wanaotumia mbinu ya kutojihusisha ambapo wazazi huepuka majukumu yao na kuwatelekeza watoto. Utafiti huu pia umedhihirisha kuwa kuna wazazi wanaotumia mbinu ya ushirikiano kuwalea watoto wao.

Lengo la pili ni kueleza asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto. Utafiti huu umetimiza lengo hili kwa kuonyesha asasi na hali hizo katika riwaya teule. Asasi na hali hizi ni pamoja na asasi ya utamaduni, asasi ya elimu, asasi ya familia na ndoa, hali ya jinsia na uana, hadhi na cheo cha wazazi, taasubi ya kiume, hali ya uchumi, hali ya ulevi na tamaa na ubinafsi wa wahusika

Lengo la tatu ni kueleza athari zinazotokana na mbinu za malezi wanazotumia walezi. Lengo hili pia lilitimizwa. Athari zilizobainishwa ni utengano katika familia, utovu wa nidhamu kwa watoto, mimba na ndoa za mapema kwa wasichana, Watoto kukumbwa na maradhi, kuzorota kwa elimu, watoto kufungwa jela, majuto kwa wazazi na pia watoto kutamauka.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia iliyoasisiwa na Gustave Flaubert (1850). Mihimili ya nadharia ya uhalisia ilitumiwa kufanikisha utafiti huu. Mihimili ya nadharia hii iliyotumiwa ni: Usawiri na uelezaji wa hali kwa kuzingatia uhakika wa maisha kwa maana ya uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Mhimili huu umetumiwa kuonyesha jinsi mwandishi anavyotoa malighafi katika jamii anapoandika kazi yake. Mbinu za malezi zilizotumiwa na wahusika katika riwaya teule zinalingana na mbinu wanazotumia walezi katika jamii. Mhimili wa pili ni wahusika huwa halisi na lugha

wanayotumia huwa rahisi na inayoeleweka. Mhimili huu umeonyesha kuwa wahusika ambao wametumiwa na mwandishi ni wa kweli na wanapatikana katika jamii. Mhimili wa tatu ni kuwa kazi ya msanii inapaswa kuonyesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao. Mhimili huu umeonyesha jinsi watoto wanavyohisi na kutenda wanapokosa malezi mema. Kwa mfano, watoto hutamauka, wengine hutoroka nyumbani ili kuepuka madhila wanayopitia nyumbani, watoto hukosa elimu bora na wengine afya yao huzorota.

Sura ya kwanza iliangazia suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia pamoja na mbinu za utafiti.

Sura ya pili ilichunguza mbinu mbalimbali za malezi katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006). Mbinu za malezi ya watoto zilizobainishwa katika sura hii ni: Mbinu ya kimabavu, mbinu ya kimamlaka, mbinu ya kudekeza, mbinu ya kutojihusisha pamoja na mbinu ya ushirikiano. Utafiti huu umeonyesha kuwa kila mzazi huwa na mbinu mahsusi ya kuwalea watoto wake. Mbinu hizi za malezi ya watoto huweza kutofautiana hata katika familia moja pale ambapo mzazi wa kiume hutumia mbinu tofauti na mzazi wa kike na migogoro ya malezi hutokea.

Sura ya tatu ilichunguza asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto katika riwaya teule. Katika riwaya hizi, asasi na hali mbalimbali zimetambuliwa kwa mfano, asasi ya utamaduni, asasi ya familia na ndoa, asasi ya elimu, hali ya jinsia na uana, hali ya hadhi na cheo cha wahusika, hali ya uchumi na hali ya ulevi. Imebainika kuwa,

utamaduni ni mojawapo ya asasi zinazoathiri mbinu zinazotumiwa kuwalea watoto kwa kiwango kikubwa katika riwaya teule.

Sura ya nne ilichunguza athari za mbinu za malezi katika riwaya teule. Athari hizi ni utengano katika familia, watoto kukumbwa na maradhi, mimba na ndoa za mapema kwa wasichana, wizi na watoto kufungwa jela, matumizi ya dawa za kulevya, watoto kutamauka na utovu wa nidhamu miongoni mwa watoto.

Sura ya tano ni hitimisho la utafiti. Katika sehemu hii, Utangulizi umetolewa pamoja na muhtasari wa utafiti. Muhtasari huu umeelezwa kulingana na malengo na maswali ya utafiti. Vile vile, sura hii imeeleza matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi.

### 5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza taswira ya malezi ya watoto katika riwaya za *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006). Utafiti huu uliongozwa na mihimili ya nadharia ya uhalisia. Uchanganuzi wa riwaya hizi teule umeonyesha kuwa suala la malezi ya watoto ni suala nyeti katika jamii na linahitaji kuchukuliwa kwa uzito na wanajamii. Hii ni kwa sababu watoto wasipopata malezi mema hukumbwa na matatizo mbalimbali ambayo huwaathiri katika maisha ya baadaye.

Utafiti huu pia umeonyesha kuwa malezi ya watoto wa kike ni tofauti na ya watoto wa kiume katika familia nyingi. Kwa mfano, watoto wa kiume hupata elimu katika familia nyingi na watoto wa kike hupashwa tohara na kuolewa. Suala hili linatokana na utamaduni ambao unamkandamiza mtoto wa kike. Vilevile, utafiti huu umeonyesha kuwa

ushirikiano katika malezi ni jambo muhimu katika familia yoyote. Wazazi wasiposhirikiana katika malezi watoto ndio huangamia.

Mbali na hayo, uchunguzi huu umeonyesha watoto kama viumbe dhaifu ambao wanafaa kuongozwa na kuelekezwa mara kwa mara. Kulingana na utafiti huu, wengi wa watoto wanaokosa nidhamu na kutumia dawa za kulevya ni wale ambao wamekosa mwongozo kutoka kwa wazazi wao. Pia, utafiti huu umebaini kuwa kutamauka kwa watoto hutokana na mbinu za malezi wanazotumia walezi. Pia, imebainika kuwa wazazi wanapokosa kuwaelewa watoto wao, kuwaelekeza na kuwasamehe wanapokosea, watoto hukosa matumaini katika maisha na kutafuta suluhu kwa wenzao. Wengine huishia hata kujitoa uhai. Aidha, imegunduliwa kwamba wazazi wanapotumia mbinu zinazofaa kuwalea watoto wao, watoto hukua bila tatizo lolote na kufanikiwa vyema maishani. Watoto katika familia hizi, hufanikiwa katika elimu na wazazi hufurahia ufanisi wao ikilinganishwa na watoto ambao hulelewa kwa kutumia mbinu zisizofaa. Wazazi wanaotumia mbinu zisizofaa hujuta baadaye.

## 5.4 Mchango wa utafiti

Kutokana na utafiti huu, ni wazi kwamba fasihi huangazia masuala yanayokumba jamii. Watunzi wa riwaya hujikita katika mambo halisi yanayotokea katika mazingira yao. Utafiti huu umeonyesha kuwa malezi ya watoto ni suala muhimu na linahitaji kushughulikiwa. Hii inatokana na ukweli kwamba watoto ndio msingi wa kila jamii. Jamii yoyote haiwezi kuendelea pasipo watoto kupewa malezi mema.

Utafiti huu utawasaidia walezi na wanajamii katika kuwalea watoto. Pia, utawasaidia walezi ambao wamepuuza majukumu ya malezi ya watoto kwa kuwabainishia athari

zitokanazo na kutowajibika katika malezi. Utafiti huu pia una mchango mkubwa kwa wanajamii hasa wakati huu ambapo watoto wengi wameonyesha kutamauka na kujitoa uhai. Wazazi wanafaa kuelewa kuwa watoto wanahitaji kuongozwa na kuelekezwa. Watoto pia wanafaa kuhimizwa kuzungumza na wazazi wao wanapokumbana na changamoto za maisha bali sio kujitoa uhai ama kuwatoa wenzao uhai.

Vilevile, utafiti huu utawasaidia watoto kujikwamua kutoka kwa tamaduni ambazo zinawakandamiza na jambo lolote ambalo linatinga juhudi zao za kuendelea na masomo.

Utafiti huu pia utatumiwa kuwaelimisha walezi na wanajamii kuhusu athari za mbinu za malezi zisizofaa na kuwasaidia kubadilisha mbinu zao za malezi. Kwa kifupi, utafiti huu utakuwa kama kifungua macho kwa wazazi ambao wamekuwa wakipuuza malezi ya watoto wao. Pia, utawafungua macho wazazi ambao huwabagua watoto katika malezi kwa misingi ya kijinsia. Watoto wa kike wataweza kupata elimu kama wenzao wa kiume. Vilevile, utafiti huu utawasaidia wazazi ambao wanashikilia tamaduni ambazo zimepitwa na wakati na hazifai. Utafiti huu utawawezesha kuwalinda watoto wao bila kuongozwa na mila na desturi zinazowatamausha na kuzorotesha maendeleo ya elimu ya watoto.

### 5.5 Changamoto za Utafiti

Shughuli ya utafiti huu kuhusu taswira ya malezi ya watoto haikuwa rahisi. Utafiti huu ulifanywa maktabani. Shughuli hii ilikumbwa na changamoto mbalimbali. Mojawapo ya changamoto hizi ni ukosefu wa vitabu vya Kiswahili vinavyoeleza kuhusu malezi ya watoto. Tatizo la uhaba wa vitabu lilimfanya mtafiti kutafsiri maneno mengi kutoka kwa lugha ya Kingereza. Shughuli hii ya kutafsiri vitabu vya kingereza ilichukua muda mwingi.

## 5.6 Mapendekezo

Utafiti huu ulishughulikia suala la malezi ya watoto katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006). Mtafiti alionyesha mbinu mbalimbali za malezi zinazotumiwa na wazazi, asasi na hali zinazochangia katika matumizi ya mbinu hizo na athari zitokanazo na mbinu za malezi.

Vilevile, utafiti unaweza kufanywa wa kulinganisha maudhui na mbinu za kimtindo katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2004) na *Tumaini* (2006). Utafiti wa nyanjani pia unaweza kufanywa kuhusu malezi ya watoto kama chanzo cha utamaushi miongoni mwa watoto hasa wakati huu ambapo watoto wengi wameonyesha kutamauka maishani. Malengo ya utafiti huu yalichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya uhalisia. Aidha, utafiti zaidi unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia zingine.

## 5.7 Hitimisho

Kwa kifupi, utafiti huu umechunguza suala la malezi ya watoto katika riwaya ya *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004). Mtafiti ameeleza kwa kina malengo ya utafiti huu ambayo ni: Kubainisha mbinu za malezi katika riwaya teule, kueleza asasi na hali zinazochangia katika malezi ya watoto pamoja na kubainisha athari zitokanazo na mbinu za malezi. Mihimili ya nadharia ya uhalisia imetumiwa kuchanganua malengo na maswali ya utafiti. Utafiti huu ulifanywa maktabani na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Aidha, mchango na matokeo ya utafiti huu pamoja na mapendekezo ya utafiti yameelezwa. Utafiti huu ulikumbwa na changamoto mbalimbali kama vile ukosefu wa vitabu vya Kiswahili vya kuchunguzwa. Mtafiti alitafsiri vitabu vya Kingereza jambo ambalo lilichukua muda mwingi.

## MAREJELEO


Amalemba, R. (2017). "Man Who Abandoned Disabled Children Ordered to Pay Upkeep."In: *The Standard*, 6/3/2017 (uk. 24).

Ashiono, B. (2013). The Role of Parenting Style in Enhancing or Hindering Children Performance in Pre-school. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Awasthi, D. (2017). "Uninvolved Parenting Style. Traits and Effect on Children." Imepakuliwa: www.momjuction.com/articles/how-does-uninvolved-parenting-affect-your-child, 20/2/2019.

Anzilotti, A. (2017). "Talking to your Kids about STDs." Imepakuliwa: https://kidshealth.org>parents>stds, 14/7/2019.

Bancroft, L. na Silverman, J. (2016). "The Batterer as Parent: Assessing the Impact of Domestic Violence on Family Dynamics." Imepakuliwa: https://psycnet.apa.org, 10/4/2019.

Barton, A. na Kirtley, M. (2012). "Gender Differences in the Relationship Among Parenting Styles and College Students Mental Health." In: *Journal of American College Health*, 60 (1) pp: 21-26.

Baumrind, D. (1991). "The Influence of Parenting Styles on Adolescence Competence on Substance Use." In*: Journal of Early Adolescence*, 11, pp: 56-57.

Baumrind, D. (1968). "Authoritarian v. Authoritative Parental Control. Parental Authority Questionnaire." In: *Journal of Personality Assessmeent*, pp: 116-119.

Berk, L. (2016). *Development Through Lifespan*. (4th ed). Boston: Allyn and Boston.

Bett, K. (2016). "Man Charged for Forcing his Daughter to be Married." In: *Daily Nation*, 12/5/2016 (uk. 25).

Bossio, A. (2018). "Parents Reveal What They Regret Most About Raising Their Children." Imepakuliwa: https://www.healthy way.com, 10/7/2019.

Brooks, J. (2012). *The Process of Parenting*. (9th ed). Mc Graw-Hill Higher Education.

Brown, S. (2018). "What are the Causes of Teenage Pregnancy." Imepakuliwa: https://www.livestrong.com, 24/6/2019.

Brown, D. (2009). "Social Class and Status." In: *Consise Encyclopedia of Pragmatics*, pp: 953-978.

Buddy, T. (2018). "How Drinking Fathers Affect Children Development." Imepakuliwa: https://verywellmind.com, 17/6/2019

Cherry, K. (2012). Parenting Styles: The Four Styles of Parenting. Imepakuliwa: http//:psychology.about.com, 14/5/2017.

Cherry, K. (2018). Parenting Styles: How Each Style Impacts Children. Imepakuliwa: http://www.explorepsychology.com/parenting, 10/3/2019.

Cherry, K. (2019). "Why Parenting Matter When Raising Children". Imepakuliwa: https://www.verywellmind.com, 25/6/2019.

Cherry, K. na Steven, G. (2018). What is Authoritarian Parenting? Imepakuliwa: www.verywellmind.com/what-is-authoritarian-parenting, 10/3/2019

Chepkoech, A. (2019). "Answers to increased Suicide and Murder Cases." In: The *Daily Nation*, 16/3/2019.

Claire, C. (2015). Class Differences in Child Rearing are on the Rise. Imepakuliwa: https://cepa.stanford.edu>news>class-differences-in-child-rearing-are-on-the-rise, 8/4/2019.

Conlon, B., Ginn, A. na Lounsbury, D. (2015). "The Role of Parenting in Home Environment among Underserved Youth." In: *Childhood Obesity*," 11 (4),pp: 394-405.

Craig, L. (2006). "Does Fathers Care Mean Fathers Share? A comparison of how Mothers in Intact Families Spend Time with Children." In: *Gender and Society*, 20 (2), pp: 259-281.

Crow, S. (2018)."20 Biggest Regrets Nearly every Parent Has."Imepakuliwa: https:/bestlifeonline.com>parenting, 30/6/2019.

Cummings, E. na Davies, P. (1994). "Marital Conflict and Child Adjustment: An Emotional Security Hypothesis." In: *Psychology Bulletin*, 116 (3) pp: 37-411.

Darling, N. (2014). *Authoritative Versus Authoritarian Parenting Style*. Psychology Today, Sussex Publishers.

Deater-Deckard, K., Ivy, L. na Petrill, S. (2006). "Maternal Warmth Moderates the Link between Physical Punishment and Child Externalizing Problems: A Parent-offspring behaviour getting annalysis." In: *Parenting Science and Practice*, 6 (1) pp: 59-78.

Dinorah, G. (2015). "Relationship between Parenting Styles and Sexual Risk Behaviour in Adolescents." Imepakuliwa: www.medinstitute.org, 20/6/2019.

Downey, M. (2015). "Aletter from a Teacher to Parents. I can't do it Alone." Imepakuliwa: https://get schooled.blog.ajc.com.a-letter-from-a-teacher-to-parents-I-can't-do- it- alone,6/4/2019.

Eagleton, M. (1986). *Feminist Literary Theory*. Newyork: Basil and Blackwell.

Elkins, C. (2018). Alcoholism Defination, Stages, Types and Diseases. Imepakuliwa: https://www.drugrehab.com.alcohol, 15/8/2019.

Eugene, R. (2016). *Family Asset*: *Understanding and Addressing Child Marriage in Turkana.* Nairobi: United Nations Children Fund (UNICEF).

Fabrizao, Z. (2017). Parenting and Development. Imepakuliwa: https://psychcentral.com, 9/4/2019.

Francese, J. (2018). Parenting Styles in Relation to Social Economic Status, Education and Generation.Imepakuliwa:htttp://digitalcommons.sacredheart.edu, 7/4/2019.

Getao,K.(2016).Parenting the Kenyan Way.Imepakuliwa: https://www.nation. co.ke/ lifestyle/saturday/flakes-parenting-the-kenyan-way, 28/2/2019.

Hare, A.Marston, E. na Allen, J. (2011). "Maternal Acceptance and Adolescence Emotional Communication. A Longitudinal Study." In: *Journal of Youth and Adolescence*, pp: 744-751.

Hegel, G. (1979). *Introduction to Aesthetics*: Oxford:Clarendon Press.

Hirshi, T. (2009). *Causes of Delinquency*. Berkeley: University of California Press.

Hudson, J. (2013). Parent-Child Relationship in Early Childhood and Development of Anxiety and Depression. Imepakuliwa: https://www.child.encyclopedia.com, 20/6/2019.

Johnson, S. (2016). "Parenting Styles and raising Delinquent Children. Responsibility of Parents in Encouriging Violent Behavior." In: *Forensic Research and Criminology International Journal*, 3 (1) pp: 320-325.

Julie, C. (2017). "Role of Culture in influencing Parenting Styles." Imepakuliwa: http://www.livestrong.com, 6/5/2019.

Kamau, L. (2016). Relationship Between Family Background and Academic Performance of Secondary School Students: A Case Study of Siakago Division, Embu County. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Karanja, D. (2008). Usawiri wa Maswala Ibuka katika Hadithi za Watoto. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kavuria, P. (2008). Dhuluma Dhidi ya Watoto katika Riwaya Teule za Fasihi. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kearns, K. (1996). *Ninteeth-Century Realism*: Through the looking-Glass. Cambridge: Cambridge University Press.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: East African Publishers.

Kinoti, M. (2017). "Education is a Key Driver in Ending Child Marriages." In: *Daily Nation*, 14/9/2017. ( uk.16)

Kipyegon, H. (2017). "Influence of Parenting to Child Education." Imepakuliwa: https://www.kenyaplex.com>resources, 30/6/2019.

Kombo, M. (2015). Influence of Involvement in Education on Performance of Urban Refugee Pupils in Public Primary Schools in Kamukunji District, Nairobi County, Kenya. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu chaNairobi. (Haijachapishwa).

Kwamboka, E. (2018). "Parenting Contributing to Unrest in Schools." Imepakuliwa: https://www.standardmedia.co.ke, 25/6/2019.

Larkin, M. (1977). *Man and Society in the Ninteenth Century Realism*. London: Macmillan.

Late, A. (2015). "To End the AIDS Epidermic start Focussing on Adolescent." Imepakuliwa: https://www.avert.org>hiv-social-issues, 23/6/2019.

Lawall, S. na Maynard, M. (1984). *The Norton Anthology of World Literature*. London: Norton and Company Ltd.

Lukacs, G. (1972). *The Meaning of Contemporary Realism*. London: Merlin Press.

Maccoby, E. na Martin, J. (1983). "Socialization in the Context of Family: Parental Child Interaction." In: *Handbook of Child Psychology,* vol 4, pp:1-101.

Maigallo, A. (2015). Parenting Styles Used by Parents in Boarding Schools in Kiambu District. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Chuka. (Haijachapishwa).

Mavisi, R. (2007). Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Kazi ya Zainab Burhani. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mayieka, N. (2015). Maswala Ibuka katika Riwaya za Kisasa. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mbatia, M. (1998). Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona* na *Mzingile*. Katika *Mulika* namba 24, TUKI. Kur 1-11.

Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*: Nairobi: Standard Textbook &Graphics and Publishing.

Mc Kinney na Renk, K. (2008). "Differential Parenting between mothers and Fathers: Implication for late Adolescence." In: *Journal of Family Issues*, 29(6), pp: 806-827.

Miller, C. (2015). Class Differences in Child Rearing are those on the Rise. Imepakuliwa: https://cepa.stanford.edu>news>class-differences-in-child-rearing-are-on-the-rise, 8/4/2019.

Mohammed, A. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Momanyi, C. (1998). Usawiri wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama Inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Momanyi, C. (2006). *Tumaini*. Nairobi: Vide-Muwa.

Mowin, A.(2018).Parenting Styles from Around the World. Imepakuliwa: http://www.verywellfamily.com, 8/4/2019.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*: Nairobi: E.A.E.P.

Muiruri, P. (2014). "How can Parents Marry Different Parenting Styles?" In: *The Standard Digital*, 29/3/2014. (uk. 5)

Mulili, W. (2014). Utamaushi wa Wahusika wa Kike katika Riwaya ya *Kiu* na *Mwisho wa Kosa*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Munyoki, J. (2015). Familia za Kiafrika katika Njia Panda: Mitagusano na Changamano za Usasa katika *Mhanga Nafsi Yangu*. S.A. Mohammed. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Murphy, S. na Johnson, S.(2011)."The benefit of Long-lens Approach to Leader Development: Understanding the Seeds of Leadership."In: *The Leadership Quarterly*, 22(3), pp: 459-470.

Mutani, B. (2019). "Wazazi Wasipowaelekeza Watoto Upotovu Utazidi."Imepakuliwa: https://www.taifaleo.nation.co.ke, 14/7/2019.

Muyalo, J. (2017). Parents Related factors influencing Learners Academic Performance in Kenya Certificate of Secondary Education in Igembe North Sub-county Meru, Kenya. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mwanjala, C. (2015). Determinants of Juvenille involvement in Criminal Behaviour in Taita Taveta Taveta County, Kenya. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Hijachapishwa).

Mwenesi, S. (2016). 6 Ways that Parenting Styles have Changed over Time. Imepakuliwa: https://www.afromum.com, 29/2/2019

Naliaka, E. (2012). Uhakiki wa Hali ya Vijana katika Riwaya ya *Vipanya vya Maabara*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ngwiri, L.(2008).*Powerful Parenting*. What every Parent should know. Nairobi: Queenex Holding Ltd.

Njogu, S. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ochieng, O. (2019). "How Modern Parents are Raising Weak Children." In: *The Daily Nation*, 4/5/2019.

Njoka, S. (2017). "Siblings Left to Die in the Tank Still Alive." In: *People Daily*, 13/9/2017 (uk.8)

Oburu, P. (2011). Attributions and Attitudes of Mothers and Fathers in Kenya. Parenting,11(2-3).Imepakuliwa:152-162.doi:10.1080/15295192.2011.585561, 20/3/2019

Ojiambo, B. (2019). "Causes of Teenage Pregnancies in Kenya." Imepakuliwa: https://www.zakenya.com>education, 15/6/2019.

Omar, L. (2004). *Dunia Mashaka Makuu*. Nairobi: City Book Publishers.

Ombere, J. (2014). Drugs and Substance Abuse Among Secondary School Students in Embakasi District, Nairobi County. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Omondi, A. (2015). Factors Influencing Influx of Street Children in Kitale Town, Trans Nzoia County, Kenya. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Onyango, K. na Muchiri, G. (2016). *Understanding Gender Based Violence*. Nairobi: Community Based Education.

Osore, M. (1994). Uhakiki wa Kiisimu wa Riwaya za Suleiman Mohammed. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Panagloti, M., Gooding, P. na Tarrier, N. (2012). "Hopelessness, Defeat and Entrapment in Posttraumatic Stress Disorder: Their Association with Suicidal Behavior and Severity of Depression." In: *The Journal of Nervous and Mental Disease*, 200 (8), pp: 676-683.

Preston,N.(2016).Signs of Narcissistic Parent. Imepakuliwa: https://www. psychology today.com, 3/ 4/2019.

Reese. F. na Roosa, M. (1991). "Early Adolescence Self Report of Major Life Stresses and Mental Health Risk." In: *Journal of Early Adolescence*. vol 11, pp: 363-378

Santrock, J. (2006). *Lifespan Development*. (10th Ed). New York: Mc Graw-Hill

Santrock, J. (2007). *A Topical Approach to Life Span Development*. (3rd Ed). New York: Mc Graw- Hill.

Scroeder, R. na Mowen, T. (2014). "Parenting Style." In: *Transitions and Delinquency Youth and Society*, 46 (2), pp: 228-254.

Shabas, N. (2016). "Relationship between Parents and Pre-School Age Children Attending Kindergartens." In: *Journal of social and behavioural sciences*, pp: 269-273

Sharma, M. (2015). "Substance Abuse in Adolescents: Implication for Research and Practice." In: *Journal of Alcohol and Drug Education*, pp: 321-330.

Simiyu, W. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi*. Nairobi: Mwanza. Serengeti Bookshop.

Tomison, A. (1996). "Child Maltreatment and Substance Abuse." Discussion Paper number 2. National Child Protection Clearing House, Melbourne: Australian Institute of Family Studies.

Traore, P. (2008). Suala la Familia katika Riwaya Sita za Said Ahmed. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

UNICEF (2017). *Mid-year Humanitarian Situation Report Kenya*. Nairobi: United Nations Children Fund.

Wachira, G. (2017). "Why my Daughter Took a Unique Path to Womanhood." In: *People Daily*, 29/11/2017. (uk. 21)

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wako, A. (2017). "Child Marriage Rampant in Kenya due to Poverty and Gender Inequality." In: *The Star*, 11/12/2017.

Wambui, R. (2015). "Parenting in a Big World." In: *Daily Nation*, 30/10/2015. (uk. 20).

Wamitila, K. (2005). *Uhakiki wa Fasihi, Nadharia na Misingi yake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wangu, J. (2017). "Two Women Charged with Neglect." In: *Daily Nation*, 14/9/2017. (uk. 23)

Wangui, C. (2017). Effect of Parental Alcoholism on Student Education in Public Secondary Schools. A Case Study of Kangema Sub-County- Muranga. Tasnifu ya M.A Kenya Methodist University (Haijachapishwa).

Wanjohi, A. (2007). The Role of Fathers in Upbringing their Children Among the Maasai People of Kenya. Imepakuliwa: https:/ssrn.com, 10/9/2016.

Wanyama, M. (2015). "Parenting Crisis: What is the Way Forward." In: *The Star*, 27/10/2015. (uk.15).

Wawira, E. (2013). Parenting Styles on Academic Performance of Adolescent in Secondary Schools. A case Study of Manyatta Constituency, Embu County. Tasnifu ya M.A: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Webukha, W. (2014). Maudhui ya Matumaini Miongoni mwa Wahusika katika Riwaya Teule za Kiswahili.Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Winter, A. (2014). "Influential factors of parental Substance and Alcohol Abuse on Children Academic Achievement."In: *Research Journal*, pp: 1-12.

Yaffe, Y. (2018). "Establishing Specific Links Between Parenting Styles and the Anxieties in Children: Separation, Social and School." In: *Journal of Family Issues*, 39 (5): pp: 1419-1437.

Zombwe, P. (2008). *Hata Maskini wana Haki za Binadamu*. Dar es Salaam: HakiElimu Working Papers.

Zubaida, A. (2009). "Indiscipline and Management Techniques: Acase study of aspecial Education School in Kano state." In: *The Journal of National Council for Exceptional Children*, 11(2) pp: 455-463.